

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA NANE

Kikao cha Kumi na Tano – Tarehe 12 Februari, 2010

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua

KIAPO CHA UAMINIFU

Waheshimiwa Wafuatao waliapa Kiapo cha Uaminifu:-

Mhe. Ismail Jussa Ladhu

Mhe. Janet Zebedayo Mbene

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Mheshimiwa Mbunge anayeuliza swali, naomba kwa niaba yenu kwa sababu ya tukio lililotokea sasa hivi kuwapongeza sana Mheshimiwa Jussa na Mheshimiwa Mbene kwa kupokelewa leo hapa kuwa Wabunge wenzetu. Nyote wawili nakutakieni shughuli njema na nina hakika tutapata ushirikiano wenu katika kuiendeleza nchi yetu. Karibuni sana.

Swali la kwanza kama kawaida linaelekezwa Ofisi ya Waziri Mkuu, linaulizwa na Mheshimiwa James Lembeli – Mbunge wa Kahama.

Na. 168

**Mgodi wa Buzwagi Kusaidia Kutengeneza
Barabara za Mji wa Kahama**

MHE. JAMES D. LEMBELI aliuliza:-

Kwa kuwa, kabla ya kuanza kwa ujenzi wa mgodi wa dhahabu wa Buzwagi matumizi ya barabara katika Mji wa Kahama yalikuwa ya wastani, hivyo Halmashauri hiyo ilimudu kufanya matengenezo na ukarabati wa kawaida; na kwa kuwa shughuli za mgodi wa Buzwagi zimesababisha ujio wa magari mengi makubwa kwa madogo na kusababisha uharibifu mkubwa

wa barabara za Kahama Mjini; na kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Kahama haina uwezo wa kukarabati barabara hizo kila mara:-

Je, Serikali iko tayari kusaidia Halmashauri ya Wilaya ya Kahama kuibana Kampuni ya Buzwagi kufidia gharama za matengenezo ya barabara za Halmashauri ya Kahama?

NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU -TAMISEMI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha, naomba kuungana na wewe kuwapongeza sana ndugu zetu hawa, Mheshimiwa Janeth Mbene na Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu kwa kuapishwa hapa baada ya kuteuliwa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa James Lembeli - Mbunge wa Kahama kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli matumizi ya barabara katika Mji wa Kahama yameongezeka kutokana na kuanzishwa kwa mgodi wa Dhahabu wa Buzwagi ambao umevuta wafanyabiashara na wananchi wengi kwenda Kahama kwa ajili ya biashara na ajira. Mgodi una magari mengi yanayosafirisha watumishi na kutafuta mahitaji Mjini Kahama, hivyo kusababisha uharibifu wa barabara za Mjini Kahama ambazo kwa kiasi kikubwa ni barabara za changarawe.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kahama ina mtandao wa kilometa 1,451 za barabara na bajeti yake ya mwaka ni Shilingi milioni 337. Ukizingatia gharama za matengenezo ya barabara ya barababara zilizvopanda, fedha hizo ni ndogo kukidhi matengenezo ya mtandao mzima wa barabara ikiwa ni pamoja na zile za mjini.

Mheshimiwa Spika, mgodi wa Buzwagi kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kahama, umeendelea kusaidia shughuli za jamii inayowazunguka na kwa hivi sasa mgodi unasaidia katika ujenzi wa madarasa katika Shule za Sekondari na Msingi. Halmashauri ya Wilaya ya Kahama ilituma maombi kwa mgodi wa Buzwagi ili waweze kuwasaidia katika matengenezo ya barabara za mjini kwa barua yenye Kumbukumbu Na. AB.276/347/02/30 ya tarehe 17 Desemba, 2008 ambayo haijajibiwa mpaka hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kahama imeahidi kukumbushia tena maombi yao na kwa vile pande zote mbili zina mahusiano mazuri, ni mategemeo yangu kwamba Mgodi wa Buzwagi utakubaliana na maombi hayo mara tu watakapomaliza shughuli za ujenzi wa madarasa. Hata hivyo, ni vyema Halmashauri ya Wilaya ya Kahama iweke vipaumbele vya matengenezo ya barabara zilizopo ili itumie fedha zinazotolewa kama ruzuku ya barabara kufanya ukarabati wa barabara hizo kadiri itakavyohitajika.

MHE. JAMES D. LEMBELI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo kwa kweli hayajaniridhisha mimi na wananchi wa Kahama, nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa katika hali ambayo si ya kawaida na ya kistaarabu, uongozi wa Mgodi wa Buzwagi sio tu kwamba hauna mahusiano mazuri na viongozi wa Halmashauri na wananchi

wanaouzunguka mgodi ule; na Kwa kuwa barua iliyotumwa mwezi Desemba, 2008 bado haijajibiwa mpaka hii leo; na Waziri anasema uongozi wa Halmashauri uendeleo kuwasiliana na mgodi; haiwezekani mwaka mmoja na nusu uongozi wa mgodi unashindwa kujibu barua ya kuomba msaada wakati ni mgodi huo huo wenye magari mengi katika Mji wa Kahama na ndiyo zinazoharibu barabara za miji wa Kahama lakini hawataki kujibu: Mimi naomba Serikali inieleze inawasaidia vipi wananchi wa Mji wa Kahama kuwabana hawa ndugu watengeneze hizo barabara?

NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI: Mheshimiwa Spika, ni bahati mbaya sana leo rafiki yangu Mheshimiwa Lembeli hajaridhishwa na majibu ambayo nimeyatoa hapa. Kwa sababu mimi Kahama nimekwenda mara mbili; nilikwenda alipokwenda Mheshimiwa Rais, halafu nilifanya na ziara katika lile eneo. Sasa ukitaka kuwa *scientific* unaangalia mambo *in a historical perspective*. Nataka nijibu vizuri kwa sababu hili linalosemwa hapa ni jambo kubwa.

Maelezo niliyoyapata hapa hawa mabwana wa Buzwagi kuna wakati walikuwa tayari kutengeneza barabara za Kahama kwa kiwango cha lami, lakini wakatofautiana na utaratibu utakaotumika kwa ajili ya kujenga zile barabara. Inavyosemekana Halmashauri iliwataka wapeleke moja kwa moja ili ishughulikie ujenzi wa hizo barabara. Buzwagi nilivyoieleza, walisema kwamba wao watakuwa tayari kutengeneza hiyo barabara kwa *ku-hand over keys*, wakatofautiana katika jambo hilo. Mimi kwa maoni yangu nikaona kwamba nia ya Buzwagi kusaidia pale katika kutengeneza barabara ilikuwepo na sasa hapa kinachozungumzwa kama ninaelewa vizuri ni kwamba Serikali kwa maana ya Serikali itumie msuli wake kuihakikisha kwamba Buzwagi inafanya kazi hiyo.

Kuna pande mbili pale ambazo ninazona. La kwanza, ni kweli kabisa Buzwagi inatakiwa ione kwamba barabara za Kahama zinakuwa nzuri ili ihusianishwe na uzuri wa barabara za pale. Lakini la pili, ni kweli kabisa kwamba suala la kuitaka Buzwagi ifanye hivyo ni suala la ridhaa ya Buzwagi yenyewe na ndiyo maana kuna *correspondance* hapo.

Nami ninapokuja hapa kujibu maswali nina *file* liko pale. Habari ya barabara inazungumzwa katika Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Kahama na habari hii imezungumzwa na Mkuu wa Wilaya pamoja na Kamati yake ya Ulinzi na Usalama. Wamezungumza mpaka sasa hivi wamesema kwamba wao wanasaidia kwanza sekondari na wanasaidia Shule za Msingi. Hii ina maana kwamba tukiendelea tunaweza tukawasaidia wenzetu wakapata barabara kule. Sasa mimi nataka nikae na Lembeli akitaka mimi niondoke hapa nitamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu niende mpaka Buzwagi pale, tuzungumze nao ili wahakikishe kwamba wanatengeneza hizo barabara. Lakini hizo ndiyo jitihada zilizotolewa hapa.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ukiangalia miradi mingi mikubwa inayofanywa nchini na wakandarasi mbalimbali wanaokuja, bahati mbaya wanakuja na vifaa ambavyo uwezo wake na uwezo wa barabara zetu huwa ni tofauti sana na kwa maana hiyo kampuni nyingi zinapoondoka zinatuachia matatizo makubwa sana ya miundombinu kwa sababu vifaa wanavyovitumia ni vikubwa. Je, Serikali haioni sasa imefika

wakati hasa kwa wawekezaji kukawa na sera inayosema unakuja kuwekeza hapa mazingira yetu ni moja, mbili, tatu, nne tano iingie ndani ya Mkataba badala ya kuvutana badala ya kuwalazimisha watekeleze yale tunayokubaliana ili iwe ni *package* moja ya kueleweka kabla ya *investor* hajafanya ili tuondokane na matatizo haya?

WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, kwanza napokea maoni ya Mheshimiwa Mbunge, lakini namba mbili kwa upande wa ujenzi wa miundombinu ya barabara wakati wote tumekuwa waangalifu kuhakikisha kwamba hawa wanaokuja kutufanyia kazi hizi wanakuwa na mitambo ile ambayo inakidhi haja ya ujenzi wa miundombinu hiyo.

Swali Na. 169

(Swali lililotajwa hapo juu liliondolewa na Muuliza Swali)

Na. 170

Vijana Wanaokimbiza Mwenge wa Uhuru

MHE. JOHN P. LWANJI aliuliza:

Kwa kuwa, mara baada ya mfumowa vyama vya Siasa kuanzishwa nchini, majukumu ya kukimbiza Mwenge wa Uhuru yaliwekwa chini ya Serikali kupitia Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana;

- (a) Je, ni utaratibu gani na vigezo gani vinavyotumika katika kuwateua vijana wanaokimbiza Mwenge?
- (b) Je, vijana hao wanapata posho kiasi gani kwa siku na kuna malipo yoyote wanayopewa baada ya kumalizika kwa kazi ya mbio za Mwenge?
- (c) Je, vijana hao hulipwa nini pindi wanapopatwa na ajali wakati wakikimbiza Mwenge?

WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Kwa mujibu wa mwongozo wa Mbio za Mwenge, utaratibu wa kuwapata Wakimbizi wa Mwenge kitaifa ni kama ifuatavyo:-
 - (i) Mwenge wa Uhuru kitaifa hukimbizwa na vijana sita. Kati ya vijana hawa mmoja huchaguliwa kuwa kiongozi. Kiongozi wa Mbio za Mwenge huchaguliwa kwa zamu kutoka Tanzania Bara mwaka mmoja na mwaka unaofuata Tanzania Visiwani. Aidha, uteuzi wa wakimbiza Mwenge

unazingatia kwamba jinsia zote zinashiriki. Mikoa inayoanzia au kumalizia Mbio za Mwenge hutoa mkimbiza Mwenge mmoja kila mwaka;

- (ii) Wakimbiza Mwenge huchaguliwa kutoka Majeshi, Taasisi za Serikali, Vyama vya Hiari ama Vikundi vya Vijana vya Uchumi;
- (iii) Maombi ya Wakimbiza Mwenge watatu (3) yanatoka Mikoa inayozindua na kuhitimisha Mbio za Mwenge yatapitishwa na Kamati ya Ulinzi kabla ya kuwasilishwa Wizarani kwa uteuzi; na
- (iv) Wakimbiza Mwenge kutoka Zanzibar huteuliwa huko huko Zanzibar na majina huletwa Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana.

Aidha, vigezo vinavyotumika kuwapata wakimbiza Mwenge ni pamoja na vijana wanaoomba kukimbiza Mwenge kuwa na sifa zifuatazo:-

- (i) Watanzania wenye umri kati ya miaka 18 – 35;
 - (ii) Wawe na Afya njema, tabia njema na akili timamu;
 - (iii) Wawe na Elimu ya Kidato cha Nne au zaidi na wenye ufahamu wa masuala mbalimbali ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii;
 - (iv) Wawe na wwezo wa kujieleza mbele ya wananchi;
 - (v) Wawe na uwezo wa kufaulu mafunzo yatakayotolewa ikiwa ni pamoja na uwezo wa kumudu mazoezi ya viungo na nadharia wakati wa maandalizi; na
 - (vi) Wawe na nia ya dhati ya kujitolea kukimbiza Mwenge na wakubaliane na masharti ya uendeshaji wa shughuli za Mbio za Mwenge.
- (b) Mheshimiwa Spika, kazi ya kukimbiza Mwenge wa Uhuru dhana yake hasa ni ya kujitolea. Hata hivyo, wakimbiza mwenge hulipwa posho ambayo kwa sasa ni Tshs kwa siku kwa ajili ya matumizi ya mahitaji madogo madogo yanayoweza kujitoleza katika safari hiyo. Wizara sasa hivi inapitia posho hizi ili ikiwezekana zirekebishwe kulingana na mahitaji na gharama za sasa.
- (c) Kutokana na umuhimu wa shughuli hii vijana wanapopatwa na ajali wanalipwa Bima. Hivyo, Wizara huhakikisha kwamba vijana wamepata kinga ya Bima ya ajali kabla ya kuanza Mbio za Mwenge.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja la nyongeza. Kumekuwa na malalamiko kwamba katika ujumbe ambao wakimbiza mwenge hutoa mara nyingine wamekiuka na kujiingiza katika masuala yasiyohusu ujumbe wanaopaswa kutoa katika mbio hizo: Je, Serikali inasemaje kuhusu

suala hili? Maana imefikia kiasi kwamba manung'uniko haya yamejikita zaidi kwenye masuala ya siasa badala ya kupeleka ujumbe unaotakiwa!

WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Spika, ujumbe ambao hutolewa na wakimbiza mwenge ni ujumbe ambao dhana yake imeandaliwa na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Kwa hiyo, kunakuwa na vipengele ambavyo vimeanishwa kwa mfano UKIMWI, rushwa na kadhalika. Sasa kutoka nje ya hapo sisi hatujapata malalamiko rasmi kama wapo waliohibitisha hivyo hata wakati mbio za mwenge zinaendelea, tafadhali tufahamishwe mapema ili tuweze kuchukua hatua muafaka ikiwezekana hata kumsimamisha anayefanya shughuli hizo nje ya utaratibu ambao mwenge unapaswa kuhudumiwa.

MHE. HAFIDH ALI TAHIR: Mheshimiwa Spika, nakushukuru na namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake. Katika maelezo aliyoyatoa alisema kwamba mwenge shughuli zake hasa ni kuhamasisha maendeleo, lakini vilevile kuzuia mambo ya UKIMWI na mambo mengine. Lakini mwenge ni wa Watanzania. Mheshimiwa Waziri anaweza kutuambia kwamba katika kumbukumbu zake za ukimbizaji mwenge, wenzetu upande wa CUF waliwahi kukimbiza mwenge hata mara moja? (*Kicheko*)

WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Spika, kama tulivyosema mwenge huu ni wa Serikali na hauna itikadi yoyote. Wanaokimbiza mwenge chujio lao ni Kamati ya Ulinzi na Usalama, basi. Wakishakuwa na uhakika huyu ni kijana mwenye tabia njema, sio mtu ambaye anaweza akaamua siku moja akatupa na mwenge wenyewe aone atakachofanywa; sisi tunasema tunaletewa tunamteua. Hili la kuendesha mambo bila kuzingatia itikadi yako katika maeneo mengi, kwa mfano unaweza ukawa hata *Referee* kama ndugu yangu Mheshimiwa Hafidh Ali, hupaswi kuonyesha itikadi yako kama wewe ni Simba au Yanga. Unapokuwa uwanjani kazi yako pale ni kutenda haki. Lakini wapo ma-*referee* tunawafahamu hawatendi haki.

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Waziri kwa mfano mzuri huo. Waheshimiwa tunaendelea, sasa ni zamu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, swali linaulizwa na Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar.

Na. 171

Mpango Madhubuti wa kudhibiti Ajali Nchini.

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR aliuliza:-

Kwa kuwa, katika siku za hivi karibuni kumejitokeza hali ya kuwepo kwa ajali nyingi za magari, treni, meli na ndege; na kwa kuwa ajali hizo zimesababisha watu wengi kupoteza baadhi ya viungo vya mwili:-

Je, Serikali ina mipango gani madhubuti ya kukabiliana na tatizo hilo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na *SUMATRA*, *TBS*, *TAMISEMI*, *TANROAD*, Baraza la Usalama Barabarani, *TRA*, Vyama vya wamiliki wa magari ya usafirishaji, Chama cha Madereva, Bima, Kikosi cha Zimamoto na uokoaji Wizara ya Afya na wananchi, limeendelea kufanya yafuatayo:-

- (i) Kusimamia Sheria na Kanuni za Usalama Barabarani ikiwa ni pamoja na kufanya doria, misako, kukagua magari na leseni za madereva na kuwafikisha Mahakamani wakosoaji;
- (ii) Kutoa Elimu ya usalama barabarani kwenye Shule mbalimbali za Msingi na Sekondari na madereva wa mabasi ya mikoani;
- (iii) Kukusanya na kutunza kumbukumbu za wakosaji waliohukumiwa ili kuwafuatilia wanaotenda makosa kwa kujirudia;
- (iv) Kukagua na kuyatambua maeneo korofi yasiyo na alama za barabarani ili kupanga askari kudhibiti mwendo kasi wa magari na kuweka alama za tahadhari;
- (v) Makao Makuu ya Kikosi cha Usalama Barabarani imeanzisha utaratibu kupitia Kazi moja *Vehicle Information Centre* ambapo kupitia Namba 0732 928723 na 0767750198 ya *moderm* hupokea taarifa za matukio ya kuvunja Sheria za Usalama Barabarani kutoka kwa wananchi na kuzipeleka kwa watendaji ili ziweze kufanyiwa kazi. Kwa kutumia namba hizo tumeweza kupata taarifa mbalimbali za makosa ya barabara na kuweza kuzuia ajali za barabarani na makosa mengine.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mikakati niliyoitaja hapo huu na ile ambayo nilieleza katika hotuba yangu wakati wa kikao cha Bunge la Bajeti ya mwaka 2009/2010, Wizara yangu kupitia Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wadau niliowataja hapo juu, limeanzisha Opereshi ya pamoja (*joint operation*) kwa ajili ya kudhibiti makosa ya usalama barabarani. Makosa ambayo yamekuwa sugu ambayo ni pamoja na ubovu wa magari, mwendokasi, kuzidisha mizigo/abiria, uendeshaji mbaya wa magari, madereva kuendesha wakiwa wamelewa na kutokuwa na leseni au kuwa na leseni za kugushi.

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuulizwa maswali ya nyongeza. Kwa kuwa kuna baadhi ya madereva huwaachia makondakta kuendesha gari na kwa kuwa makondakta hao wengi wao huwa hawana sifa ya udereva: Je, Serikali inasema nini kuhusiana na watu kama hao ambao wanasababisha ajali kila siku?

Swali la pili, kwa kuwa ajali nyingi zinazotokea ni zile za magari yanayokwenda Mikoani; na kwa kuwa pengine zinatokea kwa sababu na uchovu wa madereva pengine anakuwa dereva ni mmoja: Je, Serikali itakubaliana nami kwamba sasa ni wakati muafaka wa kupanga ama kuweka taratibu wa kuweka taratibu wa kuweka madereva wawili kwa magari ya kwenda Mikoani ili kusaidiana pale mmoja anapochoka?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwanza, kwa kweli ni kosa na hili tumekuwa tunalisemea sana. Madereva wawe ni madereva na wala sio makondakta kuweza kuendesha na nadhani hilo kwa kweli tumelidhibiti na sidhani kama ni kitu ambacho kinatokea mara kwa mara kwa sababu ushahidi tulionao ni kwamba huko tumekwisha toka na kwa kweli hilo tumeridhibiti, kwa sababu Sheria inasimamiwa na tumeshawaambia ma-traffic wawe wakali na wala wasiwe na huruma kwa sababu hizi ajali zinatimalizia raia wetu.

Kuhusu swali la pili, ni kwamba, SUMATRA imetoa mwongozo huo na hili ni suala ambalo limekuwa linasimamiwa na tumehakikisha kwamba magari yanakuwa na madereva wawili ili kuondoa ile hali ya uchovu.

Lakini kama tulivyosema, kwa kweli sababu ambazo zinasababisha hizi ajali kwa kweli ni nyingi na mojawapo ikiwa ni hii ambapo tumejaribu kuweza kuzidhibiti na zipo nyingine tunazifuatilia lakini kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, mkazo utawekwa kwa yale mabasi yanayokwenda Mikoani ili kuhakikisha kwamba kunakuwa na madereva wawili. (*Makofi*)

MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na kwa kuniona. Hapa nachukua nafasi hii makusudi kuja kumfunda mwali; na napenda nichukue nafasi hii kuwapongeza wateule wote walioteuliwa na Mheshimiwa Rais, tunawakaribisha katika Bunge hili na tunategemea mchango wao mkubwa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo, naomba niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa tuna Wiki ya Usalama Barabarani, tuna Askari wa Usalama Barabarani; ni lini tutapata Wiki ya Usalama Majini na Askari wa Usalama Majini, hasa ukizingatia ajali nyingi zinazotokea katika Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa na katika Bahari ya Hindi? (*Makofi*)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba wiki moja ya kuangalia suala la usalama barabarani haitoshi. Kimsingi, kitu ambacho tumeamua ni kwamba zoezi la kuhakikisha kuna usalama barabarani ni suala endelevu na siyo tu la wiki moja. Tuko katika mkakati tukishirikiana na wenzetu wa Wizara ya Miundombinu na SUMATRA kubadilisha mfumo wa kuangalia masuala ya usalama barabarani na siyo kwa wiki ya kwenda kwa usalama barabarani. Ningependa pia kusema kwamba, katika suala la usalama katika maeneo yetu ya maji, maziwa na bahari, pia tunatambua kwamba wiki moja peke yake haitatosha. Katika Ziwa Victoria ambalo ameliongelea, Serikali imedhamiria kuongeza vitendea kazi ili kuhakikisha kwamba katika Maziwa yote hapa nchini kunakuwa na usalama.

Mheshimiwa Spika, ningependa kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba wiki ijayo tarehe 17, Wizara yangu itasaini mkataba na Serikali ya Marekani ili kutusaidia boti za doria katika Maziwa yetu hapa nchini. Boti tano za kwanza tunatarajia zitafika hapa nchini kuanzia mwezi Julai, 2010 na Boti nyingine zitafika kwa awamu katika kipindi cha mwaka mmoja na nusu.

Mheshimiwa Spika, tungependa kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inafanya kila jitihada kwamba katika Ziwa Victoria na Maziwa mengine hapa nchini, kuhakikisha kwamba usalama unakuwepo.

SPIKA: Ahsante kwa majibu mazuri.

MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa sababu ajali nyingi zinawaumiza wananchi wetu: Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuwalazimisha wamiliki wa vyombo hivi kuweka bima ya abiria?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwa kweli suala la jali nchini hapa hususan katika barabara, limekuwa ni suala ambalo ni zito sana na kuna mijadala mingi sana kwa wadau wote anaohusika. Suala la bima limekuwa miongoni mwa masuala ambayo bado yanazungumzika. Hivi sasa kwa kweli siwezi nikamwambia Mheshimiwa Mbunge litakwenda vipi kwa sababu ni suala ambalo linawahusu wenyewe wakata bima, *of course* kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, ni suala linalohusu vyombo mbalimbali, Serikali na kadhalika. Niseme tu kwamba ni suala ambalo bado linazungumzika na isingekuwa busara sasa hivi niweze kutoa kauli ya kusema kwamba iwe hivi ama iwe vile.

Lakini, Serikali inazingatia na kweli imekuwa msitari wa mbele, Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amekuwa akilisemea hili la ajali barabarani, Waziri Mkuu amekuwa akilisemea mara kwa mara na kwa kweli tumekuwa tunajipanga. Miongoni mwa mambo ambayo tunajaribu kuyatazama ni kuona ni vipi wale waathirika wanaweza wakasaidiwa. Ni hilo suala la bima. Lakini nini yatakuwa matokeo; kwa kweli ningemwomba Mheshimiwa Bakary nisiende huko kwa sasa hivi.

Na. 172

Uwekaji wa Umeme katika Jengo la Polisi – Bububu

MHE. MASOLWA C. MASOLWA aliuliza:-

Je, Serikali itakamilisha lini uwekaji umeme katika jengo wanaloishi Askari Polisi Kituo cha Bububu ambalo halina umeme kwa miaka mingi?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mbunge wa Bububu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua kuwa katika Kituo cha Polisi Bububu kuna nyumba ya makazi ya Askari yenye nafasi ya kuishi familia mbili ambayo haina umeme kwa muda mrefu sasa. Ili kuunganisha umeme katika jengo hilo zinahitajika jumla ya shilingi 2,500,000/=.

Mheshimiwa Spika, ni nia ya Serikali kuhakikisha kwamba Askari wake wanaishi katika mazingira mazuri ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na *morally* ya juu. Hata hivyo, nia hiyo inakwamishwa na ufinyu wa bajeti inayotengwa kwa ajili ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, tumeagiza fedha hizo zipatikane ili suala hili ambalo limechukua muda mrefu lipate kutatuliwa.

MHE. MASOLWA C. MASOLWA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Waziri amekiri kwamba suala hili lina miaka mingi; na kwa taarifa ni zaidi ya miaka 15 kwa maana ya bajeti 15; sasa, pamoja na kwamba ameagiza zipatikane pesa; ni lini sasa (*time frame*) pesa hizo zitapatikana ili umeme uingizwe pale?

Swali la pili, kwa kuwa Wizara imekuwa na mtindo wa kuanzisha miradi mipya kabla ya kuikamilisha ile ya zamani; sasa haioni hivi sasa ni vyema kukamilisha miradi ya zamani kwanza ndipo ianzishe miradi mipya?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, hakika anaponiuliza ni lini, nadhani Mheshimiwa Masolwa anatambua kwamba siku za nyuma hapo tulikuwa tunamwambia kwamba tutajitahidi, kwa sababu ya ufinyu wa bajeti haitawezekana. Sasa hivi ninasema kwamba nimetoa agizo na hilo agizo amelitoa Mheshimiwa Waziri kwamba hili jambo lifanyike na kwa imani yangu, katika kipindi hiki cha bajeti, kabla bajeti hii tuliyonayo haijakwisha, hili suala tutakuwa tumefikia ufumbuzi wake. Kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge na mimi nilivyosema ni kwamba limechukua muda mrefu sana.

Sasa, kuhusu suala la pili, kusema kwamba Wizara imekuwa na mtindo na hasa nawekelele ile *shade* katika mtindo, mimi nasema kwamba kwa kweli hapo Mheshimiwa Mbunge anatuonea, maana Wizara haina mtindo wa kusema kwamba inaanzisha mambo mapya na inaacha yale ambayo imeanza bila kuyakamilisha.

Hili suala lake ni kweli lilikuwa moja miongoni mwa yale mambo ambayo yamekuwepo; na nia na dhamira ya Serikali na Wizara yangu imekuwa ni kukamilisha yale yote ambayo tumeyaanzisha, na kama tumefika mahali tumekwama, siyo kwa sababu ya utashi wa Wizara kutotaka kufanya hayo ama kuyakamilisha hayo, lakini imekuwa ni kwa sababu ya uhaba wa fedha na pale ambapo fedha zinapatikana, miradi ambayo inakuwa inasimama, tunakuwa tunaikamilisha.

Na. 173

Kuandaa Mazingira Bora kwa Wafugaji

MHE. SHOKA KHAMIS JUMA aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania ni nchi iliyojaaliwa mifugo mingi kama vile ng'ombe, mbuzi, kondoo, na kadhalika; na kwa kuwa Serikali imeshindwa kabisa kuandaa mazingira bora yatakayowahakikishia wafugaji ubora wa mifugo yao na ndio maana huwa wanahamama kila wakati: Je, Serikali inasema nini juu ya hoja hii?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mbunge wa Micheweni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka mazingira bora kwa ajili ya wafugaji ili waweze kufuga mifugo yao kibiashara na kitaalam kwa kuandaa sheria, kanuni na miongozo mbalimbali inayosimamia shughuli za sekta ya mifugo. Sheria hizi ni pamoja na Sheria ya Nyama Na.10 ya mwaka 2006, Sheria ya Maziwa Na.8 ya mwaka 2004, Sheria ya Ustawi wa Wanyama Na.19 ya mwaka 2008, Sheria ya Magonjwa ya Mifugo Na.17 ya mwaka 2003, Sheria ya Veterinari Na.16 ya mwaka 2003 na Sheria ya Ngozi Na.18 ya mwaka 2008.

Aidha, hadi sasa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Halmashauri mbalimbali zimetenga maeneo yenye jumla ya hekta 1,391,109.4 kwa ajili ya wafugaji katika Mikoa 13, Wilaya 31 na Vijiji 240. Zoezi la utengaji wa maeneo bado linaendelea kadiri ya upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kuimarisha mashamba ya kuzalisha mbegu za malisho ya mifugo ili kuboresha upatikanaji wa malisho katika mashamba ya Langwira (Mbeya), Vikuge (Pwani), Mabuki (Mwanza), *Sao Hill* (Iringa), Kizota (Dodoma) na Kongwa (Dodoma).

Aidha, Wizara inashirikiana na wadau wengine kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*DADPS*) kuimarisha na kujenga miundombinu ya mifugo ambapo kuanzia mwaka 2001/2002 hadi sasa jumla ya malambo 852 yamejengwa, 32 yamekarabatiwa pamoja na visima virefu 13 katika Wilaya 65. Majosho mapya 182 yamejengwa na 605 yamekarabatiwa. Pia katika mwaka 2008/2009, Serikali ilitumia shilingi bilioni 11.4 kwa ajili ya ruzuku ya dawa ya kuogesa mifugo. Serikali pia imetoa chanjo kwa ajili ya kudhibiti ugonjwa wa homa ya mapafu ambapo katika mwaka 2008/2009 jumla ya dozi milioni 3.2 za chanjo ya *CBPP* zilinunuliwa na ng'ombe milioni 2.5 walichanjwa.

Mheshimiwa Spika, katika suala la uhamilishaji, Kituo cha Kuzalisha Mbegu Bora za Mifugo cha Taifa (*NAIC*) kimeendelea kuimarishwa kwa kununua madume 10 kutoka Afrika Kusini na kufikisha madume 34 kituoni hapo. Lengo ni kuzalisha dozi 100,000 kwa mwaka badala ya dozi 65,000 zilizozalishwa mwaka 2008/2009. Katika jitihada za kurahisisha upatikanaji wa mbegu bora katika maeneo mengi hapa nchini, Wizara imeanzisha Vituo vya Uhamilishaji vya Kanda vikiwemo vya Nyanda za Juu Kusini (Mbeya), Kanda ya Ziwa (Mwanza), Kanda ya Mashariki (Kibaha) na Kanda ya Kati (Dodoma).

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutoa elimu ya ufugaji wa mifugo bora ambapo mwaka 2008/2009 wafugaji 21,106 walipewa mafunzo. Aidha, watalaam wa ugani 1,185 wapo katika Vyuho mbalimbali vya Mifugo na wanagharamiwa masomo na Wizara. Vipindi vya Redio 52 na vya Televisheni 12 kuhusu ufugaji bora vimetayarishwa na kurushwa hewani.

Mheshimiwa Spika, ili kuwapatia wafugaji soko la uhakika la ndani na nje ya nchi, Wizara inaendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda vidogo, vya kati na vikubwa vya kusindika nyama na maziwa. Hadi sasa kuna machinjio za kisasa manne yaliyopo Dodoma, Arusha, Sumbawanga na Morogoro. Aidha, vipo viwanda vya maziwa vikubwa vitano vya *Tanga Fresh*, *New Musoma Dairy*, *Mara Milk*, *ASAS Dairy* (Iringa) na *International Dairy Product* (Arusha) na vya ngozi sita.

Mheshimiwa Spika, kutokana na juhudi hizi za Serikali nilizozitaja, sio kweli kwamba Serikali imeshindwa kuandaa mazingira bora kwa wafugaji badala yake Serikali imeandaa na itaendelea kuboresha Mazingira.

SPIKA: Loh! Kwa kweli jibu refu! Natumaini Mheshimiwa Shoka, swali lako litakuwa fupi. Swali la nyongeza!

MHE. SHOKA KHAMIS JUMA: Mheshimiwa Spika, kama kawaida yangu, maswali yangu yanakuwa mafupi. Pamoja na majibu marefu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda nimwulize kama ifuatavyo:-

Swali la kwanza, Wizara ya Mifugo pamoja na Wizara ya Ardhi tayari wameshaanza kutenga maeneo kwa ajili ya wafugaji; na kwa kuwa kabla ya maeneo hayo hayajaanza kufanyiwa kazi, Serikali imeishaanza kuwahamisha wafugaji: Je, Serikali itakuwa tayari kuwalipa fidia wafugaji hawa watakaopata hasara kutokana na zoezi hili?

Swali la pili, pamoja na sheria na miongozo ambayo ameitaja Mheshimiwa Naibu Waziri: Je, Serikali ina mpango gani mahsusi wa kuinua ubora wa mifugo hapa Tanzania?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali ili kutatua matatizo ya wafugaji imeona ni vizuri kupima na kutenga maeneo ya ufugaji na hivi karibuni tunatarajia Muswada unaohusu malisho na vyakula vya mifugo utaletwa hapa Bungeni ili sehemu za ufugaji ziwepo kabisa zimewekwa ili mtu mwingine akiziingilia, basi ataambiwa kwamba hizo ni sehemu za wafugaji.

Kuhusu wafugaji waliohamishwa ni kwamba kuna watu walikuwa kule Kilosa wakahamishiwa sehemu nyingine. Sasa kuhusu tatizo hilo, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshaunda Tume, tunatarajia hiyo taarifa ya hiyo Tume itakapotoka na Serikali kupitia ripoti hiyo, ndipo tunaweza kuja na aidha walipwe ama wasilipwe fidia. Kwa hiyo, tungoje majibu ya Tume iliyoundwa.

Kuhusiana na suala la miongozo gani ya kuboresha mifugo, nafikiri nimeshataja. Kwa mfano, kwa sasa hivi kuna uhamilishaji. Tumeimarisha kile Kituo cha Uhamilishaji cha Nike kilichopo kule Arusha ambacho kwa kweli sasa hivi tunatoa mbegu bora. Kwa hiyo, natoa wito

kwa wananchi na Halmashauri kwa ujumla kutumia mbegu bora ili kuweza kuhamilisha ng'ombe wao. Vile vile tuna mashamba ya mbegu za malisho bora. Tunaomba wananchi wazitumie. Vile vile tunaendelea kuweka miundombinu kupitia DADPS na katika kufanya hivyo tunajua kwamba mifugo itaboreshwa.

Na. 174

**Mchango wa Tanzania katika Mradi wa Kuongeza
Mipaka ya Nchi**

MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA (K.N.Y. MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA)
aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ya Norway inaisadia Serikali ya Tanzania kutayarisha miradi kwa kuomba Umoja wa Mataifa kuiongezea Tanzania mipaka upande wa Bahari kwa kiasi cha Nautical Miles 200; na kwa kuwa Norway imetoa Dola milioni 4.6 na Tanzania kutakiwa kuchangia Dola milioni 2.6; na kuwa ongezeko hilo la mpaka litaifaidisha nchi yetu katika sekta za mafuta, gesi, uvuvi na kadhalika:-

- (a) Je, ni lini Serikali itatoa mchango wake wa Dola milioni 2.6?
- (b) Je, Serikali inafahamu kuwa mwisho wa kupeleka mradi huo ni mwezi Mei, 2009?

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, chini ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa Unaosimamia Masuala ya Baharini (*The United Nations Convention on the Law of the Sea*), nchi zilizoridhia Mkataba huu zimepewa fursa ya kuongeza umbali wa awali wa kiuchumi baharini zaidi ya umbali wa awali wa maili za majini 200.

Nchi inayokusudia kuongeza ukanda wake inatakiwa kufanya utafiti mahsusi katika eneo hilo na hatimaye kutoa ushahidi wa kisayansi wa kuthibitisha kuwa tabaka la udongo na miamba katika eneo hilo ni mwendelezo wa tabaka la miamba iliyopo katika ufukwe wake au ina uwiano na miamba hiyo. Kazi hiyo ni kubwa na yenye kuhitaji teknolojia na taaluma ya hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ilianza kutekeleza mradi huu katika mwaka wa fedha 2008/2009 kwa kushirikiana na Serikali ya Norway. Serikali ya Norway imetoa msaada wa Dola za Marekani milioni 4.6.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2008/2009, Serikali ya Tanzania ilitenga Dola za Marekani milioni moja kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Kiasi hicho kilifikwa kufuatia uchambuzi wa mahitaji halisi kwa kipindi hicho. Kwa kuwa mradi huu bado unaendelea, Serikali itaendelea kutenga fedha kulingana na mahitaji kwa ajili ya utekelezaji wake.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu kuwa tarehe ya kuwasilisha hoja ya kuongeza Ukanda wa Kiuchumi Baharini huko Umoja wa Mataifa ilikuwa ni tarehe 13 Mei, 2009. Tanzania ilifanikiwa kuwasilisha hoja yake ya awali (*preliminary report*) tarehe 7 Mei, 2009 kabla ya tarehe ya mwisho iliyowekwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya Umoja wa Mataifa kupokea hoja ya awali, imeiongezea Tanzania miaka miwili ya kukamilisha na kuwasilisha hoja kamili (*final report*) ifikapo mwezi Mei, 2011. Serikali iko katika hatua za mwisho za kukamilisha kukamilisha hoja hiyo na mara itakapokamilika Tanzania itaiwasilisha Umoja wa Mataifa.

MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA: Mheshimiwa Spika, kwa kweli sina swali lolote, isipokuwa kuipongeza tu Serikali kwa hatua ambayo imefikia na kwamba hoja zenyewe tayari zimeshafikia kikomo. Nawashukuru sana. Ahsante sana.

SPIKA: Asante sana. Mheshimiwa Waziri pokea hizo shukrani na pongezi. Tunaendelea.

Na. 175

Gharama za Kuhamisha Wananchi Wanaozunguka Eneo la Mabibo

MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR aliuliza:-

Kwa kuwa eneo la uwekezaji la Benjamin Mkapa lililopo Mabibo limezungukwa na nyumba za wananchi na kwamba kwa usalama wa eneo hilo ni muhimu nyumba hizo zikabomolewa:-

- (a) Je, wananchi wa maeneo hayo watalipwa lini?
- (b) Je, tathmini ya gharama imeishafanyika?
- (c) Je, bajeti ya eneo hilo imepangwa kwa mwaka huu?

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mbunge wa Mkwajuni, naomba nitoe maelezo ya jumla kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba eneo la uwekezaji la Benjamin William Mkapu lililoko Mabibo limezungukwa na nyumba za wananchi. Katika tathmini ya fidia ya awali iliyofanyika mwaka 2007, ilikubalika kuwa nyumba zilizomo ndani ya umbali wa mita 30 kutoka ukuta wa mradi, zibomolewe kwa usalama wa eneo. Tathmini hiyo ilionyesha kuwa gharama ya fidia ni shilingi bilioni 10.

Baada ya majadiliano na wananchi wa eneo hilo, ilionekana kwamba umbali wa mita 30 kutoka ukuta wa mradi ni mkubwa mno na hauhitajiki. Umbali huu ungewaathiri wananchi wengi na kuhitaji gharama kubwa ya fidia pasipo umuhimu. Hata hivyo, Mamlaka ya EPZ kwa kushirikiana na watalaam kutoka Chuo Kikuu cha Ardhi wameshakamilisha tathmini mpya ambayo inahusisha nyumba zilizomo ndani ya umbali wa mita 7 – 10 hususan zile ambazo zitapata athari au zinaleta athari za moja kwa moja kwenye mradi. Nyumba zitakazoathiriwa na zoezi hili zitafidiwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mbunge wa Mkwajuni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kufuatana na kukamilika kwa tathmini mpya, wananchi wote ambao wamo ndani ya mita 7 - 10 watalipwa fidia stahili. Gharama ya tathmini mpya ambayo imepunguza umbali wa eneo la fidia kutoka mita 30 hadi mita 7 – 10 kutoka kwenye ukuta ni kiasi cha shilingi bilioni 1.2. Kutokana na hali halisi ya mapato ya Serikali, katika mwaka huu wa fedha 2009/2010 kiasi cha shilingi milioni 500 kimetengwa kwa ajili ya fidia kwa wananchi wa maeneo hayo. Aidha, tutaendelea kutenga katika bajeti zifuatazo kiasi cha fedha kilichobaki.

MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa Serikali hivi sasa ina utamaduni wa kuchelewesha malipo ambayo yamefanyiwa tathmini; na vile vile huwapunja wananchi katika nyumba zao: Je, Wizara imejipangaje kwa hili ili kuepuka yale matatizo yaliyotokea Mbagala na Kipawa?

Swali la pili: Je, hizo Shilingi milioni 700 zilizobakia Wizara inatarajia kuzilipa lini kabla haijawahamisha wananchi?

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Spika, kwanza, namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake. Kuhusu swali la kwanza kwamba Wizara imejipangaje, nataka kumhakikishia kwamba kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi, mwaka huu wa fedha tumetenga Shilingi milioni 500 na katika bajeti zijazo na ikiwezekana bajeti inayokuja tutapanga Shilingi milioni 700 zilizobaki ili kuhakikisha kwamba wananchi hao wanalipwa na eneo lenyewe linabakia salama.

Kuhusu Shilingi milioni 700 kwa swali la pili, ningependa kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inalipa madeni yote kutokana na bajeti ambayo Bunge letu Tukufu

limepitisha na kwa hiyo, malipo ya madeni yote yanatokana na uwezo wa Serikali wa bajeti yake. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu na wananchi wa Tanzania kwamba wananchi hawa ndio wadau wakubwa wa Serikali, kwa hiyo, Serikali haicheleweshi malipo yao bila sababu. Ningependa kuwaeleza kwamba kila tutakapopata uwezo, tutawalipa wananchi wanaoidai Serikali. Asanteni sana.

Na. 176

Upotoshaji wa Dhana ya Soko Huria

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO aliuliza:-

Kwa kuwa, kumetokea wimbi la upotoshaji wa dhana ya soko huria hapa nchini hasa katika maeneo ya wakulima wadogo ambapo mikataba yao ya biashara ya chai huingiliwa na kuvurugwa na wakulima wakubwa wa chai:-

Je, Serikali ina maelezo gani kuhusu jambo hilo hasa katika Wilaya ya Lushoto?

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Chai Tanzania ilipewa jukumu la kusimamia na kudhibiti biashara ya chai kwa kutumia Sheria ya Chai ya mwaka 1997 na Kanuni zake za mwaka 1999. Kutokana na sheria hiyo, Wakala wa Wakulima Wadogo wamepewa jukumu la kuendeleza zao la chai kwa wakulima wadogo nchini. Katika kusimamia sheria hiyo, pamoja na mambo mengine, Bodi ya Chai Tanzania imekuwa inatoa leseni za kununua chai kwa wenye viwanda na hii hufanyika baada ya kufanya utafiti wa kina ambao umeshirikisha kikamilifu uongozi wa maeneo husika kama ilivyoainishwa kwenye Kanuni za Sheria ya Chai za Mwaka 1999.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Lushoto viwanda vilivyopewa leseni kununua majani ya chai vilikuwa viwili ambavyo ni Kiwanda cha Mponde ambacho kinamilikiwa na wakulima wadogo na Herkuru ambacho kinamilikiwa na wakulima wakubwa. Kiwanda hiki kinanunua chai kutoka kwa wakulima wadogo walioko karibu na kiwanda hicho.

Mheshimiwa Spika, mikataba ya aina hii ni ya kawaida, kwa mfano, Wilaya ya Rungwe, kuna Kampuni ya Wakulima Wakubwa ya *Tea Company (WATCO)* ambayo imeingia mkataba na wakulima wadogo kupitia umoja wao wa wakulima uitwao Rungwe *Smallholders Tea Growers Association (RSTGA)*. Vile vile kampuni ya wakulima wakubwa ya Mufindi *Tea and Coffee Company* wamengia mkataba na wakulima wadogo kupitia umoja wao wa *Mkonge Tea Block Farm* na Chama cha Wakulima Wadogo wa Chai Mufindi. Aidha, kampuni ya *Mohamed Enterprise* imeingia mkataba wa kununua chai kupitia Ushirika wa Wakulima Wadogo Korogwe. Katika mikataba yote hii, ununuzi hufanywa kulingana na makubaliano yaliyomo ndani ya mikataba waliyoandikishana. Wakati wa mauzo, Serikali hufuatilia kwa karibu

kuhakikisha kuwa Sheria, Kanuni na taratibu zilizoko za soko huru hazivunjwi wala kukiukwa. Napenda kurudia kwamba siyo soko huria, ni soko huru.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo hayo, ni dhahiri kwamba upo utaratibu madhubuti unaotumika katika kufanikisha biashara ya chai katika Wilaya ya Lushoto. Hata hivyo, napenda kumwomba Mheshimiwa William Shellukindo atupe taarifa kama kuna dalili zozote za upotoshaji wa soko huru ili Serikali ichukue hatua haraka.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza maswali mawili madogo. Pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Waziri: Je, atakubaliana na mimi kwamba kwa sababu wakulima wadogo wa chai wa Usambara – *UTEGA* ndio wamiliki wa kiwanda cha Mponde na kwamba kiwanda kile kimepanuliwa, kina uwezo wa kuchakata chai ya wakulima wote? Je, kutoa leseni kwa mkubwa huyo Bambay Burmah kunua chai ya hao wenye kiwanda ni kudhoofisha umoja wetu?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri alitaka kujua kama kuna wanaopotosha ukweli wa soko huru kwasababu wakulima wadogo hao wana mikataba na wamedhaminiwa mikopo ya benki, kwa hiyo, kuja kununua chai yao ni sawa na kutaka kuvuruga umoja huo kwa kushindwa wakulima hao kulipa mikopo yao?

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa William Shellukindo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ninamshukuru sana na ninampongeza sana kwa kufuatilia maslahi ya wakulima wadogo. Kwanza kabisa, kutoa leseni kwa wakulima wakubwa sio kudhoofisha wakulima wadogo pale ambapo nimesema kuna utaratibu na ningependa kusema kwamba katika uchumi wa soko na soko ambalo ni huru, udhibiti lazima uwepo na usimamizi lazima uwepo ili wakubwa na wadogo wote wapate maslahi yao kama inavyotegemewa na kwa hiyo, nitafuatilia kama kuna kudhoofisha wakulima wadogo ili hatua stahili ziweze kuchukuliwa katika kudhibiti wote wawili, wakulima wadogo na wakulima wakubwa waweze kuendelea kwa maslahi ya uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Herkuru wanavyopotosha soko huru hilo nitalifuatilia, na kwasababu yeye ameeleza hapa, Wizara yangu itafuatilia na kuona kwamba udhibiti unafanya kazi yake na yule ambaye anavuruga biashara katika uhuru kwa vyovyote vile kwa mujibu wa Sheria ya udhibiti tutajua la kumfanyia.

SPIKA: Tunaendelea. Waheshimiwa Wabunge, sasa ni Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika swali linaulizwa sasa na Mheshimiwa Charles Keenja wa Ubungo.

Na. 177

Kauli mbiu ya Bajeti ya 2009/ 2010 – “Kilimo Kwanza”

MHE. CHALRES N. KEENJA aliuliza:-

Kwa kuwa Kauli ya bajeti 2009/2010 ni “Kilimo Kwanza”

- (a) Je, kauli mbiu hiyo ni sahihi kwa kiwango gani?
- (b) Je kauli mbiu hiyo itatekelezwe katika jiji la Dar es Salaam na miji mingine?
- (c) Je, ni mikakati gani iliyoandaliwa kutekeleza mpango huo?

WAZIRI WA CHAKULA, KILIMO NA USHIRIKA alijibu:-

(a) Kauli mbiu hiyo ni sahihi kwasababu ina azma ya Kilimo Kwanza ni kuleta mapinduzi ya kijani kwa lengo la kukifanya kilimo cha Tanzania kuwa cha kisasa na cha kibiashara. Kilimo Kwanza inatambua kuwa changamoto kubwa kwa Watanzania ni kupambana na umaskini na kujitosheleza kwa chakula. Hivyo Kilimo Kwanza ni muhimili muhimu katika kuongeza kasi na utekelezaji wa programu ya kuendeleza sekta tya kilimo (*ASDP*) na kufanikisha malengo ya mkukuta, milenia ya utekelezaji wa dira ya Taifa ya maendeleo 2005.

Aidha, kupitia adhima ya Kilimo Kwanza, watekelezaji wa *ASDP* wameongezeka kwa kuwa zimehusisha Wizara zote, sekta binafsi na washirika wa maendeleo. Kilimo Kwanza pia imewezesha kuwa na utaratibu wa Kitaifa wa mipango rasilimali, usimamizi na uwajibikaji ili kuongeza kasi ya kuleta mapinduzi ya kilimo nchini. Kadhalika utashi wa kisiasa (*Political will*) uliopo unaipatia nguvu zaidi ya utekelezaji.

(b) Kwa kuwa utekelezaji wa kaulimbiu unahusisha wadau wote wakiwamo sekta binafsi, kaulimbiu hiyo itatekelezwa katika Jiji la Dar es Salaam ukiwemo usindikaji wa mazao ya mimea na mifugo, uimarishwaji wa mauzo na masoko ya uhakika kwa mazao ya mimea na mifugo na uimarishwaji wa upatikanaji na usambazaji wa pembejeo na zana za kilimo katika miji midogo ambao wakazi wake ni wakulima. Tunafanya mashauriano na Wizara ya ardhi ili kuhakikisha kwamba upimaji wowote wa ardhi katika miji hiyo uzingatie mahitaji ya ardhi ya kilimo ili kuhakikisha maendeleo ya kilimo katika miji midogo ile ambayo haikui na kuwa miji ya watu walio na ajira.

(c) Mkakati wa Kilimo Kwanza ulizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa Sherehe za Nane Nane ambapo mfumo wa utekelezaji wa zile nguzo kumi za Kilimo Kwanza uliotolewa ambao unaainisha shughuli, majukumu, muda wa kutekeleza, mhusika mkuu na wahusika wengine. Katika mwaka wa fedha wa 2009/ 2010 Wizara zote zimeandaa mpango kazi wa kutekeleza Kilimo Kwanza na kila mdau atahitajika kuandaa atakavyotekeleza Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Spika, napenda kisisitiza kuwa utekelezaji wa Kilimo Kwanza ni jukumu la Watanzania wote zikiwemo Wizara za sekta za kilimo kwa kushirikiana na Wizara zote na wadau wengine kama vile sekta binafsi mabenki na washirika wa maendeleo. Hivyo, ni matumaini yetu kwa kupitia Braza la Taifa la Biashara sekta binafsi itaongeza uwekezaji katika sekta ya kilimo sambamba na Serikali.

MHE. CHARLES N. KEENJA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo sana ya nyongeza na ninamshukuru Waziri kwa majibu yake.

Tangu hii kauli ya Kilimo Kwanza ianze wadau wengi wa kilimo wamechanganyikiwa juu ya tofauti iliyopo kati ya Kilimo Kwanza na *ASDP*, ningeomba Waziri afafanue hili ili atuondolee mkanganyiko huu.

Mheshimiwa Spika, swali dogo la pili miaka iliyopita tumekuwa na kauli mbiu kama hizi, kuna maazimio mfano Azimio la Maputo ambalo lilitaka tutenge asilimia 10 ya bajeti zetu kwa ajili ya kilimo. Kwa sababu mbalimbali hatukuweza kuyatekeleza; Serikali inafanya nini sasa kuhakikisha kwamba kauli mbiu hii itatekelezwa? Ni mpango gani utawekwa katika bajeti ya mwaka ujao?

WAZIRI WA CHAKULA, KILIMO NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, ni dhana ambayo inazungumzia kukipa kilimo nafasi muhimu zaidi katika Uchumi wa Tanzania kwa sababu ambazo zinaeleweka, kwamba kilimo ndio kinaajiri asilimia kubwa ya Watanzania wote na kinategemewa, kinatakiwa kiboreshwe ili kukuza uchumi wa nchi. *ASDP* ni programu ambayo inatekeleza dhana hii ya Kilimo Kwanza ambayo ina mipango mahsusi na inasimamiwa na inatekelezwa katika ngazi zote. Lakini Kilimo kimepanuka, kimeingiza sekta binafsi, kinataka kuhusisha sekta ya viwanda kuhakikisha ya kwamba siyo tunalima tu, lakini vilevile tunaongeza thamani ya mazao.

Mheshimiwa Spika, kwa vile kuna sekta ya Miundombinu ambayo inatakiwa iende sambamba na utekelezaji wa programu hizi za Kilimo Kwanza ili kuhakikisha kwamba mazao yanayolimwa yanafikia soko. Pia kuna masuala mengi ambayo yamejumuishwa katika zile nguzo kumi za Kilimo Kwanza na kwamba *ASDP* ni programu na Kilimo Kwanza ni dhana pana zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la pili la Azimio la Maputo siyo kwamba limeshindikana kutekelezwa. Wakati Maputo inapitisha Azimio hili uwekezaji katika Sekta ya Kilimo ulikuwa chini ya asilimia tano. Mwaka jana sekta ya kilimo ilitengewa bajeti kufikia asilimia 7.2 na shabaha ni kuendelea kufikia utekelezaji halisi wa Kilimo Kwanza. Matumaini yetu ni katika bajeti ijayo kutakuwa na ongezeko zaidi katika bajeti ya sekta ya kilimo. Kwa hiyo, tunaendelea kutekeleza Azimio la Maputo.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda umetutupa mkono na hiki ndiyo kikao cha mwisho cha Bunge la Mkutano wa Kumi na Nane. Kwa hiyo, tunaendelea. Swali linalofuata la Wizara hiyo hiyo linaulizwa na Mheshimiwa Godfrey Zambi wa Mbozi Mashariki.

Na.178

**Mbolea ya Ruzuku Kutowafikia Wakulima
wa Wilaya ya Mbozi**

MHE. GODFREY W. ZAMBI aliuliza:-

Kwa kuwa katika taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2008 ilibainishwa kwamba mbolea yenye ruzuku

yenye thamani ya Sh. 30,402,100/= haikuwafikia wakulima wa Wilaya ya Mbozi na kwa kuwa tarehe 27 Julai, 2009 Serikali iliombwa kutoa maelezo juu ya hatua kwa wakala waliohusika na upotevu wa mbolea akasema kuwa mchakacho wa suala hilo unaendelea na kwamba majibu ya hoja yangepelekwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali:-

(a) Je, mchakato huo umefikia wapi?

(b) Mawakala waliohusika na upotevu huo wa mbolea wamechukuliwa hatua gani za Kisheria?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali iliahidi kutoa majibu ya hoja iliyodai mbolea ya ruzuku yenye thamani ya Sh. 30,402,100/= haikuwafikia wakulima wa Mbozi na kwamba majibu hayo yangepelekwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Baada ya kufuatilia suala hilo, ilibainika kwamba mbolea iliawafikia wakulima na kusambazwa katika vituo husika, tatizo lilijitokeza ni kuwa, wakati ukaguzi unafanyika, mawakala waliopewa kazi ya kusambaza mbolea ya ruzuku walikuwa wamemaliza kazi na kurudi nyumbani, hivyo hawakuwepo kwenye vituo vya mauzo. Daftari linaloonyesha wakulima walinunua mbolea ya ruzuku na kusaini tayari limekwishawakilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

(b) Mheshimiwa Spika, hakuna wakala yeyote aliyechukuliwa hatua za Kisheria kwa kuwa hakuna upotevu wa mbolea uliobainika.

MHE.GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya kuridhisha kwa kiasi fulani ya Mheshimiwa Waziri, naomba nimwulize kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, ukienda vijijini kule Mbozi kuna malalamiko ya mbolea ambayo haikuwafikia wananchi kwa msimu wa mwaka 2007/2008 na kuna mfarakano mkubwa katika baadhi ya vijiji hasa kijiji cha Isenzanya ambacho kiko katika Kata ya Nambinzo kule Mbozi sasa Mheshimiwa Waziri anapotoa taarifa kwamba hakuna mbolea iliyopotea haoni kwamba taarifa zake siyo sahihi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa hata msimu wa mwaka 2009/2010 mbolea yenye thamani zaidi ya shilingi milioni 100 imepotea kule Mbozi na baadhi ya watumishi walifikishwa Mahakamani lakini wameshinda kesi zile Mahakamani, lakini wameshinda kesi zile Mahakamani na mbolea imepotea na hawa ni watumishi wa Serikali: Kwa nini Serikali isichuke hatua za kinidhamu dhidi ya watumishi hao ambao wamehusika na upotevu wa mbolea nyingi kiasi hicho?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwanza kuwa kuna malalamiko, inawezekana yakawepo malalamiko. Lakini ni vizuri kupata malalamiko *specific* ili tuweze kuyashughulikia lakini suala la msingi lilikuwa linauliza juu ya jambo *specific* kwamba kuna mbolea ya shilingi milioni 30 iliyopotea. Tulifuatilia suala hili tukagundua haikupotea, hiyo ndiyo tuliyojibu, lakini kama kuna malalamiko zaidi ambayo Mheshimiwa Zambi angependa tuyashughulikie, atuletee malalamiko *specific* ili tuweze kuyashughulikia maana malalamiko ya jumla hayawezi kwisha duniani hapa, inategemea yako wapi na yanahusu nini.

Mheshimiwa Spika, suala la pili juu ya mbolea ambayo anasema ni ya shilingi milioni 100, ni kweli kulikuwa kumetokea dalili za ubadhirifu katika Wilaya ya Mbozi na Mkoa wa Mbeya ulichukua hatua kabla mbolea ile haijapotea. Uchunguzi umeendelea na ndiyo napata habari sasa hivi kwamba wale watu wameachiwa. Sasa kama wameachiwa, sisi tutawasiliana na wenye mamlaka ya nidhamu juu ya watu hawa kujua kama ni watu wanaostahili kuendelea na Utumishi wa Umma au hawastahili.

SPIKA: Sasa tunahamia Wizara ya Nishati na Madini, swali linaulizwa na Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mbunge wa Kyela.

Na. 179

Hatua za Kuwezesha TPDC iwe Imara Kibiashara

MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE aliuliza:-

Kwa kuwa katika Kikao cha Nne cha Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge la tarehe 31 Oktoba, 2008, Serikali ilitamka kuwa ilikuwa katika hatua za mwisho kuiwezesha *TPDC* kuagiza mafuta kwa wingi (*bulk procurement*) ili kuleta ushindani katika biashara ya mafuta nchini na vilevile kuipatia *TPDC* mgao wa asilima 50 kwa mauzo ya gesi asilia ili kuiwezesha kushiriki kikamilifu katika miradi ya utafutaji na uzalishaji wa mafuta na gesi:-

Je, utekelezaji wa hatua hizo mbili umefikia wapi sasa?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Harrison George Mwakyembe, Mbunge wa Kyela kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tarehe 31 Oktoba, 2008 wakati wa kujibu swali Na. 50 lililoulizwa na Mheshimiwa Fuya John Kimbita - Mbunge wa Hai hapa Bungeni, ilielezwa kwamba Wizara yangu ilikuwa kwenye hatua za mwisho za maandalizi ya Waraka wa Baraza la Mawaziri wa mapendekezo ya kuiwezesha *TPDC* kuagiza mafuta kwa wingi na pia Waraka wa kiasi cha asilimia ya mapato ya gesi kitakachobaki *TPDC*. Aidha, Wizara yangu ilifanya kazi ya utafiti wa kutuwezesha kulinganisha mfumo unaokusudiwa na uzoefu uliopatikana kwenye nchi nyingine ili kufikia ukamilishaji wa mchakacho huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maamuzi ya ngazi za Serikali kukamilika, ilionekana ni bora kwanza kupata ushauri wa kitaalamu wa namna ya kuagiza mafuta ya pamoja. Hivyo, *EWURA* ambao ndiyo wadhibiti wa sekta ya mafuta waliteua mdhibiti mwelezi, kampuni ya *Petroleum Development Consultant TPDC* ya Uingereza ambayo inafanya tathimini ya hali ya soko la mafuta la Kimataifa na kushauri namna ya kutekeleza azma ya Serikali ya kuagiza mafuta kwa shehena kubwa (*Bulk Procurement*) katika mazingira ya soko hili. Ugizaji wa mafuta kwa kutumia shehena kubwa unatarajiwa kuanza kwa mwaka huu wa 2010 mara baada ya kukamilika kwa tathimini na kuwasilisha ripoti ya mwisho inayoendelea ya kazi kufanywa na mshauri mwelekezi aliyeajiriwa na *EWURA*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *TPDC* kupewa mgao wa asilimia 50 ya mapato yatokanayo na gesi asilia, Serikali ilikwishafanya uamuzi wa msingi ya kuiruhusu *TPDC* kufanya kupewa sehemu ya mapato hayo. Hata hivyo, ilitakiwa utaratibu wa kuruhusiwa ufuate misingi iliyowekwa ambapo Wizara ya Fedha na Uchumi hujadili maombi ya mgao katika kikao maalumu cha masuala ya mgao (*rentention*) kabla ya kuingizwa katika mfumo wa bajeti ya Serikali kwa mwaka huo.

TPDC walikwisha wakilisha Wizarani mpango wao wa kazi (*Business Plan*) kwa kushiriki katika utafutaji na uzalishaji wa gesi na Wizara imeupitia na kuridhika nao. Kwa sasa Wizara yangu inakamilisha kuandaa mapendekezo ambayo yatapelekwa kwenye mamlaka ya ngazi husika kwa ajili ya maamuzi.

MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE: Mheshimiwa Spika, naomba niulize swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa uamuzi wa kuiwezesha *TPDC* kuagiza mafuta kwa wingi ulifanyika na Serikali miaka miwili iliyopita, hivyo hivyo uamuzi wa kuipatia *TPDC* mgao wa asilimia 50 ya mauzo ya gesi ili kuiongezea *TPDC* uwezo kifedha wa kushiriki kwenye miradi ya utafutaji na uzalishaji wa gesi na mafuta: Maelezo haya ya Serikali ya mchakato mrefu wa kutafuta ushauri wa kitaalamu kutoka nje sasa unamaanisha kuwa Serikali yetu ilipofanya maamuzi hayo miaka miwili iliyopita ilijitosa tu bila ushauri kamilifu wa kitaalamu?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, hapa pana masuala mawili, yako tofauti kabisa. Kuna suala moja la *retention* na suala *Bulk Procurement*. Swali hili tulijibu tarehe 31 Oktoba, 2008, tukasema kwa ufahamu wetu wa soko la Tanzania lilivyo tunatarajia mwanzoni mwa mwaka 2009 tutaanza na utaratibu wa *Bulk Procurement* kwa malengo mazuri ya kuhakikisha kwamba Tanzania ina-import mafuta *total* kama *2.4 millions tons*, sasa hiyo, watu wakianza kuleta mafuta kidogo kidogo tani elfu tano, tani elfu sita pale bandarini panakuwa na msongamano, bei ya mafuta inapanda kwa sababu ya *Economies of scale*.

Kwa hiyo, kuna mambo mengi tuliyosema tukifikia hatua ya maamuzi ya msingi kabisa kwamba *Bulk Procurement is a way forward*, lakini kwasababu ya mazingira maalumu ya masoko yetu kuna waagizaji wadogo wadogo wengi kama *DAPCO*, *OIL COM* na kadhalika, tukasema tuangalie namna ambayo hii *bulk procurement* inaweza kufanya kazi katika mazingira yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, baadaye tulipata fundisho moja tarehe 10 mpaka 13 Januari, 2009 tulipata *shortage* kubwa sana ya mafuta iliyotokana na mambo hayo ya sekta ambayo kusema kweli yalitupa mafundisho mazuri zaidi. Kwa hiyo, tulitumia mafundisho hayo na tumepata uzoefu wa nchi nyingine kujua kwamba katika mazingira maalumu ya soko la Tanzania na *demand* yetu ya 2.4 tons ambayo ni kama tani 120,000 kwa kila mwezi, tunafanyaje. Tumepata mafunzo hayo tukasema badala ya kuingia kwa pupa na kupata mtihani mkubwa zaidi, tuliangalie kwa watu wenye uzoefu. Tumepata mshauri mwelekezi amemaliza kazi yake Julai mwezi Agosti.

Mheshimiwa Spika, *EWURA* wameingia kwenye *public enquiry*, wamewaita wadau wote mwezi wa Oktoba, 2009, wamekutana nao wakatoa maamuzi Desemba, 2009 kwamba *we are going forward*. Kwa hiyo, tunafanya kazi ya hizi *results* za *EWURA* na yale ambayo tumebaini sisi wenyewe tunatarajia kwamba tutaingia ndani na kuweza kufanya hili jambo mwaka huu kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, hili suala la *retention* mapato yanayopatikana na gesi ni Shilingi bilioni 14.6 na wenzetu wa Wizara ya Fedha watakuwa tayari wameshakadiria hizi Shilingi bilioni 14.6 ziende kufanya kazi gani katika takwimu za Serikali. Sisi tunashauriana nao kusema watupe zile *at least 50%* ziingie kwenye masuala ya uwekezaji ya utafutaji na kadhalika kupitia hao *TPDC*. Kwa hiyo, ni maamuzi ndani ya Serikali kwa ajili ya kupata ufanisi juu ya jambo lenyewe na kusema kweli japo linaonekana limechelewa lakini ni kwasababu limepitia utaratibu wa kawaida.

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Waziri, majibu yamejitosheleza, ni zamu sasa ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, swali linaulizwa na Mheshimiwa Mchungaji Dr. Getrude Rwakatare, Mbunge wa Viti maalum.

Na. 180

**Kuongeza Somo la Ujasiriamali kwenye
Mtaala wa Elimu**

MHE. MCH. DR. GETRUDE P. RWAKATARE aliuliza:-

Kwa kuwa mfumo wa elimu yetu haumrusu mhitimu kujiajiri badala yake inamfanya awe tegemezi wa ajira tu:-

Je, Serikali itakuwa tayari kuongeza somo la ujasiriamali kwenye Mtaala wa Elimu kuanzia Shule ya Msingi hadi Chuo Kikuu?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mchungaji Dr. Getrude Rwakatare, Mbunge wa Viti Maalum, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, wanafunzi katika Shule za Sekondari na Vyuo Vikuu wanapata wanapata mafunzo ya ujasiriamali kupitia masomo mbalimbali wanayosoma katika ngazi zote za elimu. Serikali kwa kutambua umuhimu wa somo la ujasiriamali, iliandaa waraka wa Elimu Na.2 wa mwaka 2006. Nyaraka hizi zimeweka bayana masomo atakayosoma mwanafunzi wa Shule ya Msingi na Sekondari.

Mheshimiwa Spika, kutokana na nyaraka hizi, mitaala imeboreshwa ili kumwezesha mhitimu aweze kupimwa ujuzi/maarifa.

Mheshimiwa Spika, kuanzia Darasa la Kwanza hadi Vyuo Vikuu, wanafunzi wamekuwa wakifundishwa somo la stadi za kazi/au ujasiriamali katika ngazi husika. Somo hili huwajengea uwezo wa kuweza kujitegemea kwa kujiajiri kutokana na ujuzi wanaoupata.

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu kuwa wanafunzi watakaohitimu sasa hawatakuwa tegemezi kwa kuwa watakuwa na ujuzi na stadi mbalimbali.

Na 181

Refresher Course

MHE. SAID AMOUR ARFI aliuliza:-

Kwa kuwa kozi za muda mfupi (*Refresher Course*) zilisaidia sana katika kuboresha taaluma ya Ualimu, mbinu za ufundishaji na maadili:-

(a) Je, ni walimu wangapi wamepata mafunzo hayo kwa mwaka 2006 na 2007?

(b) Je, ni walimu wangapi kutoka Wilaya ya Mpanda wamepata taaluma hiyo?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda Kati lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitambua umuhimu wa mafunzo kazini kwa walimu katika kuboresha taaluma na mbinu za kufundishia na kujifunzia kwa kadri mabadiliko yatakavyojitokeza katika nyanja za kijamii, Uchumi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, Mafunzo ya Walimu kazini Rekebishi (*Refresher Courses*) yana sura ya Kitaifa na utekelezaji wake umekuwa ukisimamiwa na Vyuo vya Ualimu katika kanda na hivyo kutoa fursa kwa walimu kutoka Halmashauri mbalimbali kuweza kujiendeleza kitaaluma.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2007 mafunzo ya walimu kazini yaliendeshwa kuboresha ufundishaji wa masomo ya sayansi ikiwemo fizikia, Kemia, Elimu ya Viumbe, Hisabati na *English* kwa Walimu 3.753 wa Sekondari.

Aidha, Mafunzo Kazini Rekebishi yamekuwa yakitolewa kwenye vituo vya walimu (*Teachers Resources Centers – TRCs*) chini ya Halmashauri. Ili kuhakikisha kuwa kila mwalimu anafikiwa, kuna utaratibu wa kuendesha mafunzo haya kwa kila shule (*school based training*) kwa kadri hitaji la mafunzo linavyojitokeza.

MHE. SAID AMOUR ARFI: Mheshimiwa Spika, napenda niamini majibu yanaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba ni sahihi. Lakini pia nitapenda anieleze ni kwa nini matokeo ya mitihani ya Shule za Misingi na Sekondari Kidato cha Pili na Kidato cha Nne katika masomo hayo hayo ambayo walimu hao hao aliowataja wamepata mafunzo, matokeo yake yamekuwa mabaya, watoto wetu hawafundishiki, au tatizo liko kwa walimu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Shule za Misingi na Sekondari umekuwa na mafanikio makubwa kwa maana ya udahili wa wanafunzi, lakini matokeo yake ni watoto wengi kufeli kwa sababu hakukuwepo na maandalizi mazuri ya walimu na kupewa mafunzo ya muda mfupi: Je, sasa Serikali imejipangaje ili kuondoa kasoro hii ya kuwa na walimu ambao wanaweza kutoa mafunzo stahiki kwa watoto wetu?

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba idadi ya wanafunzi ambao tunao katika Elimu ya Misingi na Elimu ya Sekondari imeongezeka na hatua mbalimbali zinachukuliwa ili elimu iboreke.

Katika mwaka 2006/2007, 2007/2008 na 2008/2009 wanafunzi katika Elimu ya Misingi na Elimu ya Sekondari hawakufanya vizuri katika masomo ya Hisabati na Kiingereza. Katika Hisabati ni asilimia ya vijana 17 tu waliofaulu mtihani wa Hesabu mwaka 2006/2007 na 2008/2009 idadi hii iliongezeka kidogo na kufikia asilimia 20.

Mheshimiwa Spika, katika somo la Kiingereza, watoto waliofaulu katika miaka yote hii hawakuzidi asilimia 35. Tatizo hili ni kubwa na katika mkutano wetu maalum mkuu wa elimu tuliofanya mwezi Februari mwaka huu tumeazimia kuchukua hatua mbalimbali ili kupambana na tatizo hili. Ni kuongeza mafunzo rekebishi ya walimu mashuleni ili walimu waweze kuwa mahiri zaidi katika masomo haya.

Mheshimiwa Spika, kwa hili nawaomba Waheshimiwa Wabunge tushirikiane hasa katika mambo mbalimbali. Katika eneo la Sekondari masomo hayo hayo watoto wanafanya vibaya sana na katika masomo ya Sayansi ni budi tuweke juhudi kubwa kuongeza Maabara Shuleni ili kuongeza ufanisi wa kufaulu.

Mheshimiwa Spika, kwa hatua ambazo tunachukua sasa na ambazo tutaendelea kuchukua tukianza na mradi wa *MESS* Na. II mwaka huu mwezi Juni, mimi nina imani kabisa kwamba matatizo haya makubwa yataondoka. Ahsante sana.

Na. 182

**Veta Kuanzisha Kitengo cha Mafunzo kwa Vijana
Walioathirika na madawa ya Kulevya**

MHE. DIANA M. CHILOLO aliuliza:-

Kwa kuwa kuna Vyuo vya Ufundi *VETA* kwa kila Mkoa, sasa Serikali inapanga kila Wilaya iwe na Chuo cha *VETA* na kwa kuwa Vyuo hivi vinafanya kazi nzuri sana ya kusaidia Mitaani na vijijini wakiwa wameathirika na madawa ya kulevya:-

Je, Serikali haioni kwamba sasa kuna haja kila Chuo cha Ufundi (*VETA*) kuwa na kitengo cha mafunzo kwa vijana walioathirika na madwa ya kulevya?

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo - Mbunge wa Viti maalumu Singida napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja ya majukumu ya *VETA* ni pamoja na kutoa elimu ya stadi za kazi, yaani (*Vocational Education*) kwa vijana wote wa Kitanzania ili waweze kuingia katika soko la ajira na waweze kukabiliana na mazingira yanayowazunguka. Aidha, sifa ya kudahiliwa katika vyuo vya *VETA* ni pamoja na kuhitimu Elimu ya Msingi au Kidato cha Nne ambapo kabla ya kudahiliwa ufanyike mtihani wa usaili.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Diana Chilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kozi zote za Ufundi Stadi zinazofundishwa katika Vyuo vya *VETA* zinajumuisha somo la Stadi za Maisha ambalo ni somo la lazima. Kati ya mada zinazofundishwa katika somo hilo la Stadi za Maisha ni pamoja na madhara yanayotokana na dawa za kulevya na virusi vya UKIMWI na jinsi ya kujiepusha nayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vijana waliopo mafunzoni pia hupatiwa ushauri nasaha ili kujiepusha na utumiaji wa dawa za kulevya na upimaji wa hiari wa virusi vya UKIMWI. Kwa mafunzo haya vijana wote katika vyuo vya VETA wakiwemo walioathirika kwa dawa za kulevya, husaidiwa kurudia maisha ya kawaida.

Aidha walimu wa mafunzo ya ufundi, hupatiwa mafunzo ya stadi za maisha na namna ya kuzifundisha katika kozi za Ualimu wa Ufundi yanayotolewa katika Chuo cha Ualimu wa Ufundi Morogoro. Kutokana na hiyo hakuna ulazima wa kuwa na kitengo maalumu cha mafunzo kwa vijana walioathirika na dawa za kulevya. *(Makofi)*

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na vyuo vya VETA napenda kuuliza swali mmoja la nyongeza.

Kwa kuwa vijana hawa walioathirika na dawa za kulevya, siyo rahisi kutuma maombi wala kwenda kufanya usaili ili waweze kujiunga na vyuo vya VETA, na kwa kuwa vijana hawa ni kero katika familia, jamii na ni aibu kwa Taifa, je, Serikali haiwezi kuchukua ombi langu kwa makusudi kabisa watafakari na waone njia ya makusudi kuwakusanya vijana hawa kwa nguvu kuwapeleka Vyuo vya VETA, kuwawekea kitengo maalumu ili adha hii inayopatikana mijini iondoke?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA): Mheshimiwa Spika, lazima tukubaliane kwamba Vyuo vya VETA au Mafunzo ya Ufundi ni kwa ajili ya wanafunzi ambao wapo *sober* na ambao wako tayari kusoma. Kwa mwanafunzi ambaye bado ana *hang over* ya dawa za kulevya siyo rahisi kumbeba na kumpeleka katika kituo cha ufundi au VETA kwenda kusoma, kwa hiyo, tunategemea kwamba vijana wale ambao wameshaondokana na dawa za kulevya na wao wamemaliza darasa la saba kama sifa mojawapo au kidato cha nne, basi sisi tunaoishi katika mazingira ya vijana hawa tuwatie moyo na tuwashauri waweze kujiunga katika Vyuo vya VETA kwa kutumia utaratibu huu tuliouweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini siyo rahisi sisi kuandaa mpango kuwatafuta vijana walioathirika na kuwapeleka katika Vyuo vya VETA pamoja na ushauri mzuri wa Mheshimiwa Diana Chilolo, mimi nafikiri wananchi na wengine ambao wanaweza kufanya kazi hii wafanye kama ilivyofanyika katika kituo cha Ulemo pale Singida kwa mama Sara Mkumbo ambaye alishirikiana na Mheshimiwa Martha Mlata kupeleka vijana pale na kuwafundisha masomo mengine tofauti. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naongeza muda kidogo kwa sababu muda wetu wa maswali ulichukuliwa na kuapishwa kwa Waheshimiwa leo, kwa hiyo, sasa nitaruhusu maswali mawili mafupi ya nyongeza.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Spika, ahsante Mungu akubariki kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri na kwamba anakitambua kile chuo cha Ulemo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, chuo kile bado miundombinu yake siyo mizuri, maji pamoja na umeme, je Wizara inasema nini kukisaidia chuo hicho ili wananchi wa Iramba waweze kufaidika?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA): Mheshimiwa Spika, naomba niseme tu kwamba tutatuma watalaamu wetu wakaangalie kile chuo tuone kama tunaweza kusaidaje katika matengenezo na kuhakikisha kwamba kuna maji. *(Makofi)*

MHE. BUJIKU P. SAKILA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya mwaka jana na Bajeti inayoisha mwaka huu Serikali ilisema kwamba ingejenga Chuo cha Ufundi Wilayani Kwimba katika Kijiji cha Kigeboi, wananchi wa Kwimba wangenda kusikia hatua ya ujenzi huo umefikia hatua gani?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA): Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa tuliahidi kwamba katika Ilani yetu ifakapo mwaka 2010 tutakuwa tumejenga vyuo hivi.

Mheshimiwa Spika, Vyuo hivi ni vingi katika Wilaya zote ambazo zilikuwa zimeshatembelewa na kuangaliwa, hali halisi ya mazingira ya stadi ambazo tunaweza kuanzisha katika vyuo hivi, lakini naomba niseme tu kwamba pamoja na juhudi na nia njema ya Serikali fedha tulizokuwa tumetarajia kutoka kwa wahisani bado hatujazipata, lakini nia iko pale pale, na mara tutakapopata pesa tutaanza ujenzi. Kwa sababu hatua za awali zimeshafanyika katika maeneo mengi katika Wilaya hizi. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Bujiku endelea kuvumilia. *(Kicheko)*

Na. 183

Mabadiliko ya Sheria ya Ndoa na Mirathi na Uhitaji wa Kadhi

MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB (K.n.y MHE. YAHYA KASSIM ISSA) aliuliza:-

Kwa kuwa wakati wa Mkutano wa Kumi na Mbili wa Bunge lilijitokeza suala la Marekebisho ya Sheria ya Ndoa na Mirathi; na kwa kuwa ilithibitika kwamba baadhi ya dini hususani ya Kiislam zinafuata taratibu zilizowekwa katika *Quran* Tukufu na hakuna uwezekano wa kubadili taratibu hizo kwa njia yoyote ile:-

(a) Je, Sheria hiyo itatumika vipi Mahakamani wakati kuna suala la dini ya Kiislam juu ya ndoa na mirathi na Hakim mhusika ni Mkristo?

(b) Je, Serikali haioni kuwa utaratibu na kutokuwepo Kadhi Tanzania Bara unawabana Waislamu?

(c) Je, kuna sababu gani za msingi za kutokuwepo kwa Kadhi huyo kwa kuwa hata zamani wakati wa utawala wa Waingereza Kadhi alikuwepo bila kuathiri Ukristo wao?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba uniwe radhi kwamba tofauti na kawaida yangu jibu langu safari hii litakuwa refu sana kutokana na kwamba swali lenyewe ni maswali matatu tofauti, kwa hiyo, inabidi niyajibu kwa ufasaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mbunge wa Chwaka, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, tangu tumepata Uhuru Serikali yetu imekuwa ikirekebisha, ikifuata na kutunga sheria za nchi pale inapobidi ili kukidhi matakwa ya wananchi wetu na pia kwenda sambamba na maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa yanayoendelea kujitokeza kila wakati duniani. Kwa sababu hizo Serikali yetu inayodhamira ya kufanya marekebisho katika sheria ya ndoa na sheria za urithi na mirathi kwa kuwashirikisha wananchi kupitia waraka maalum wa Serikali. Hii inatokana na ukweli kwamba maeneo yanayohusu sheria hizi yanagusa sana imani, mila na desturi za wananchi wetu wakiwemo Waislamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika imani hizo kila dini au madhehebu ya dini wana utaratibu wa kufungisha ndoa na namna ya kurithishana mali. Serikali kwa upande wake inapaswa kuwa na sheria za nchi zinazotambua taratibu za ndoa na mirathi lakini pia na yenyewe ikiwa na sheria ambayo pamoja na kutambua taratibu hizo kuwa na vipengele katika sheria ambayo vitaweza kumlinda mwananchi yeyote ambaye kwa upande wake hafungamani na taratibu za kidini au kimila. Nia ya Serikali ni kuboresha sheria hizi ili ziweze kuwanufaisha wananchi wote.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Sheria hiyo itaweza kutumika mahakamani kwa sababu itatambua kuwepo kwa taratibu za ndoa na mirathi za dini za kimila. Aidha, zitaweka pia mazingira ambayo yatamwezesha hata mwananchi asiyefungamana na madhehebu au kufuata mila na desturi za kabila lolote nae aweza kupata haki katika mahakama za nchi yetu.

Wale watakaona kwamba kutokana na imani na maisha yao watahitaji kutatua migogoro ya ndoa na mirathi kwa kuzingatia dini au mila na desturi wataweza kufanya hivyo kwa kuwa lengo la sheria hizo ni kuweka utaratibu utakaotambua mazingira hayo. Mwananchi atakayeamua kufuata sheria ya nchi katika kutatua mgogoro wa ndoa au mirathi, basi atakayeamua atakuwa mtu yeyote aliyepewa dhamana ya kutolea uamuzi suala hilo bila ya kujali dini, rangi, kabila au jinsia yake.

(b) Mheshimiwa Spika, kutokuwepo kwa Kadhi Tanzania Bara hakuwabani Waislamu katika imani zao juu ya masuala ya ndoa na mirathi. Napenda niseme kwamba tangu tulipopata Uhuru na kuwa na mfumo mmoja wa mahakama kuanzia ngazi ya Mahakama za Mwanzo hadi Mahakama ya Rufaa mashauri mengi yameamuliwa na Mahakama zetu na wananchi wamekuwa wakiridhia juu ya mfumo huo na kupata haki zao pale walipoamua mashauri yao yaamuliwe kwa kufuata misingi ya dini au mila na desturi zao.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali haijawahi kuzuia kuwepo kwa Kadhi. Hata hivyo hoja ambayo ipo ni iwapo mfumo wa Kadhi uingizwe katika mfumo wa Mahakama za nchi chini ya usimamizi wa Serikali au uwe ni mfumo wa kuanzishwa na Waislamu wenyewe lakini Serikali ikitunga sheria zilizokubaliwa na madhehebu yote ya Waislamu kwa ajili ya wao wenyewe kuzitumia.

Katika Mkutano wa Kumi na Mbili wa Bunge letu Tukufu, nilieleza msimamo wa Serikali wa kukubali sheria za kiislamu zitafsiriwe na kuingizwa katika msimamo wa Serikali wa kukubali sheria za kiislamu zitafsiriwe na kuingizwa katika sheria za nchi. Serikali itaendelea kushirikiana na Waislamu katika kufikia muafaka wa suala hili. *(Makofi)*

MHE. MANJU S. MSAMBYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Waziri nadhani hakujiielekeza kujibu sehemu (c) ya swali lililoulizwa, kwa bahati nzuri mimi nimesoma elimu ya msingi ya mwanzo na watoto wa Kadhi pale Kigoma, kwa nini Waziri asituambie ni sababu gani zilizopelekea ofisi ya Kadhi kuondolewa ambayo sasa hivi imekuwa ni dai la Waislamu kwa muda mrefu? *(Makofi)*

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, mwaka 1963 wakati Bunge lako Tukufu likijadili sheria ambayo iliunganisha Mahakama zote, jambo la msingi pale ilikuwa ni suala la kuleta umoja na kuondoa dhana ya ubaguzi wa dini, kabila, hisia na kadhalika. Ukisoma *Hansard* za mwaka 1963 utakuta hayo ndiyo yalikuwa madhumuni yake na mpaka sasa tunadhani hayo ndiyo madhumuni mazuri. *(Makofi)*

Lakini tunaposema dunia huenda ikibadilika, kama hivi sasa tunaona ipo haja ya kufanya hivyo basi ni jambo la kufikiria tu kulirudisha, lakini imani yangu kwamba bado suala zima la kuunganisha nchi yetu kuwa na sheria moja inayokata kwa kila mtu ni la msingi sana. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda umekwishapita wa maswali, sasa ni matangazo, nasikitika naanza na Tanzania, Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Felister Bura, amefiwa na mumewe jana saa tatu usiku, ofisi inafanya utaratibu wa kuuleta mwili kutoka Dar es Salaam leo, taratibu zingine mtaelezwa kuhusu maziko. Msiba uko nyumbani kwa Mheshimiwa Felister Bura. Kwa wale ambao wanapenda kwenda kutoa ubani au kuwaliwaza watoto na Mbunge mwenzetu pia basi mjisikie huru, nadhani anaishi *Area D*, Mungu aiweke mahali pema peponi roho ya marehemu, Amina.

Kutokana na hilo basi Mheshimiwa Ledian Mng'ong'o ameomba wanawake wote mkutane saa saba katika Ukumbi wa Pius Msekwa kwa taratibu za kawaida za kupanga namna ya kumfariji mwenzetu kwa karibu zaidi.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wa Mheshimiwa Janeth Zebedayo Mbene, ana wageni wake ambao ni mwanae Modesta asimame tafadhali, Abela na Ndugu Amani Ngowi ambaye ni kaka yake, karibuni sana. Tunashukuru kwamba mmemsindikiza Mheshimiwa katika hatua yake hii muhimu ya maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu, anaye mgeni wake ambaye ni Mheshimiwa Juma Duni Haji, Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar na ni Mjumbe pia wa Kamati Kuu ya CUF, karibu sana Mheshimiwa Duni tunafurahi sana kukuona hapa, ila ninaushauri tu kwamba kidogo maneno yako katika hotuba huwa makali sana, punguza kidogo tu lakini mantiki ni safi kabisa. *(Makofi/Kicheko)*

Wageni wa Mheshimiwa Idd Azzan, Mbunge wa Jimbo la Kinondoni ni viongozi 30 wa Umoja wa Vijana Chama cha Mapinduzi kutoka Kata zote kumi za Jimbo la Kinondoni, Wenyevidi wa Kata, Makatibu wa Kata, Wahamasishaji ngazi ya Kata, wakiongozwa na Ndugu Mossy Khamis Mfaume, Katibu wa UVCCM Wilaya ya Kinondoni tafadhali asimame, Ndugu Muhsini Ramadhani, Katibu Uhamasishaji Wilaya, Ndugu Kassim Kavitenda, Mkuu wa mafunzo UVCCM Mkoa wa Dar es Salaam, wageni wote wa Dar es Salaam Kinondoni wasimame ili Wabunge waweze kuwaona. *(Makofi)*

Pamoja na mambo mengine, Mheshimiwa Azzan amefanya utaratibu huu ili hao wote waje wamuenzi kutokana na nishani aliyopata jana ile medali, golikipa wa timu ya Bunge na Bunge lina ushindi wa kihistoria kwa hiyo kwa kweli tunawashukuru sana Kinondoni kwa jinsi mlivyokuja, ni dhahiri kwamba mnamuunga mkono Mbunge huyu kama ambavyo Spika naye ni shabiki sana wa Mheshimiwa huyu. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, mgeni wa Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi ni Ndugu Marwa Siagi, Mkurugenzi wa *Musoma Utalii College* na Mweka Hazina wa CCM Wilaya ya Musoma Mjini, karibu sana kutoka Musoma tunafurahi kukuona. *(Makofi)*

Wageni tisa kutoka ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, wakiongozwa na Ndugu yetu Ludovick Utouh, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, karibuni sana tunafarijika sana mara kwa mara kukuona kwa sababu kazi zetu zinashabihiana na mambo yako ya Ukaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Maria Hewa, ana mgeni wake Ndugu Malando Habari, Mwandishi wa Habari kutoka Mwanza, karibu sana. Wageni wa Waheshimiwa Wabunge kutoka Mkoa wa Mbeya, ambaye ni ndugu Verena Shumbusho, Katibu wa CCM Mkoa wa Mbeya naomba usimame karibu sana, Ndugu Bashiri Madiki, Katibu wa Siasa na Uenezi wa CCM wa Mkoa karibu sana na Ndugu Godfrey Sanga, Katibu Kata wa CCM Kata ya Vyawa Mbozi, karibuni sana kutoka Mbeya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Monica Mbega ana mgeni wake ambaye ni Mchungaji Rose Loiser Kutoka Iringa Mjini karibu sana. Wageni wa Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa ambao ni Ndugu Ali Salum na Ndugu Issa Ali wasimame tafadhali, karibuni sana, hawa nina hakika ni wanachama wa Chama cha *CUF* hawa, ingawa mimi Mheshimiwa Khalifa ni rafiki yangu sana lakini tuko vyama tofauti. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mbunge wa Busanda ana mgeni mmoja, Mheshimiwa Leonard Shiganga, Diwani wa Kata ya Bukoli, karibu sana. Wapo wageni wa Mheshimiwa Al-Shymaa Kwegyir kutoka Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu Tanzania linalounganisha Vyama vya Kitaifa vya Watu wenye Ulemavu mbalimbali wageni hao ni kama ifuatavyo, Ndugu Lupi Mwaisaka, Mwenyekiti, Ndugu Felician Mkude, Katibu Mkuu, Ndugu Abrahmani Lugone, Mtunza Hazina na Ndugu Kudra Munisi, Mkalimani wa lugha ya alama, huyu Mkalimani ni muhimu kwa sababu Mwenyekiti anahitaji huduma zake nadhani mnanielewa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni wengine ambao nimeletewa vikaratasi hapa ni pamoja na wageni wa Mheshimiwa Mwanne Mchemba ambao ni Ndugu Heri Tuwa na Bi Hadija Tuwa, hawa ni wafanyakazi wa Kampuni ya *Zain Dar es Salaam*, karibuni sana. Nadhani huo ndiyo mwisho wa matangazo ya wageni, sasa matangazo ya vikao na matangazo mengine. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwanza Mheshimiwa John Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali anaitisha Kikao cha Kamati leo tarehe 12 Februari, 2010 saa nane na nusu mchana katika ukumbi namba 231 anasisitiza ni mkutano mfupi na Wajumbe wote wa *PAC* wahudhurie kwa sababu Mkutano huo pamoja na mambo mengine utapanga ratiba ya kazi, kwa hiyo, saa nane na nusu ukumbi namba 231. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi ameniomba nitangaze kwamba Wajumbe wote wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Wajumbe wa Hesabu za Serikali, Wajumbe wa Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma, Wajumbe wote wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwamba ile inayoitwa *Forum ya Parliamentary Public Expenditure* itafanyika siku mbili kesho na kesho kutwa kuanzia saa mbili asubuhi kesho, Ukumbi wa Msekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mudhihir Mohamed Mudhihir, Mbunge wa Mchinga ameniomba nitangaze kwamba kile kitabu chake alichokitunga cha Mwele Bin Taaban, kimezinduliwa jana na Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba yangu, kitabu hiki kinazungumzia wapiga kura wetu na wajibu wetu Wabunge katika dunia ya tatu, kinapatikana eneo la uwanja wa sherehe za Bunge na bei yake ni rahisi tu shilingi elfu tano. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tafadhalini mwenzetu amechomoza ameandika kitabu kizuri kimetoka kwa wakati, kwa sababu tunakihitaji sana kitabu kinachotuelekeza namna ya kushughulika na wapiga kura wetu katika hali ambayo ni kama ya riwaya lakini ina mafunzo mazuri, basi kila Mbunge ajitahidi kupata kitabu hiki, mimi ninacho tayari. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ofisi inaomba kutangaza ifuatavyo, kwamba tunao Wabunge wawili ambao wametupa heshima kubwa mwaka jana kwa kutambuliwa Kimataifa, wa kwanza ni Mheshimiwa Anna Abdallah, bahati mbaya naona hayupo ametunukiwa na Jamhuri ya Afrika Kusini Tuzo ya *The Companion of Oliver Thambo* katika amepata nishani ya *Silver*, kama ya daraja la pili, lakini wale mnaofahamu historia Oliver Thambo ndiye aliyeachiwa wakati Mzee Mandela yupo jela, yeye ndiye alikuwa anaendesha ANC, kwa hiyo kwa kumbukumbu uwanja wa ndege unaitwa jina la Oliver Thambo lakini jina hilo hilo sasa linatambua wale waliotoa mchango maalum na Mheshimiwa Anna Abdallah akiwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro katika miaka ya 1978 na 1979 aliweza kuwapatia ardhi katika eneo la Mazimbu chama cha *African National Congress* kilichokuwa kikiongoza mapambano dhidi ya ubaguzi wa rangi. Aliwalea vijana vizuri kiasi kwamba kule Afrika Kusini anafahamika kabisa kama Mama Anna popote anapopita, tunashukuru sana mwenzetu kwa tuzo hii ambayo ni heshima kwa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Abdulkarim Esmail Shah, Mbunge wa Mafia, mnamo Novemba 2009 alituwakilisha katika Mkutano kule *Port Villa Vanuatu* hiki ni kisiwa kilichopo *Pasific*, Mkutano huu ulikuwa unazungumzia mabadiliko ya hali ya hewa na ulikusanya watu mbalimbali mashuhuri wanaotoka katika maeneo ya visiwa duniani. (Makofi)

Mheshimiwa Shah alipofika kule kutokana na umahiri alioupata hapa Bungeni alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa kwanza wa mtandao wa Wabunge wa Visiwa vya Bahari ya Hindi, Mheshimiwa Shah naomba usimame, ahsante sana. Huyu ndiye Mwenyekiti wa Wabunge wote wa Visiwa vya Bahari ya Hindi, ukiacha Zanzibar ambayo iko Tanzania. (Makofi/Kicheko)

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, tunampongeza kwa kuwa Mwenyekiti wa kwanza na jambo hili nadhani Mafia wamesikia, kwa hiyo, wale waliokuwa wanataka kuyumba yumba waelewe kwamba Mbunge wao ni madhubuti kabisa. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, leo mara baada ya kuahirishwa Bunge tutakuwa na hafla fupi sana ya kupokea vifaa mbalimbali vilivyotolewa na CAG chini ya mradi wa *Public Finance Management Reform Project*, ni vifaa vyenye thamani ya mamilioni ya fedha kwa ajili ya kuboresha uwezo wa Kamati zetu za *oversights*, hafla hiyo itafanyika ukumbi wa Spika, jengo la Utawala naomba wawakilishi mbalimbali wa Kamati zetu na Wabunge wengine waweze kuwa pale. (Makofi)

Si vibaya wakawapo Wabunge ambao wanaweza kupiga vigelegele kwa sababu ni utamaduni wetu unapopata mambo ya furaha basi kunakuwa na chereko na vigelegele. Karibuni sana mara baada ya kuahirisha Bunge. Ahsante sana kwa hayo na pia uvumilivu wenu. (Makofi)

Kuna tangazo lingine hili limetoka kwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Christopher Chiza, nitalisoma kwa sababu hayo siyo maoni yangu ni maoni yake huyu. Kesho tarehe 13 Februari, yule Bingwa wa Tanzania Bara katika medani ya mchezo wa soka *Dar Young Africans* wataliwakilisha Taifa katika mchezo Kablu Bingwa Afrika, nawaomba Wabunge wote wakiwemo Profesa Kapuya na Profesa Sarungi wajitokeze kuishangilia Yanga. Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge. (Kicheko)

UCHAGUZI WA WAJUMBE KWENYE TAASISI YA ELIMU YA JUU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, *Returning Officer*, Katibu wetu alitoa waraka kuhusu nafasi iliyopo katika la Taasisi ya Teknolojia Mbeya (*Mbeya Institute of Science and Technology*) na nafasi hii kwa bahati sasa imekuwa haina ushindani, tumepokea jina moja tu. Kwa hiyo, namtangaza mwakilishi huyo kwamba ni Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge amepata nafasi hiyo. Ahsante sana. Ahsante hongera sana kwa kupata nafasi hiyo. (*Makofi*)

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Uchaguzi wa Mwaka 2009 (*The Electoral Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2009*)

(*Kusomwa Mara ya Pili*)

WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:
Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa hoja ambayo iko mbele yetu na mimi nimeguswa na kifo cha mume wa Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Felister Bura. Naomba nitoe rambirambi zangu kwa Mheshimiwa Felister Bura.

Mheshimiwa Spika, hayati Bura atakumbukwa sana na Bunge hili hasa kwa vile alihusika sana na ujenzi wa ukumbi huu mzuri wa Bunge lakini pia ujenzi wa majengo yale ambayo sasa hivi tunatumia kama Ofisi za Bunge na pia ukumbi wa Pius Msekwa wakati huo akiwa Mkurugenzi wa *LAPF*. Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika, leo tumewapokea Wabunge wapya, Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu na Mheshimiwa Janet Mbene. Naomba nichukue fursa hii kusema kwamba tunawakaribisha sana, historia ya Chama cha Wananchi (*CUF*) na hasa matukio ya kisiasa ya hivi karibuni inamhusia sana Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu hivyo Mheshimiwa Ladhu anaingia katika nyumba hii akiwa na utajiri mkubwa sana wa kisiasa ambao utalisaidia Bunge letu. Tunasema karibu sana Mheshimiwa Ladhu. (*Makofi*)

Historia ya utajiri wa siasa wa Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene kwa Bunge hili nao siyo haba. Mheshimiwa Mbene anajulikana baina ya Wabunge hasa kwa umahiri aliyonyesha wakati wa kinyang'anyiro cha Ubunge wa Bunge la Afrika Mashariki. Lakini naamini pia Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Naibu wake wanafahamu kwamba baada ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwezi Oktoba, 2009 katika Serikali zetu karibu 12,000 Mwenyekiti mmojawapo aliyepatikana siyo mwingine naye ni Janet Mbene. Inawezekana katika wale Wenyeviti wanaokaribia 12,000 wa Serikali zetu za Mitaa Mheshimiwa Janet Z. Mbene akawa ndiyo msomi kuliko wote kwa sababu Mheshimiwa Mbene amebobea sana katika taaluma ya menejimenti naye tunamkaribisha sana katika Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liupokee, liujadili na hatimaye kuupitisha Muswada wa Sheria uitwao *The Electoral Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2009*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijaelezea kwa undani Muswada huu naomba nitoe shukrani za kipekee kwako na ofisi yako kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Muswada huu mbele ya Bunge lako Tukufu kwa wakati huu. Pia, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa George Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala pamoja na Wajumbe wa Kamati yake kwa kuujadili na hatimaye kupendekeza uletwe mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Naomba pia nimshukuru Ndugu Peniel Lyimo, Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Ndugu Fanuel Mbonde, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu na wataalam wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu, pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wataalam wake akiwemo Mwandishi Mkuu wa Sheria kwa maandalizi ya Muswada huu yaliyowezesha sasa niufikishe katika hatua hii.

Mheshimiwa Spika, Muswada ulioko mbele yetu unakusudia kufanya marekebisho katika Sheria ya Uchaguzi, Sura ya 343 na Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Sura ya 292 ili kuondoa mapungufu mbalimbali ambayo yamekuwa yakijitokeza katika chaguzi zilizopita kwa lengo la kuiwezesha Tume ya Uchaguzi kuendesha chaguzi kwa ufanisi zaidi. Baadhi ya mapungufu yanayokusudiwa kurekebisha na Muswada huu ni pamoja na Tume kutokuwa na madaraka ya kuwateua Waratibu Waandikishaji wa Mikoa, kipindi cha kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kutotajwa bayana katika Sheria, Sheria kutoruhusu baadhi ya Watendaji wa Tume kuingia katika vituo vya kupigia kura ili kufuatilia zoezi la upigaji kura na marekebisho yanayotokana na Sheria mpya ya Matumizi ya Fedha Nyakati za Uchaguzi (*The Election Expenses Act*) inayotarajiwa kuanza kutumika sambamba na Muswada huu ambao sasa hivi utajadiliwa na Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Muswada ulioko mbele yetu umegawanyika katika sehemu kuu nne. Sehemu ya Kwanza ni utangulizi yaani Jina la Sheria ya Marekebisho. Sehemu ya Pili, inahusu marekebisho yanayopendekezwa kufanyika katika Sheria ya Uchaguzi Sura ya 343 kama ifuatavyo; katika Ibara ya 3, Muswada unapendekeza kuongeza tafsiri ya maneno mbalimbali katika Sheria ya Uchaguzi. Aidha, inapendekezwa kurekebisha tafsiri ya maneno uteuzi na Mbunge ili kujumuisha katika tafsiri ya uteuzi, uteuzi wa Wabunge Wanawake wa Viti Maalumu; na katika tafsiri ya Mbunge, Mbunge wa Kuteuliwa wa Viti Maalum vya Wanawake. Tafsiri hizo hazikuwepo katika sheria ya awali ya mwaka 1985. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ibara za 4 na 5 zinapendekeza marekebisho katika mafungu ya 7 na 7A ya Sheria ya Uchaguzi ili kuipa Tume mamlaka ya kuteua wasimamizi wa uchaguzi kutokana na ofisi au sifa zao tofauti na ilivyo sasa ambapo Tume imebanwa ili kuteua Wasimamizi wa Uchaguzi kutokana na ofisi tu. Vilevile inapendekezwa katika Ibara ya 7A kuipa Tume mamlaka ya kuteua waratibu waandikishaji wa Mikoa na kutambua uwepo wa waandishi wasaidizi wa vituo na watendaji wengine wanaoweza kuteuliwa na Tume kwa ajili ya kuboresha Daftari la Taifa la Kudumu la Wapiga Kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 6 inapendekeza marekebisho katika fungu la 15 la Sheria ili kuweka bayana kipindi cha kufanya uboreshaji wa Daftari la Taifa la Kudumu la Wapiga Kura kuwa mara mbili kati ya Uchaguzi Mkuu mmoja na unaofuatia. Aidha, kwa lengo la kuongeza

uwazi katika zoezi la uandikishaji wapiga kura, inapendekezwa katika Ibara ya 7 kuwa na fungu jipya la 15A katika sheria linalotoa nafasi kwa vyama vya siasa kuteua mawakala watakaokuwepo katika vituo vya kuandikisha wapiga kura kama ilivyo wakati wa upigaji kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 9 inapendekeza marekebisho katika fungu la 35A la Sheria ya Uchaguzi kwa lengo la kupunguza muda wa kusubiri kabla ya kufanya uteuzi wa mgombea mwingine wa Urais au Umakamu wa Rais inapotokea wagombea hao wamefariki ili uwe ndani ya siku 14 badala ya siku zisizopungua 21 za sasa. Muda wa sasa umelalamikiwa na wadau kuwa ni mrefu na unaongeza gharama kwa wadau wa uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 10 inapendekeza marekebisho katika fungu la 37 la Sheria ili kuweka ukomo wa muda wa kufanya chaguzi ndogo za Bunge kama ilivyobainishwa katika Ibara ya 76(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Toleo la mwaka 1977.

Vilevile Ibara ya 10 inarekebisha kifungu cha 37 ili kumpa mamlaka Mheshimiwa Spika kutangaza nafasi wazi za Wabunge zinazotokana na sababu nyingine zozote isipokuwa sababu inayotokana na Mbunge kuondolewa na Mahakama kwa mujibu wa kifungu cha 113 cha Sura ya 343 ya sheria za Tanzania. *(Makofi)*

Aidha, katika Ibara ya 11 inapendekezwa kufuta kifungu kidogo cha (3) cha fungu la 47 kinachompa mamlaka msimamizi wa uchaguzi kupanga siku nyingine ya kupiga kura badala ya siku iliyopangwa na Tume kwa msingi wa manufaa ya umma.

Mheshimiwa Spika, kutoa mamlaka kwa msimamizi wa uchaguzi ya kupanga siku nyingine ya kupiga kura nje ya ratiba iliyotolewa na Tume kunaweza kusababisha zoezi la Uchaguzi Mkuu kutokamilika kwa wakati. Ibara ya 12 inapendekeza kufuta kifungu kidogo cha (4) cha fungu la 50 ambacho kimetajwa katika fungu la 37. Inapendekezwa pia katika Ibara ya 13 kufanya mabadiliko katika fungu la 63 la Sheria ili kuruhusu waratibu wa Mikoa na Maafisa wa Tume ya Uchaguzi kuingia katika vituo vya kupigia kura kwa lengo la kuimarisha usimamizi katika vituo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 14 inakusudia kufanya marekebisho katika Sura ya “V” ya sheria kwa kuongeza sehemu mpya ya “III” inayohusu mchakato na mamlaka ya Tume kuwatangaza Wabunge Wanawake wa Viti Maalum walioteuliwa na vyama vyao kuwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ibara za 15 na 18 zinapendekeza kufutwa kwa mafungu ya 87, 97, 98 na 109 ya Sheria ya Uchaguzi yanayoruhusu utoaji wa takrima.

Ibara za 19, 20 na 21 zinapendekeza marekebisho katika mafungu ya 113, 114 na 115 ya Sheria ili kutoa nafasi ya kukata Rufaa katika Mahakama ya Rufani dhidi ya maamuzi ya Mahakama Kuu kwenye kesi za uchaguzi. Pia inapendekezwa kuweka ukomo wa muda wa Mahakama ya Rufani kusikiliza rufaa za uchaguzi ambapo inapendekezwa kuwa kipindi kisichozidi miezi 12. Aidha, inapendekezwa pia kuongeza muda wa kufungua kesi za uchaguzi kuwa siku 30 badala ya siku 14 ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, Muswada unapendekeza vilevile katika Ibara ya 22 kuongezwa fungu jipya la 124A linaloipa mamlaka Tume kwa kushirikiana na wadau wakuu ambao ni Serikali na vyama vya siasa kutayarisha maadili ya uchaguzi na kuyafanya yatekelezwe kisheria. Kwa sasa tunafahamu kwamba Tume imekuwa ikitayarisha maadili ya uchaguzi ambayo yamekuwa yakijadiliwa na kusainiwa kwa hiari na vyama vya siasa, Tume na Serikali. Utaratibu huu umesababisha maadili hayo kukiukwa mara nyingi hasa na vyama vya siasa kwa kuwa hayana msingi na nguvu ya kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu ya Muswada huu inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Sura ya 292 kama ifuatavyo; katika Ibara ya 24, Muswada unapendekeza kuongeza tafsiri ya maneno mbalimbali katika Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Aidha, inapendekezwa kurekebisha tafsiri ya neno Uteuzi na neno Diwani ili kujumisha katika tafsiri ya Uteuzi, uteuzi wa Madiwani Wanawake wa Viti Maalum; na katika tafsiri ya Diwani, kujumuisha Diwani wa Kuteuliwa na Diwani wa Viti Maalum vya Wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 25 inapendekeza mabadiliko katika fungu la 13 ili kumpa mamlaka Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa kutangaza rasmi kiti cha Udiwani kilichoachwa wazi baada ya kutaarifiwa na Mwenyekiti wa Halmashauri husika. Ibara hii inapendekeza zaidi mazingira yatakayosababisha kiti cha Udiwani kuwa wazi. Inapendekezwa kuwa uchaguzi wa kujaza viti vya Udiwani vilivyoachwa wazi ufanyike mara mbili kwa mwaka badala ya kufanyika ndani ya siku 90 kila kiti kinapoachwa wazi kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 26 inapendekeza marekebisho katika fungu la Sheria la kuruhusu wasimamizi wa uchaguzi na wasimamizi wa uchaguzi wasaidizi kuthibitisha matokeo ya kwenye maeneo yao badala ya kusubiri matokeo hayo kutangazwa na mamlaka ya uchaguzi. Utaratibu huu umekuwa ukisababisha ucheleweshaji usio wa lazima wa kutangaza matokeo ya kura za Madiwani katika kata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa lengo la kuongeza uwazi katika zoezi la uandikishaji wapiga kura, inapendekezwa katika Ibara ya 26 kuwa na fungu jipya la 15A katika Sheria linalotoa nafasi kwa vyama vya siasa kuteua Mawakala watakaokuwepo katika vituo vya kuandikisha wapiga kura wakati wa zoezi la uandikishaji kama ilivyo wakati wa upigaji kura.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 28 na 29 inapendekeza marekebisho katika mafungu ya 21 na 23 ya Sheria ili kuweka bayana kipindi cha kufanya uboreshaji wa Daftari la Taifa la Wapiga Kura kuwa mara mbili kati ya Uchaguzi Mkuu mmoja na unaofuata, vilevile kuruhusu uwepo wa Waandishi Wasaidizi na Watendaji wengine wanaoweza kuteuliwa na Tume kwa ajili ya kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 31 inapendekeza kufanya mabadiliko katika fungu la 63 la Sheria ili kuruhusu Waratibu wa Mikoa na Maafisa wa Mamlaka ya Uchaguzi kuingia katika vituo vya kupigia kura kwa lengo kuimarisha usimamizi katika vituo hivyo.

Ibara ya 32 inakusudia kufanya marekebisho kwa kuongeza sehemu mpya ya XIA inayohusu mchakato na Mamlaka ya Tume kuwatangaza Madiwani Wanawake wa Viti Maalumu walioteuliwa na vyama vyao kuwa Madiwani.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 34 inapendekeza marekebisho katika fungu la 114 la Sheria kwa lengo la kuweka muda wa kusikiliza na kutoa maamuzi kwenye kesi ya uchaguzi katika Mahakama ya Hakim Mkazi. Muda huo unapendekezwa kuwa sasa kuwa uwe ni mezi 18.

Muswada unapendekeza vilevile katika Ibara ya 35 kufuta na kuandika upya fungu 125 ili kuondoa mamlaka ya kutunga Kanuni za Uchaguzi kutoka kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa na kuipa Mamlaka ya Uchaguzi. Lengo hapa ni kuimarisha uhuru wa Mamlaka ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne ya Muswada huu inapendekeza marekebisho ya Sheria za Serikali za Mitaa ili kuziwezesha kwenda sambamba na Sheria za Uchaguzi. Aidha, yameongezwa marekebisho mengine yanayotokana na kuanzishwa kwa Sheria ya Gharama za Uchaguzi katika Jedwali la Marekebisho ili kuhuisha Sheria za Uchaguzi na Sheria mpya ya Gharama za Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya naomba kuwashukuru wote kwa kunisikiliza, na naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu na mtoa hoja hii ya Muswada wa Mabadiliko ya Sheria ya Uchaguzi. Sasa namuita Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala au mwakilishi wake.

MHE. PAUL J. LWANJI - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA: Mheshimiwa Spika, nami pia naomba niungane na wenzangu katika kutoa salaam za pole kwa Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Felister Bura, kwa kufiwa na mumewe.

Pia nichukue nafasi hii kuwapongeza wenzetu Wabunge wawili ambao wameapishwa leo baada ya kuteuliwa na Rais. *(Makofi)*

Baada ya kusema hivyo, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Uchaguzi *(The Electoral Laws (Miscellaneous Amendments) Bill 2009)*.

Mheshimiwa Spika, utangulizi kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nitoe maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya

Sheria Mbalimbali za Uchaguzi (*The Electoral Laws (Miscellaneous Amendments) Bill 2009*). (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuipelekea Kamati yangu kazi ya kushughulikia Muswada huu kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1), tarehe 20 Januari, 2010 Kamati ilikutana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, Mheshimiwa Philip Marmo, na wataalamu mbalimbali wa Serikali. Katika kikao hicho Kamati ilielezwa kuwa Muswada huu kwa ujumla wake unapendekeza kuleta marekebisho katika Sheria ya Uchaguzi, Sura 343 na Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Sura ya 292 ili kuondoa upungufu mbalimbali yaliyojitokeza katika chaguzi zilizopita kwa lengo la kuiwezesha Tume kuendesha chaguzi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, katika ufafanuzi wake wa kina Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, alieleza Kamati maeneo mbalimbali ambayo yamekusudiwa kurekebisha ambayo ni pamoja na Tume kutokuwa na madaraka ya kuwateua waratibu waandikishaji wa Mikoa, kipindi cha kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kutotajwa bayana katika Sheria na Sheria kutoruhusu baadhi ya Watendaji wa Tume kuingia katika vituo vya kupigia kura ili kufuatilia zoezi la upigaji kura.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 84 (2) ya Kanuni za Bunge za kudumu, Toleo la mwaka 2007. Ofisi ya Bunge ilitoa tangazo katika vyombo vya habari na mwaliko wa barua kwa wadau mbalimbali kuchangia mawazo yao juu ya Mswada huu. Wadau walioshiriki ambao Kamati ilipata fursa ya kuwasikiliza ni pamoja na Kituo cha Msaada wa Sheria (NOLA) na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (*Legal and Human Right Centre*). (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tarehe 21 Januari, 2010, Kamati ilikutana tena ili kupitia na kuchambua Muswada pamoja na maoni ya wadau. Maoni na ushauri wa Kamati baada ya kutafakari kwa kina maelezo ya Serikali na wadau, sasa naomba kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kamati nikianza na maoni ya ujumla.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo yoyote ya marekebisho ya sheria yanayolenga kuboresha na kuimarisha utawala bora yanapaswa kuungwa mkono. Aidha, marekebisho ya sheria yanayokusudia kuondoa dosari ambazo zimekuwa zikijitokeza katika chaguzi zilizopita ni jambo la msingi katika kuinua demokrasia hapa nchini. Kwa kuzingatia hayo, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali katika Muswada huu kama ilivyoelezwa na mtoa hoja. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu ambao umezingatia mambo mengi muhimu katika kuboresha chaguzi zijazo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda nijielekeze katika Ibara mahususi za Muswada. Katika Ibara ya 6(5) kulikuwa na mtazamo kuwa neno *immediately* lilivyotumiwa katika Muswada, libadilishwe kwa kuwa uboreshaji wa daftari la kudumu ukianza mara baada ya Uchaguzi Mkuu hakutakuwa na idadi ya kutosha ya wapiga kura wa kujiandisha. Kamati ililijadili suala hilo na kuafiki ili kutoa nafasi ya kupata idadi ya wapiga kura wakutosha. (Makofi)

Aidha, katika Ibara ya 21 ambayo inapendekeza kuongezwa Kifungu cha 124A 1(a) katika Sheria ya Uchaguzi, Sura ya 343, Kamati inashauri kuwa neno *of liondolewe* katika sentensi inayosomeka *"Ethical conducts for of political parties and the Government,"* ili kuleta maana yenye kueleweka zaidi.

Mheshimiwa Spika, mbali na maoni kuhusu matumizi ya lugha na sarufi, Kamati pia ilitoa maoni kutaka ufafanuzi kuhusu Ibara ya 16 ambayo wadau walipendekeza kuwa adhabu na faini kwa hongo na rushwa ni ndogo vikilinganishwa na makosa yenyewe. Serikali ilitoa ufafanuzi kuwa Ibara hii haihusiani na makosa ya hongo wala rushwa bali ni makosa ya kuchana mabango na machapisho, ufafanuzi ambao ulikubaliwa na Kamati yangu. *(Makofi)*

Vilevile, katika Ibara ya 33(3) ya Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Namba 4 ya mwaka 1979, inayoelezea muda uliowekwa kusikiliza kesi za Udiwani ambao ni miezi 18, Kamati ilijadili Ibara hii kwa kina na inashauri kuwa kwa mazingira ya Halmashauri zetu muda wa miezi 12 ndio muda unaofaa kwa Mahakama kusikiliza kesi za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia vipengele mbalimbali vilivyotolewa na wadau ili kuuboresha Muswada huu, Kamati ilishauri kuwa ni vyema Sheria za Uchaguzi zikasimamiwa vizuri zaidi bila kujali itikadi za kisiasa kwa lengo la kuimarisha demokrasia nchini. Pamoja na hayo, Kamati inashauri kuwa Maadili ya Uchaguzi kama yanavyoelezwa katika Ibara ya 21 ya Muswada ni vyema yapewe nguvu kisheria ili kusaidia utekelezaji wake. Zaidi ya hayo inasisitiza kuwa kwa wale watakaokiuka maadili ya uchaguzi wawajibishwe kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Aidha, Kamati inasisitiza kuwa suala la takrima wakati wa kampeni za uchaguzi ni vyema likatokomezwa ili kuleta ushindani wenye tija kwa lengo la kuwapata viongozi bora wenye kuleta maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuwa suala hili linahitaji uelewa wa kina kwa lengo la kuinua demokrasia katika uchaguzi, Kamati inashauri kuwa Tume ya Uchaguzi itoe elimu ya kutosha itakayosaidia kupata wapigakura wa kutosha na hatimaye viongozi bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hitimisho, kabla ya kuhitimisha maoni ya Kamati, naomba tena nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Philip Marmo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge na wataalamu wake kwa ushirikiano na ufafanuzi waliutoa kwenye vikao vya Kamati na kufanikisha Muswada huu. Vilevile nawashukuru wadau kutoka NOLA na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kwa michango yao mizuri iliyoisadia Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia niwashukuru na kuwapongeza Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kwa michango yao ya kina iliyowezesha kuboresha Muswada huu. Naomba kuwatambua kama ifuatavyo, Mheshimiwa George Lubeleje, Mwenyekiti, Mheshimiwa Ramadhani Maneno, Makamu Mwenyekiti na wajumbe ambao ni Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mheshimiwa Rajab Hamad Juma, Mheshimiwa Riziki Omar

Juma, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary na mimi pia Mheshimiwa John Lwanji.

Wengine ni Mheshimiwa Fatma Maghimbi, Mheshimiwa Yusuf Makamba, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Salim Yussuf Mohamed, Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mheshimiwa Abbas Mtemvu na Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru. *(Makofi)*

Aidha, napenda pia kuwashukuru Watumishi wa Ofisi ya Bunge, bila kuwasahau Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Elihaika Mtui na Ndugu Athuman Hussein, chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Dr. Thomas Kashililah, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha zinakamilika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa John Lwanji, mwakilishi wa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kusoma kwa ufasa kabisa taarifa ya Kamati ambayo itafuatiwa sasa na hotuba ya mwakilishi au Mwenyekiti kutoka Kambi ya Upinzani kuhusu masuala ya Katiba na Sheria. Naona ni Mheshimiwa Halima Mdee, karibu.

MHE. HALIMA J. MDEE - MSEMAJI MKUU WA KAMBI LA UPINZANI, WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, mimi ni Waziri Kivuli sio Mwenyekiti. Kwanza na mimi nichukue fursa hii kutoa pole kwa familia ya Mheshimiwa Bura kwa msiba mkubwa walioupata kwa kupoteza mume pamoja na baba.

Vilevile nitoe pongezi kwa hawa Waheshimiwa Wabunge wawili ambao wamejiunga nasi leo asubuhi, nina amini huu ndiyo utakuwa mwanzo wa miaka mitano inayokuja kwa sababu kwa miezi nane ni mingi lakini ni michache sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa nikiwa mzima wa afya ili kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani juu ya Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali za Uchaguzi, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 86(6) toleo la mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoainishwa katika madhumuni na sababu ya Muswada. Muswada huu unakusudia kufanya marekebisho katika sheria mbalimbali za uchaguzi (*The Elections Act and the Local Government Elections Act*) ili kuondoa mapungufu mbalimbali ambayo yamejitokeza katika chaguzi mbalimbali kwa malengo ya kuiwezesha Tume kufanya kazi zake kiufanisi.

Mheshimiwa Spika, tukianza na Sheria ya Uchaguzi Mkuu (*The Elections Act*) pendekezo kubwa linalohusiana na utaratibu wa uteuzi wa Wabunge wa Viti Maalum. Kifungu cha 13 kinafanyia marekebisho Sura ya "V" ya Sheria ya Uchaguzi kwa kuingiza sehemu mpya (*Part III*) inayohusu uteuzi wa Wabunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwa umakini, hakuna kilicho kipya katika mapendekezo haya, kilichofanyika ni kuhamisha Ibara ya 78 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (*Chapter 2 of the Revised Edition of Laws of Tanzania*) na kuiweka katika sheria ya uchaguzi. Mtindo huo huo wa kunakili na kuhamisha umefanywa katika Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa ambapo kipengele kipya (*Part XI(A)*) kinachohusiana na uteuzi wa Madiwani wa Viti Maalum kinapendekezwa kuingizwa katika sheria husika ya Muswada huu, nacho kipo kwenye Katiba.

Mheshimiwa Spika, halikadhalika kifungu cha 15 kinachopendekeza kukifuta kipengele cha 100 cha Sheria ya Uchaguzi kinachohusiana na makosa ya uchaguzi kama vile hongo, kukirimu na ushawishi (*bribery, treating and undue influence*) kwa wajumbe na watumishi wa Tume ya Uchaguzi. Kipengele hiki kilichofutwa kinabadilishwa na kipengele kipya ambacho kinataja makosa mapya kama hongo, rushwa na ushawishi dhidi ya wajumbe na watumishi wa Tume ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, hapa kilichofanyika ni kuliondoa neno kukirimu (*treating*) lililokuwepo katika kipengele cha awali na kulibadilisha kwa neno rushwa (*corruption*).

Mheshimiwa Spika, suala kama hilo limejirudia tena katika kipengele cha 10 cha Muswada ambacho kinafanya kuingiza katika Sheria ya Uchaguzi Ibara ya 76(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano inayozuia chaguzi ndogo kufanyika ndani ya kipindi cha miezi kumi na mbili kabla ya kuvunjwa kwa Bunge. Halikadhalika kipengele cha 18 cha Muswada hakileti badiliko lolote zaidi ya kukigawa kifungu cha 113 cha Sheria ya Uchaguzi katika makundi mawili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kinachojionyesha hapa ni kwa Serikali kutokuwa na dhamira ya dhati ya kufanyia mabadiliko mfumo mzima wa uchaguzi ambao pia ulipendekezwa jana na Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, wakati ambapo Katiba na Sheria ya Uchaguzi imetoa mamlaka kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi kusimamia na kuratibu uchaguzi wa Rais, Ubunge na Udiwani. Uhalisia ni kwamba Tume husika imekuwa kama kiini macho tu! Kwa kuwa uhalisia unaonyesha kwamba ni watumishi wa serikali za mitaa (*local government machinery*) inayosimamia chaguzi zote za Tanzania.

Mheshimiwa Spika, wakiwa kama waajiriwa wa TAMISEMI wasimamizi hawa wanawajibika moja kwa moja kwa Serikali Kuu. Watumishi wa Halmashauri wanageuka kuwa Tume ya Uchaguzi kwa mujibu wa sheria chini ya kifungu namba saba cha Sheria ya Uchaguzi ambayo inatamka bayana kwamba Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya, Manispaa na Miji na kadhalika na watumishi wao wa ngazi za chini wanageuka kuwa wasimamizi wa uchaguzi wakati wa kipindi cha Uchaguzi Mkuu. Wao pia wanahusika katika zoezi zima la uandikishwaji wa wapiga kura kwa mujibu wa kifungu cha 8 cha Sheria ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya Uchaguzi haina mamlaka yoyote ya uteuzi wa maafisa hawa. Matokeo yake wengi wa maafisa hawa wamekuwa wakitekeleza kazi zao sio kwa matakwa ya Tume ya Uchaguzi bali kwa matakwa ya mwajiri wao. Haya yamekuwa yakitekelezwa tokea kipindi cha uandikishwaji wa daftari la kudumu la kupigia kura mpaka wakatio wa uchaguzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani kwa miaka kadhaa sasa imekuwa ikidai mabadiliko chanya ya sheria za uchaguzi yenye lengo la kuunda Tume huru ya uchaguzi itakayowaondoa kabisa watumishi wa Halmashauri katika nyanja zote za usimamizi wa uchaguzi. Ndio maana Machi 2008 viongozi wa vyama vya upinzani waliingia makubaliano na msajili wa vya siasa wakikubaliana kwama watendanji wa kata na vijiji wasiruhusiwe kuusimamia uchaguzi wa vijiji, mitaa na vitongoji ambao ulifanyika mwezi Oktoba 2009.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyotarajiwa, wakati kanuni za uchaguzi husika zilipoandaliwa, makubaliano ya viongozi wa vyama yalipuuzwa na maafisa husika waliendelea kuwa wasimamizi wa uchaguzi. Matokeo yake ni kuwa uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitingoji, katika maeneo mengi ulioendeshwa kwa ubabaishaji mkubwa pasipo kuzingatia sheria nataratibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Muswada unapendekeza kukifanyia mabadiliko kifungu 7(2) cha Sheria ya Uchaguzi ili kuipa Tume ya Uchaguzi mamlaka ya kuteua mtu kwa ofisi au kwa jina kutokana na watumishi wa umma kwa madhumuni ya kuendesha zoezi la uchaguzi. Kipengele 7(2) ambacho kimefanyiwa marekebisho kilikuwa kinaipa Tume mamlaka ya kuteua wasimamizi wa uchaguzi na wasimamizi wasaidizi kama itakavyoona inafaa. Kitu pekee kilichoongezwa ni uwezo wa tume kuchagua mtu kwa jina. Jambo la msingi na la muhimu ambalo limejitokeza kwenye maeneo yote ni kwamba watu wote wanaoteuliwa ni waajiriwa wa Serikali. Tume kama Tume bado haijapewa mamlaka ya kuwa na watumishi wake, ambao watawajibika kwa Tume na si kwa matakwa ya Wizara ama Idara yoyote ya Serikali ambayo uzoefu umeonyesha unawajibika kwa Serikali iliyo madarakani.

Mheshimiwa Spika, katika mwendelezo huo huo kipengele cha saba cha Muswada, kuna kifungu kipya cha 15A cha sheria ya uchaguzi kinachohusiana na haki ya vyama vya siasa kuwakilishwa na mawakala wakati wa uandikishwaji wa wapiga kura. Kwa kadri tunavyofahamu hili halijawahi kuwa tatizo tokea sheria ya uchaguzi ilipofanyiwa marekebisho mwaka 2004 iliyokuwa na malengo ya kuanzishwa daftari la kudumu la wapiga kura. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, halikadhalika Muswada unalenga kupunguza siku za kuteua mgombea Urais/Makamu wa Rais pindi akipoteza maisha wakati wa mchakato wa uchaguzi kutoka siku 21 mpaka siku 14 (*Clause 9*). Halikadhalika kuweka ukomo wa kesi za uchaguzi kumalizika ndani ya miaka miwili (katika ngazi ya kusikilizwa na ngazi ya rufaa), tofauti na ilivyo sasa hivi ambapo kuna ukomo wa miaka miwili katika hatua ya kusikilizwa, lakini hakuna ukomo katika hatua ya rufaa. Wakati huo huo Muswada unalenga kuongeza muda wa kukata rufaa mahakamani kutoka siku 14 mpaka siku 30. Japokuwa marekebisho haya ni mazuri, lakini haya mabadiliko bado hayajatatua matatizo ya msingi na mapungufu ya kisheria ambayo yamekuwa yakilalamikiwa kwa miaka mingi na wadau.

Mheshimiwa Spika, Muswada pia umeingiza kifungu kinachoitaka Tume ya Uchaguzi kuzitengeneza na kuzichapisha *electoral codes of conducts*, lengo likiwa ni kuhakikisha kwamba uchaguzi unakuwa huru na wa haki (*Clause 21*). *Electoral Codes of Conduct* zitaelezea namna vyama vya siasa, Serikali na vitakavyotakiwa kujiendesha wakati wa kampeni za uchaguzi. Yeyote atakayekiuka *codes of conducts* atapata adhabu kama ambavyo itakavyobainishwa na *codes of conducts* husika. Swali la msingi la kujiuliza ni kwa namna gani *codes of conduct*

zitawezesha kuufanya uchaguzi uendeshwe kwa uhuru na haki wakati mfumo mzima wa uchaguzi hauko huru? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa malengo ya mabadiliko ya sheria ni kuongeza ufanisi wa Tume ya Uchaguzi katika kuendesha zoezi la Uchaguzi Mkuu, Muswada huu ulitakiwa uangalie maeneo ya mbalimbali yaliyokuwa na mapungufu katika uchaguzi uliopita. Kinyume na matarajio na kama ilivyoainishwa na mapendekezo yaliyoletwa mbele ya Bunge lako Tukufu, Muswada huu hauna malengo ya kuboresha mfumo mzima wa uchaguzi ili uwe huru na haki.

Mheshimiwa Spika, kinachoonekana dhahiri hapa ni kwamba kuletwa kwa mabadiliko haya ni kama kiini macho kwa Watanzania na wafadhili ili ionekane kwamba Serikali imefanyia marekebisho sheria za uchaguzi, wakati ukweli unabaki kwamba kilichofanyika ni kuhamisha vifungu kutoka kwenye Katiba na kuvileta kwenye sheria mama ya uchaguzi kama vilivyo na kufanyia mabadiliko kiduchu baadhi ya vifungu ambavyo havikuwa na unyeti na wala haviathiri Tume ya Uchaguzi katika utendaji wake wa kila siku.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo, Kambi ya Upinzani inapendekeza kwamba mabadiliko haya ya Muswada yaboreshwe kwa kufuta vipengele vyote ambavyo vipo tayari kwenye sheria nyingine na ambayo hayabadilishi wala kuboresha chochote katika mfumo wa uchaguzi. Vipengele vifuatavyo havina upya wowote:-

(i) Kipengele cha 13 na 31 kinachohusiana na uteuzi wa Wabunge na Madiwani wa Viti Maalum;

(ii) Kipengele cha 14 na 15 kinachohusiana na makosa ya hongo, kukirimu na tafsiri ya neno kipindi cha kampeni;

(iii) Kipengele cha 10 na 18 kinachohusiana na masharti ya muda wa kuitishwa kwa uchaguzi mdogo;

(iv) Kipengele cha 4 na 5 kinachohusiana na mamlaka ya Tume kuteua wasimamizi wa uchaguzi; na

(v) Kipengele cha 7 na 16 kinachohusiana na haki ya vyama vya siasa kuteua mawakala wakati wa kujiandikisha kupiga kura

Halikadhalika Kambi ya Upinzani, inapendekeza yafuatayo kufanyiwa marekebisho vipengele vya 7, 7A na 8 vya Sheria ya Uchaguzi na viingizwe vipengele vipya ambayo vitaipa Tume mamlaka ya kuteua maofisa na watumishi wao.

Pia utaratibu kama huu unatumika pia Ghana ambapo Ibara ya 52 na 53 ya Katiba ya nchi hiyo, toleo la mwaka 1992 inaipa mamlaka Tume ya Uchaguzi ya nchi hiyo kuteua maofisa wake na wafanyakazi wake.

Mheshimiwa Spika, halikadhalika Tume husika imepewa mamlaka ya kuwa na wawakilishi wake katika kila Mkoa na Wilaya. Kufuta Ibara ya 67(1)(b) ya Katiba ya Jamhuri

ya Muungano na Kifungu 39(2)(f) ya Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa inayokataza wagombea binafsi. Kama ilivyoelekezwa na uamuzi wa Mahakama Kuu na kama Mahakama Rufaa ilivyotilia mkazo hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kufuta kifungu cha 38(4) cha Sheria ya Uchaguzi ambacho kinamnyima sifa mgombea kushiriki kwa sababu tu hajatimiza masharti ya kipengele cha 38(3) linalo husiana na tamko la kisheria, masharti ya picha na taarifa za mgombea. Si sahihi kwa mgombea kukosa sifa za kugombea kwa kukosea tu kujaza fomu wakati ametimiza masharti yote ya Katiba. Kinachofanyija sasa, wasimamizi wengi wa uchaguzi badala ya kuwaelekeza wagombea kama kuna makosa katika ujazwaji fomu, wanakuwa chambo cha kutoa taarifa upande wa pili ili wawawekee wagombea wenza pingamizi. *(Makofi)*

Pia kufuta na kukibadilisha kifungu cha 111(2) cha Sheria ya Uchaguzi inayozuia kusikilizwa kwa kesi ya uchaguzi mpaka mlalamikaji alipe mahakamani kama dhamana, kiasi kisichozidi shilingi milioni tano kwa kila mlalamikiwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. Nashukuru. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana, nashukuru sana Mheshimiwa Halima Mdee kwa uwazi na uchambuzi mzuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninayo majina ya wachangiaji hapa ambao haitawezekana kabisa kupata nafasi kwa sababu muda umepita, wapo wachangiaji saba, mnafahamu kwamba bado tunao Muswada mwingine wa Baraza la Usalama la Taifa na tukichukua idadi hii, basi haitawezekana lengo la kukamilisha shughuli zetu. Kwa hiyo, bahati moja nzuri tu ni kwamba baadhi ya waliojaza kuongea hawamo humu, kwa hiyo wasikimbie sasa kuja, wabaki huko huko. Mheshimiwa Mtutura naona hayumo, Mheshimiwa Yono Kevela hayumo, yupo? Ah!

Mheshimiwa Dr. Mzeru nadhani hayumo, Mheshimiwa Suleiman Kumchaya hayumo, Mheshimiwa Juma Killimbah hayumo, kwa hiyo, wanaobaki ni watatu tu ambao ndiyo inafanana fanana na ninachohitaji. *(Makofi)*

Kwa hiyo, itakuwa Mheshimiwa Yono, Mheshimiwa Seleli, unajitoa? Aaha basi, safi sana. Kwa hiyo, nitakuwa na wachangiaji wawili tu. Mheshimiwa Yono Kevela na Mheshimiwa Mbunge mpya kabisa, Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu. *(Makofi)*

Nadhani ni vizuri nianze na huyu mpya huyu, ndiyo maana yake jasiri huyu, ameapishwa leo leo na anataka kusema. Karibu sana Mheshimiwa Ladhu. Mheshimiwa Kevela ujiandae. *(Makofi)*

MHE. ISMAIL JUSSA LADHU: Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nikushukuru kwa heshima hii kubwa uliyonipa kama ulivyosema umeniapisha leo na leo leo umenipa fursa ya kufanya mazoezi ya kazi hii ambayo nimepewa, ahsante sana. *(Makofi)*

Pili kabla ya kuchangia Muswada huu nilikuwa naomba pia nichukue fursa hii kumshukuru kwa dhati kabisa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, kwa heshima kubwa na imani yake kubwa aliyonipa kwa kunipa uteuzi huu.

Mheshimiwa Kikwete amefanya kitendo cha kihistoria katika Bunge hili na mimi naamini kwamba uteuzi huu ameufanya ili kuyatilia nguvu na kuonyesha kwamba maridhiano ya kisiasa Zanzibar ni ya Jamhuri nzima ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na vile vile naamini uteuzi huu umepeleka ujumbe kwa wale ambao bado wana mashaka kwamba waondoe mashaka, hakuna kurudi nyuma tena katika siasa zile za chuki, uhasama na mifarakano na badala yake tujenge siasa mpya za umoja, mashirikiano na kuenzi amani na utulivu katika nchi hii. Naomba pia niwapongeze viongozi wa chama changu, Chama cha Wananchi (*CUF*), chama mbadala nchini Tanzania wakiongozwa na Mwenyekiti wangu, Mheshimiwa Profesa Ibrahim Lipumba ambao naamini walifanikisha hatua zilizofanikisha uteuzi huu, nawashukuru wote ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na pia niwashukuru kwa kutumia fursa hii wale wote kwa mamia walioniletea ujumbe wa kunipongeza tangu lilipotoka tangazo, lilipotangazwa katika Bunge hili ambapo mimi kama wengine wote ilikuwa ni mara ya kwanza kulisikia, sikuwa na taarifa kabla. Kwa hiyo, wale wote ambao wameniletea *message* na kunipigia simu na hata kuniandikia taarifa za pongezi wote naomba kutumia fursa hii kuwashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nikija katika hoja hii au labda niseme kitu kimoja. Kuna mtu alinichokoza akasema unakwenda Bungeni bado miezi sita kabla Bunge kuvunjwa, sasa akasema ile hoja yako uliyokuwa umeitoa Zanzibar kule kwamba uchaguzi uhairishwe labda uipeleke Bungeni vilevile na akaniambia huko Wabunge wengi kuliko Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutokana na hali zao basi wataiunga mkono hoja kama hiyo, lakini sikusudi kuleta hoja kama hiyo. Niliitoa Zanzibar kwa mazingira yake maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafurahi kupata heshima ya kuwa mchangiaji wa mwanzo kwa suala hili na kutokana na uwanagenzi wangu nisingependa kuzungumzia mambo mengi sana, lakini kuna mambo ambayo nilikuwa naomba niyatolee mchango. *(Makofi)*

La kwanza kama alivyosema Msemaji wa Kambi ya Upinzani, naona kwamba sehemu kubwa ya mapendekezo haya yaliyoletwa na Serikali ni *cosmetic* yanazungumzia mambo ya juu juu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukisoma madhumuni na sababu, tunaambiwa kwamba malengo ya Muswada huu ni kufanya marekebisho kutokana na mapungufu yaliyotokana na chaguzi zilizopita hasa Uchaguzi Mkuu uliopita. Sasa kwa Serikali iliyo makini kungojea miaka minne halafu tuna miezi michache kabla ya Uchaguzi Mkuu ndiyo unaleta marekebisho ya sheria kutokana na mapungufu ya uchaguzi uliopita, hii haileti sura nzuri. Na zaidi ukiangalia haya maeneo ambayo kama alivyosema Msemaji wa Upinzani imependekewa kurekebishwa. *(Makofi)*

Mimi nilidhani pahali pazuri pa kujifunza mapungufu ya uchaguzi uliyopita ni katika ripoti ya waangalizi wa uchaguzi wa ndani na wa nje na ndiyo maana tunawaalika hawa.

Mheshimiwa Spika, na tunapokwenda kuziangalia ripoti hizi, kuna mapungufu mengi sana ambayo nilidhani kwa sababu ndiyo maana ya kuwaalika waangalizi yanakusudiwa

yatumike na tunapolalamika kuhusu uchaguzi uliopita, hasa sisi Vyama vya Upinzani huwa tunaambiwa haya yanakusudiwa kuboresha uchaguzi unaokuja, sasa tulidhani kwamba Muswada huu ungezingatia mambo hayo na wala hatuna haja ya kwenda pengine kwa ripoti nyingi za nje, ripoti ambazo mimi mara nyingi huwa nazipongeza sana ni ripoti za TEMKO, waangalizi wa humu humu ndani ya Tanzania, wanakuwa wanatoa maelezo mengi na kwa kina kabisa juu ya maeneo gani ambayo yanahitaji kurekebisha. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nilidhani kwamba kwa siku zijazo Serikali ingepaswa kuzi-consult hizi ripoti za waangalizi zisiwe tu kwamba zinaishia katika marafu ikawa kazi yetu sisi ni kualika tu kuonekana na sisi tuna uchaguzi uliokuwa wa wazi, lakini baadaye hatuzifanyi kazi. Utakuta labda nitoe mifano miwili tu, katika mambo ambayo yanalalamikiwa katika ripoti kama hizi. Moja ni suala zima la utendaji wa vyombo vya dola, hasa vikosi vya ulinzi na usalama wakati wa uchaguzi, hili hatukuliona limeguswa kabisa katika marekebisho haya ambayo yameletwa hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, na hili kidogo linanisikitisha kwamba tunashindwa hata kujifunza kutoka upande wa pili wa Jamhuri Zanzibar ni suala zima la *coverage* ya vyombo vya habari vya Serikali, yaani vinalipiwa na walipa kodi wote (*publicly owned media*) na kwa hapa zaidi tunakusudia *television* ya Taifa (TBC) na radio yake pamoja na magazeti ya Serikali ya *Daily News* na Habari Leo. Haya yanalipiwa kutokana na fedha za walipa kodi wote, na kipindi cha uchaguzi yalipaswa yatoe nafasi ya ulinganifu (*equitable*) kwa vyama vyote vinavyoshiriki katika uchaguzi na inasikitisha Zanzibar ambapo siku zote imekuwa na dosari mbaya katika uendeshaaji wa uchaguzi angalau kwa hili wakati wa uchaguzi unafanyika, vyama vya siasa vinapata nafasi sawa katika kila wiki katika kutangaza shughuli zake za kampeni. (Makofi)

Sasa kwa upande wa Jamhuri ya Muungano suala hili halijafanyika kwa hivyo ni mambo mengi ambayo hayajafanyika lakini naomba upande wa shauri unapaswa uwa-consult ili tunapoleta marekebisho ya uchaguzi tuonekana kweli tumeamua kuimarisha demokrasia na kujenga misingi imara zaidi ya utawala bora katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, la pili limezungumziwa pia katika sheria hii ni hili la *code of conduct* ni suala zuri na katika nchi nyingi za wenzetu linafanyika, lakini mimi ninaloliona tatizo kwa kwetu hapa ni *unforceability*, utekelezaji wa hizi *code of conduct*, kuna vifungu humu vya namna gani ya ku-enforce, lakini je, wakati ukifika wa utekelezaji vinazingatiwa? Hili nadhani pia ni suala ambalo Serikali inapaswa ijifunze. Hali hii ilitiwa dosari na Uchaguzi Mkuu uliopita, lakini mara nyingi huwa natoa mfano wa Kenya. Kenya tunazoea kuona Mawaziri kwa mfano wanapokiuka ile *adventure* au *incumbency* wakafanya kampeni kwa kutumia huduma za Kiserikali, Tume inawaita na tunaiona, sasa Bunge lako limeweka sifa moja chini ya uongozi wako kwamba linaweza kuibana Serikali, kwa hiyo, nadhani wakati umefika na vyombo hivi vinavyoambiwa vinatakiwa viwe huru kama Tume ya Uchaguzi, viwe na uwezo wa kuwabana hata watendaji na viongozi wa Serikali wanapokiuka mambo ambayo yanaathiri uchaguzi huru na wa haki. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ni hili linalohusu mgombea binafsi, lakini ningeomba atakapokuja Mheshimiwa Waziri atusaidie kidogo. Kulikuwa na kesi maarufu ya Mheshimiwa Mtikila, ikatolewa hukumu, Serikali haikuridhika, nadhani mara mbili katika Mahakama Kuu, imepelekwa Mahakama ya Rufaa, juzi kumetokea *error* nafikiri *technically* katika upande wa

Serikali na Jaji Mkuu akiongoza japo la Majaji wa Mahakama ya Rufaa alisema kwamba anaiambia Serikali iache mzaha kwamba ikiwa haitaendesha kesi hiyo wasichukulie kwamba hiyo ni *delincted*, lakini itasimama kama ilivyoamuliwa na Mahakama Kuu.

Sasa nimepata shida kidogo kwa sababu nadhani gazeti la juzi la *Daily News*, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali anasema kwamba maelezo ya Jaji Mkuu yalikuwa yanautatanishi na kwamba Mahakama itenganishe hilo, suala hili halitekelezeki. Sasa hii haileti taswira njema ya lile suala la kugawana madaraka katika mamlaka kuu tatu za dola.

Mheshimiwa Spika, kama tulivyokuwa na Bunge lenye meno na mahakama pia inapaswa iheshimiwe meno yake, sasa kama mahakama imesema kwamba ikiwa Serikali haikukamilisha taratibu, *the law of the land* itabakia kama ilivyoamuliwa na Mahakama Kuu basi Serikali inapaswa iweke utaratibu wa kutekeleza hilo na sio kusema kwamba suala hili haliwezi kutekelezeka, hiyo itakuwa Serikali inaingilia mkono wa pili wa dola ambayo ni mahakama. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini la mwisho kwa ruhusa yako, nilitaka kusema kwamba haya yote niliyoyazungumza ni muhimu kurebeshishwa kwa madhumuni ya kuwa na mfumo wa uchaguzi huru na wa haki ili tuiepushe nchi yetu na hii aibu ya kila wakati kutajwa tajwa katika anga za Kimataifa kwamba chaguzi zetu zina matatizo, lakini haya bado yatabakia kuwa ni kiini au dalili za maradhi yenyewe hatujayatibu, maradhi yenyewe yanahusu mfumo mzima unayoiweka Tume ya Uchaguzi ya Taifa na hili bahati mbaya halimo katika sheria tu, lakini limeanza katika Katiba yenyewe, sheria inatafsiri Katiba tu katika kifungu cha 74 cha Jamhuri ya Muungano, nilikuwa naomba nitoe pendekezo kwa heshima hii ya kuwa mtu wa mwanzo na kwa mara yangu ya kwanza kuzungumza katika Bunge hili kuiomba Serikali sasa ipunguze ule ukaidi wake na isikilize kilio cha upinzani na wanamageuzi nayo iwe kama hizi ripoti za anga za Kimataifa kwamba Tume ya Uchaguzi ifanyiwe marekebisha. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tuna mifano mingi sana, hatuzungumzi uteuzi lazima ufanywe na mtu fulani, unaweza kuendelea kufanywa na Rais, lakini pengine inafika wakati tunahitaji mfumo wa wawakilishi kwamba taasisi mbalimbali za kijamii, taasisi za kidini, jumuiya zisizo za kiraia zinawakaribisha kutoa maoni na mapendekezo yao ya watu na wanatoa maoni juu ya nani anafaa na ni wale tu *candidates* wanaopendekezwa na wao. (Makofi)

Baada ya kuwa wameridhiwa na vyama vyote vya siasa ambavyo ndiyo *players* katika uchaguzi, ahsante kwa kengele yako, wale ambao watapendekezwa na taasisi za kijamii pengine hata na siasa ikiwa na jumuiya za kidini, jumuiya zisizo za Kiserikali na wale ambao watapata alama ya kukubalika na wote kwamba hawa kweli ni watu waadilifu na watu ambao hawana mashaka ndani yake ndiyo ambao Rais atapaswa kuwateuwa katika Tume ya Uchaguzi. Nadhani tukifanya hivyo, kweli itakuwa kama tulivyosema awali kwamba tutakuwa tunalifikia lile lengo la kuweka mfumo wa utawala bora na chaguzi ambazo zitakuwa kweli na haki na kama inavyosema katika ya nchi kwamba sasa zitakuwa ndiyo msingi wa wananchi kutoa maamuzi na utashi wao wa nani hawaongoze katika nchi yao. Nakushukuru sana, ahsante sana. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ladhu, hata yule asiyekubaliana na mawazo yako itambidi akiri mambo mawili, kwanza unajieleza vizuri na pili Rais anajua kuteua, msemaji wa mwisho, Mheshimiwa Yono. *(Makofi)*

MHE. YONO S. KEVELA: Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi ya pekee kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kutoa kidogo mchango wa hii Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Uchaguzi *(Electoral Laws (Miscellaneous Amendments, 2009). (Makofi)*

Nadhani wenzetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala wamejitahidi sana kutoa marekebisho mazuri na kwa upande wa Serikali imeonekana kwa kweli ni sikivu, inapenda kurekebisha. Kabla sijaingia moja kwa moja kwenye mchango wangu, ningependa nitoe pongezi zangu za dhati kwa Wabunge wenzetu wapya waliochaguliwa; Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu, upande wa Upinzani na ndugu yetu Mheshimiwa Janet Zabedayo Mbena, upande wa CCM. Ninadhani Mheshimiwa Rais ameshakamilisha nafasi zake kumi. Ninampongeza sana. *(Makofi)*

Sasa nilikuwa ninasikiliza kwa makini upande wa Upinzani wametoa hoja nyingi nzuri, lakini nyingine kidogo zina kasoro kwa sababu kila wakati tunaweza tukawa tunailaumu Serikali, kwa kweli Serikali ni sikivu, inafanya kazi nzuri sana.

Kwa mfano, nitatoa kipengele kidogo upande wa Wakurugenzi wa Halmashauri za Miji na Wasaidizi wao; wanafanya kazi nzuri sana. Wanafanya kazi nzuri kwa sababu wanaposimamia wanafuata sheria, kanuni na taratibu. Sasa wenzangu wa Upinzani wanasema kwamba ooh! wanapendelea, wanafanya nini. Hata kama wangukuwa ni wao, sidhani kama wangufanya kazi nzuri kama wanavyofanya Watendaji wa Halmashauri. Kwa hiyo, ninawapongeza sana Wakurugenzi wa Halmashauri kwa kazi nzuri ambazo wanazisimamia vizuri upande wa uchaguzi.

Lingine, nilitaka nizungumzie kuhusu suala la utendaji wa Vyombo vya Dola; Polisi na Majeshi ya Ulinzi. Upande wa polisi nao wanajitahidi sana sana. Wale ni binadamu na kama kila kitu tutakuwa tunalaumu, hatutafika mahali pazuri, kwa sababu tunavyofahamu, sheria haiwaruhusu polisi waingie upande wa siasa, kwa maana ya kwamba, watetee Chama Tawala au Vyama vya Upinzani. Tunaona jinsi polisi wanavyojituma kwenye chaguzi mbalimbali, wanavyosimamia vizuri. *(Makofi)*

Kama dosari zinatokea ni ndogo za kibinadamu ambazo hata mtu mwingine anazifanya. Kwa hiyo, nilifikiri tuwape moyo tu kwamba, Vyombo vya Dola vinafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitaka nichangie upande wa vyombo vya habari. Kuna TBC, Chombo cha Serikali, halafu kuna magazeti ya watu binafsi. Ninadhani mchango wao kila mmoja anaufahamu. Hata vyombo vya Serikali kwa mfano, TBC na Magazeti ya Serikali, yanajitahidi ku-*balance story*. Waandishi waliopo pale ninadhani ni watu mahiri, wanajua miiko ya uandishi wa habari. Tukisema kila kitu tuwe tunailaumu Serikali, tutakuwa tunafanya makosa sana. Kwa hiyo, nilikuwa ninafikiria kwamba, hizi sheria zinapokuja, ziangalie udhaifu tunaotakiwa tuurekebishe kidogo na mazuri tuyaboreshe. Wengine wanasema watu wanadokoa

kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano inaletwa kwenye vifungu vya marekebisho. Mimi hilo ninaona kama ni nzuri kwa nini tusizifuata kama zilivyo. Kwa hiyo, nilifikiri kwamba, isiwe kila kitu tunailaumu Serikali, kuna mambo mazuri ambayo inatakiwa tushirikiane na wenzetu wa Upinzani turekebishe vizuri hizi sheria. Mimi binafsi Sheria ninazona ni nzuri sana. Sasa kwa vile wenzangu walianza kujitoa na mimi nilitaka nijitoe, lakini nikaona bora nichangie vitu vichache ambavyo ni vya msingi.

Suala la hongo, rushwa na ushawishi, hatuwezi kukataa kwamba havipo. Hivyo vitu vipo na hili suala ni la maadili. Inatakiwa sisi jamii tuangalie jinsi ya kubadilika, kwa sababu ni vitu ambavyo hata maadili ya dini zetu yanakataa. Hili halifuati chama fulani, sote tulipo hapa ni wakosaji. Leo nimekuja na Biblia hii, mimi ni Mkristo, ninaelewa sote ni wakosaji ingawa jana Mheshimiwa Makwetta aliuliza nani ambaye hajakosea wengine walisimama. Nilipokuwa ninaongea na Mheshimiwa Makwetta, alisema yeye alikuwa anataka awape *zero* wote. Kwa hiyo, niseme kwamba, mtu anayejisema ni msafi siyo kweli. Sote hapa kidogo tuna upungufu, lakini Mheshimiwa Makwetta anajitahidi sana, huwa ninaangalia kibanda chake ni kibovu kabisa. Kwa hiyo, kwa upande wa rushwa ninaweza nikamtetea Mheshimiwa Makwetta hana kabisa. *(Kicheko)*

La mwisho ni kwamba, kwa kuwa ni suala la maadali, ni vizuri Serikali ishirikiane vizuri na Taasisi za Kidini kukomesha matatizo ya hongo, rushwa na kuwa tofauti na maadili. Kwa sababu hata tukisema tuweke TAKUKURU nao ni binadamu, sijui tuweke nani, nao ni binadamu. Suala la msingi ni la maadili kwamba, tujitahidi kuangalia dini zetu zinasemaje; ukiwa ni Muislamu fuata miiko ya Uislamu, kama ni Mkristo fuata miiko ya Ukristo ili tufikie hatua ya kukomesha hili tatizo la rushwa na hongo na vitu mbalimbali. *(Makofi)*

Mwisho, niseme kwamba, mimi ninawapongeza TAKUKURU, pamoja na kwamba kuna watu wanalaumu, lakini wanajitahidi sana, ninaomba tuwape ushirikiano. Sheria tulizozitunga sisi wenyewe humu ndani ndiyo wenzetu wanazifanyia kazi, sasa zinapotugeukia tunaanza kulaumu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninawashukuru tena. Ahsanteni. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Yono Kevela. Sasa ninamwita mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge).

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):
Ahsante. Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninatoa shukrani za dhati kwa wote ambao wamechangia Muswada huu na wale ambao hawakutoa mchango wao. Kimya chao ni kwamba, wanaafiki mapendekezo ya Muswada; nao tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa ufafanuzi kwa hoja zote ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge kwa kusema na kwa maandishi, ninaomba katika ile orodha ya awali ya watu niliowashukuru kwa kusaidia kufanikisha Muswada huu nimwongeze Ndugu Kiravu, Mkurugenzi wa Uchaguzi, yeye pamoja na Watumishi wa Ofisi yake, walisaidia sana kufanikisha Muswada huu. Jana nilisahau kuwashukuru Wabunge kwa kupitisha ule Muswada

muhimu wa Matumizi ya Fedha Nyakati za Uchaguzi. Ninawashukuru sana na Ofisi ya Waziri Mkuu inatoa ahadi kwamba, tutatoa ushirikiano wa dhati sana ili tutekeleze masharti ya Muswada huo haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Ninaomba mnipe ruhusa ya kuwataja wale ambao walichangia Muswada huu. Waliochangia kwa kuzungumza ni Mheshimiwa John Lwanji, kwa niaba ya Kamati, Mheshimiwa Halima Mdee, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu na Mheshimiwa Yono Kevela. Waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Nuru Bafadhil na Mheshimiwa Stella Manyanya. Wote ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, kwa vile tulikuwa pamoja muda wote, tukiushughulikia Muswada huu, sisi upande wa Serikali na Kamati, zetu nyingi zilikuwa zimekwisha kwenye ngazi ya Kamati. Kwa hiyo, maoni yao mengi tumeyazingatia na wao wanafahamu hilo, ndiyo maana tumeleta Jedwali la Mabadiliko katika Muswada huu. Isipokuwa tu nisemee eneo moja ambalo limerejewa pia na wasemaji wengine waliofuatia hasa Msemaji wa Kambi ya Upinzani na pia Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu; hili ni eneo linalohusiana na maadili ya uchaguzi. Sasa kuwa na uzito wa kisheria, mnafahamu utaratibu wetu wa zamani ni kwamba, kabla ya Uchaguzi Mkuu, Vyama vyote vya Siasa vinavyoshiriki Uchaguzi Mkuu, kwa umoja wao wanakutanishwa na Mkurugenzi wa Uchaguzi, tukimshirikisha pia Msajili wa Vyama vya Siasa ili kuwekeana au kukubaliana maadili bora zaidi ya namna ya kuendesha uchaguzi.

Maadili haya yalikuwa ya hiari, lakini kwa bahati mbaya sana sote ni mashahidi, nyakati za uchaguzi ngazi za kampeni, maadili haya karibu yote yalikuwa yanakiukwa. Kama ni kuhujumiana tulikuwa tunahujumiana, kama ni kutoa lugha chafu, tulikuwa tunatoa lugha chafu, kama ni kutokusema ukweli, tulikuwa hatusemi ukweli na hii imethibitishwa katika uchaguzi za mwaka wa 2000 na mwaka wa 2005 na ndiyo maana tumeamua kanuni hizi sasa ziwe na uzito wa kisheria.

Nilimsahau Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, naye amechangia kwa maandishi kwenye Muswada huu. Kwa hiyo, kitakachotokea ni kwamba, wakati wa kuandaa Kanuni hizi, tutarudia tena katika utaratibu wa zamani wa kuwaita wadau mbalimbali, hasa Vyama vya Siasa ili kurejea zile kanuni ambazo tulikuwa tunazitumia kama kanuni za hiari na baadaye wakiafikiana, Waziri atazitangaza kwenye Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Martha Umbulla ametoa maoni mazito kama matano. Kwanza, anataka Sheria ya Uchaguzi iweke bayana mipaka ya utendaji wa Wabunge wa Viti Maalum, kwa kuwa kuna mgongano kati ya Wabunge hao na wale wa Majimbo. Pili, anasema Sheria ya Uchaguzi irekebishwe ili kuweka wazi mahusiano ya Wabunge watatu katika Wilaya moja yenye Wabunge wa Viti Maalum wawili na mmoja wa Jimbo.

Pia Mheshimiwa Martha Umbulla anataka Wabunge wa Viti Maalum wanapofanya shughuli za maendeleo katika Majimbo huwa wanapata vikwazo kwa Wabunge wa Majimbo. Hivyo na wao wapewe nafasi ya kuleta maendeleo katika jamii. Sheria iweke bayana ushiriki wa Wabunge wa Viti Maalum katika Halmashauri, kwa mfano, hawa hawatambuliwi na kuwekwa katika Kamati za Fedha.

Maelezo yetu ni kwamba, kwa mujibu wa Katiba ya Nchi na Sheria za Uchaguzi, Wabunge wote ni sawa. Wabunge wote ni sawa na hakuna sababu ya Wabunge wa Viti Maalum kubaguliwa katika utendaji wao wa kazi hapa Bungeni au katika maeneo yao ya kazi. Sheria ya Uchaguzi haishughulikii mahusiano kati ya Wabunge na ni wajibu wa kila Mbunge kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria. Serikali haioni kuwa ni kwa nini tunakuwa na migongano kati ya Wabunge wa aina mbili au wa aina tatu katika Jimbo moja.

Wabunge wa Viti Maalum wana haki sawa na Wabunge wa Majimbo katika kuleta maendeleo katika jamii ya Watanzania. Serikali itashirikiana na Waziri wa TAMISEMI ili kuhakikisha kwamba, Wabunge wa Viti Maalum wanashirikishwa kikamilifu katika ngazi zote za Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi sana, sasa ninaomba nitoe maelezo kuhusu maoni; kwanza, yaliyotolewa na Mheshimiwa Halima Mdee, Msemaji wa Upinzani katika masuala ya Sera, Uratibu na Bunge. Yeye anataka mfumo mzima wa uchaguzi ubadilishwe hasa katika maeneo ya utumishi katika Tume. Pendekezo hili katika mazingira yetu ni gumu kulitekeleza kwa sababu Tume yetu haina watumishi mpaka ngazi ya chini na kama itaajiri watumishi hawa wa ngazi ya chini itakuwa wa muda tu, kwa sababu baada ya uchaguzi hawatakuwa na majukumu yoyote.

Pili, watumishi wa umma huwa tunawaamini zaidi kwa sababu kwanza tunawafahamu, lakini pia tunajua majukumu yao kwa Serikali, kwa mwajiri wao, kuliko mtu ambaye unamwajiri kwa muda baadaye akifanya makosa huwezi kumtafuta au kumwajibisha. Kwa hiyo, kwa sasa hali halisi inatulazimisha tuwatumie Watumishi wa Umma kuliko watumishi wa muda katika ngazi za Wilaya na Kata.

Muundo wa Tume; hili limeelezwa vizuri sana na Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu. Niseme tu kwamba, hoja hii imejitokeza mara nyingi; ni hoja nzito na siyo hoja ya kuipuuza hata kidogo. Isipokuwa hoja hii inagusa Katiba na sisi sote tunafahamu mchakato wa namna ya kubadilisha Katiba. Kwa hiyo, pendekezo na ombi langu kwa Wabunge wote na wadau wote ni kwamba, kwa vile muda uliobaki kati ya leo na Uchaguzi Mkuu siyo mrefu, ni muda mdogo sana uliobaki na haitawezekana mchakato huu kukamilika, basi jambo hili lishughulikiwe baada ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2010 kwa utaratibu wa kawaida wa mchakato wa kubadilisha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Niseme tu kwa sasa Tume tulionayo ni nzuri, Viongozi wake ni Watumishi wa Umma, waadilifu sana na muda wote wamejaribu kutenda haki kwa uwezo wao wote. Kama kuna upungufu umetokea kwa kweli ni wa kibinadamu. Kwa hiyo, tusiwalaumu sana kwa majina yao na kwa vile wako pale kwa mujibu wa Sheria na Katiba ya sasa, tunaomba sana, siyo tu tuwaheshimu, lakini tuwape ushirikiano wa karibu na wa dhati kabisa. Kanuni za Maadili nimeelezea, siyo kweli kwamba mabadiliko yanayoletwa hapa ni kiini macho tu. Vipengele vingi hapa vinajaribu kuweka wazi zaidi hasa sehemu ile ya Wabunge wa Viti Maalum na Madiwani wa Viti Maalum. Mnafahamu wote wanavyolalamika katika utendaji wao wa kazi, lakini pia namna ya kuwapata.

Tunajaribu kwenda kwa ndani kidogo, lakini ninashindwa kwa sababu hatimaye tunajikuta kwamba, hawa wanateuliwa na vyama kutokana na idadi ya kura zilizopatikana wakati wa Uchaguzi Mkuu na mchakato wa ndani ya vyama uko nje ya uwezo wetu. Kwa hiyo, tunachokifanya ni kwamba, angalau tufikie hapa japokuwa hatutakuwa na uwezo kufikia kule ambapo huwa wanapatikana.

Mheshimiwa Spika, suala la mgombea binafsi siyo dogo. Kuna mabishano ya kisheria, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ndiye Mshauri Mkuu wa Serikali katika masuala sheria. Hali ilivyo sasa, mimi niseme kwa mara nyingine kwamba, siyo rahisi sana kwa Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu kumhusisha mgombea binafsi. Pale fursa itakapotokea, tutafuata utaratibu wa kawaida kwenda kwa Watanzania ili tubadilishe Katiba, kama Watanzania wengi watapenda tuwe na mgombea binafsi basi Serikali haitasita kufuata maagizo ya wananchi kwa mchakato wa kawaida wa kubadilisha sheria zetu.

Mheshimiwa Spika, tulimsikiliza kwa makini sana Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu, ambaye leo tu ndiyo ameapishwa na ametoa hotuba yake ya kwanza Bungeni. Mheshimiwa Ladhu, hii inaitwa *maiden speech*. Hotuba yake kwa kweli ni nzuri sana, ni ishara ya umahiri wake katika siasa. Anajenga hoja nzuri tu na kutetea hoja hizo tena kwa hisia nzito sana na huu kama ndiyo mwanzo, basi tutegemee mazuri zaidi huko tunakokwenda katika Bunge letu, japokuwa tumebakiwa na mikutano miwili tu. Bila shaka mamlaka iliyowateua itawateuwa tena au watumie madirisha au milango ambayo inafunguliwa na Muswada huu leo. Mimi ninamtakia Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu kila la kheri na mafanikio tele katika mapambano haya ya siasa na pia katika ujenzi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Yono Kevela, kwa ujumla ameunga mkono Muswada na tunazingatia maoni yake yote; tunamshukuru sana.

Mheshimiwa Nuru Bafadhil, yeye anataka tusiwahusishe sana walimu katika mchakato wa uchaguzi wetu. Ninataka kusema kwamba, walimu ni watumishi wa umma kama watumishi wengine. Kama kuna watumishi wachache au kuna walimu wachache wanakiuka maadili, tusichukulie kwamba wote ndivyo walivyo. Tukumbuke kwamba, watumishi ambao tunawapata kwa urahisi kwenye ngazi za chini ni walimu. Tume itajitahidi kuwachanganya walimu na watumishi wengine wakati wa kusimamia uchaguzi, lakini hali halisi itatufanya tusiwakwepe walimu kwa vile ndiyo wako wengi na wameenea mpaka ngazi ya chini kabisa ya vijiji vyetu katika nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine, ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia Muswada huu kwa kuongea na kwa kuandika, lakini pia kwa kukaa kimya kwa kuunga mkono. Kwa hiyo, ninadhani haitachukua muda kuupitia haraka haraka tutakapofika kwenye ngazi ya Bunge kama Kamati ya Bunge Zima.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa mara nyingine ninakushukuru tena na ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi. Waheshimiwa Wabunge, hoja ya kupitisha Muswada huo imekwishatolewa na kuungwa mkono na tutaiaamua baadaye baada ya kupitia utaratibu uliopo Kikanuni.

KAMATI YA BUNGE ZIMA

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Uchaguzi wa Mwaka 2009 (*The Electoral Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2009*)

Ibara ya 1

Ibara ya 2

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 3

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 4

Ibara ya 5

Ibara ya 6

Ibara ya 7

Ibara ya 8

Ibara ya 9

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 10

Ibara ya 11

Ibara ya 12

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 13

MHE. BERNADETA K. MUSHASHU: Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Katika mchango wangu wa maandishi na baadhi ya Wabunge waliochangia katika kipengele hiki, tulizungumzia juu ya Wabunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa mtoa hoja amesema namna ya

kumpata ni mchakato ndani ya vyama vya siasa. Kwa hiyo, Sheria hii haiwezi kuingia kwa ndani katika mchakato wa ndani ya vyama.

Nilikuwa ninauliza je, baada ya kuwa hawa Wabunge wa Viti Maalum wameshateuliwa na wameshatangazwa na Tume ya Uchaguzi; kwa nini sasa Sheria hii isibainishe wazi kwamba sasa huyu Mbunge wa Viti Maalum eneo lake la kufanyia kazi ni wapi kusudi tuache mgongano uliopo kati ya Wabunge wa Viti Maalum na wa Majimbo, maana ukienda kila Jimbo huyu anaona unamwingilia; lakini kama ingekuwa imeelezwa wazi kwamba, Mbunge wa Viti Maalum labda ni Mkoa, Taifa au ni Wilaya mbili, basi hata unapokwenda pale inaeleweka wazi kwamba ni eneo linalotambuliwa kisheria ambalo umepangiwa.

Je, Mheshimiwa Waziri hawezi kusaidia kwa kuhakikisha kwamba hicho kipengele kinaingia kwenye Sheria hii?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):
Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namshukuru sana Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, kwa kuleta suala hili. Kwa sababu jambo hili lina historia; zamani Viti Maalum ilikuwa ina sura ya Kitaifa, ukiwa Mbunge wa Viti Maalum unakuwa Mbunge wa Taifa. Hii historia imeendelea kuwepo na kwa vyama vingine inaonekana ni kama inakuwa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyofahamu ni kwamba, mazoea saa nyingine inakuwa sheria. Kwa vyama vidogo vidogo tulivyonavyo, Wabunge wa Viti Maalum kwa hakika ni Wabunge wa Taifa, isipokuwa chama kikubwa kama Chama cha Mapinduzi, kwa ajili ya wingi wao na wanapatikana kutoka Mikoani, huwa wanabaki na wanafanya kazi katika Mkoa waliyotoka. Kwa hakika walistahili wawe Wabunge wa Taifa, kwa maana halisi ya Viti Maalum. Pia hii haina maana kwamba, kuna sheria inayokatiza Wabunge hawa wafanye kazi zao katika maeneo ambayo wanaona ndiko walikopata dhamana yao hii ya kuja hapa. Kwa hiyo, kama wanaona wajikite kwenye eneo moja la Mkoa, basi wafanye hivyo. Kama wanaona wajikite kwenye Wilaya moja wafanye hivyo, kama wanataka kujikita kwenye Mkoa mzima au nchi nzima sheria haikatizi.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 14
Ibara ya 15
Ibara ya 16

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 17

*(Ibara iliyotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 18
Ibara ya 19
Ibara ya 20
Ibara ya 21
Ibara ya 22
Ibara ya 23
Ibara ya 24

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 25

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 26
Ibara ya 27

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 28

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 29
Ibara ya 30

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 31

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 32
Ibara ya 33
Ibara ya 34
Ibara ya 35
Ibara ya 36

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 37

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)
(Bunge lilirudia)*

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Uchaguzi wa Mwaka 2009 (*The Electoral Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2009*)

(Kusomwa Mara ya Tatu)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):
Mheshimiwa Spika, ninafurahi kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya kurekebisha Sheria Mbalimbali za Uchaguzi, ibara kwa ibara, imeukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Ninaomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria za Uchaguzi uitwao *The Electoral Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2009* pamoja na marekebisho yake sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya
Tatu na Kupitishwa)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni zetu, Muswada sasa umesomwa kwa mara ya tatu na hivyo sasa umepitishwa kuwa Sheria ya Nchi yetu, utasubiri tu hatua ya mwisho ambayo ni kupata ridhaa ya Mheshimiwa Rais. Ninawashukuru sana kwa kazi hii mliyoifanya. Ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Kabla hatujaendelea na shughuli inayofuata, ninalo tangazo hapa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu *CDCF*. Linasema hivi; Kanuni zimeshachapishwa na kupewa *Title ya CDCF Regulations, GN No. 30, 2010*, Tarehe 05 Februari, 2010. Nakala moja ya Kanuni tayari imekwishawasilishwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango ili kuandaa utaratibu wa kuzigawa fedha na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu

(TAMISEMI), ameagizwa asimamie zoezi la kutoa mchanganuo wa fedha za CDCF kwa haraka kadiri inavyowezekana. *(Makofi)*

Niliona mjue hilo kwa sababu imebaki miezi michache, basi tutazamie hii neema. Ninadhani kwa tafsiri hii ni kwamba, fedha za robo mwaka zote nne itamwagwa katika kipindi hicho. *(Makofi)*

Muswada wa Sheria ya Baraza la Usalama la Taifa wa Mwaka 2009
(The National Security Council Bill, 2009)

(Kusomwa Mara ya Pili)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA): Mheshimiwa Spika, nami ninaomba niungane na wenzangu katika kutoa pole kwa msiba uliotokea kwa Mheshimiwa Felister Bura na familia yake. Tunamwomba Mwenyezi Mungu, aiweke roho ya marehemu mume wa Mheshimiwa Felister Bura, Peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, vilevile na mimi ningependa niwapongeze wenzetu ambao wameapishwa leo ; Mheshimiwa Janet Mbene, ambaye na mimi pia ni Mwenyekiti wangu wa Serikali za Mitaa kule Masaki; hongera sana. Pia ninampongeze Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu.

Mheshimiwa Spika, tarehe 30 Januari, 2010 niliwasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya Baraza la Usalama la Taifa wa Mwaka 2009 ili usomwe kwa mara ya pili. Baada ya kupokea michango na hoja mbalimbali za msingi zilizotolewa na Kamati, Kambi ya Upinzani na Waheshimiwa Wabunge, niliomba kuuondoa Muswada na kuurejesha katika Kamati kwa kutumia Kanuni ya 87(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoahidi Bungeni wakati ninaomba kuuondoa Muswada, Muswada huu ulirudishwa katika Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, ambayo kwa kushirikiana na Kamati ya katiba, Sheria na Utawala, walipata fursa ya kuupitia upya Muswada na kutoa maoni yao ambayo ndiyo msingi wa Muswada huu kurudishwa Bungeni leo. Kwa kuzingatia haya, ninaomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya Baraza la Usalama la Taifa wa Mwaka 2009 *(The National Security Council Bill, 2009)*, sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, ninatoa shukrani zangu za dhiti kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa kuuchambua Muswada huu kwa kina na kutoa maoni yake ambayo yamesaidia sana katika kuuboresha Muswada huu na ninapenda kuwahakikishia kwamba, maoni na michango yao imezingatiwa kwa makini sana. Pia ninapenda kuwashukuru kwa dhiti wadau mbalimbali kwa michango yao ambayo pia imezingatiwa. Aidha, ninaishukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushauri na ushirikiano wao wa hali ya juu katika kuuandaa Muswada huu na hatimaye kufikia hatua ya kusomwa kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kueleza yale yaliyo katika Muswada huu, ninaomba kutoa historia fupi kuhusiana na mapendekezo ya uanzishwaji wa Baraza la Usalama la Taifa. Baraza la Usalama la Taifa si dhana mpya, ni chombo ambacho tayari kipo na kimekuwa kikifanya kazi. Baraza lipo lakini halipo kisheria. Baraza hili liliundwa rasmi tarehe 15 Mei, 1992 kuchukua nafasi ya iliyokuwa Tume ya Ulinzi na Usalama ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama cha Mapinduzi. Chombo hiki kimepitia hatua mbalimbali kama ifuatavyo; kwanza, Tume ya Ulinzi na Usalama. Baraza hili lilianzishwa kama Tume ya Ulinzi na Usalama, dhana hii ilibuniwa na Chama cha TANU na kutolewa katika Mwongozo wa TANU wa Mwaka 1971 na kuendelea katika Mwongozo wa Chama cha Mapinduzi, CCM wa mwaka 1981.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Ulinzi na Usalama iliundwa kufuatia Katiba ya CCM ya mwaka 1982, ikiwa ni Chombo cha kuhudumia Halmashauri Kuu ya CCM. Kazi yake kubwa ilikuwa ni kuishauri Kamati Kuu ya CCM kuhusu utekelezaji wa siasa ya Chama kuhusu ulinzi na usalama. Tume ya Ulinzi na Usalama ililiwezesha Taifa kuwa na mahusiano yanayotakiwa kati ya uongozi wa dola wa kiraiya, pamoja na vyombo vya ulinzi na usalama, *Harmonius Civil Military Relations*. Hiki kilikuwa ni chombo cha chama na hivyo kilitegemea sana mfumo wa chama.

Mheshimiwa Spika, pili; Baraza la Usalama la Taifa. Kutokana na mabadiliko ya kisiasa na kikatiba ya mwaka 1992, ambayo yalikuwa ni mabadiliko makubwa, mazito na ya msingi, moja ya mambo muhimu katika mabadiliko hayo ilikuwa ni kutenganisha shughuli za chama na zile za Serikali. Kutokana na umuhimu huo, Halmashauri Kuu ya Chama Tawala (CCM), iliagiza mabadiliko yafanyike; hivyo Baraza la Usalama la Taifa liliundwa likiwa ni chombo cha Serikali cha kumshauri Rais kuhusu masuala yote ya ulinzi na usalama wa Taifa. Chombo hiki kilichukua nafasi ya Tume ya Ulinzi na Usalama. Hata hivyo, kulijitokeza upungufu ndani ya Baraza la Usalama la Taifa kama ifuatavyo:-

(i) Pamoja na mabadiliko yaliyofanyika, sura ya utendaji kazi wa Baraza la Usalama imeendelea kuwa kama ilivyokuwa wakati wa Tume ya Ulinzi na Usalama chini ya Chama kimoja.

(ii) Kutokana na Baraza la Usalama la Taifa kubadilishwa kuwa Chombo cha Kiserikali, idadi ya Wajumbe iliongezeka kutokana na Wajumbe wengine kuingia kwa nyadhifa zao.

(iii) Pamoja na Baraza la Usalama la Taifa kuendelea kufanya kazi yake lakini halijasimikwa kisheria.

Mheshimiwa Spika, Mwenyekiti wa Baraza la Usalama la Taifa kwa kipindi hicho, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, alibaini kuwepo kwa upungufu katika muundo na uwepo wa Baraza lenyewe. Miongoni mwa upungufu huo ni pamoja na ukubwa wa Baraza na baadhi ya Wajumbe kutajwa kwa majina; na Baraza halikuwa limeanzishwa kisheria. Kuendelea kuwepo kwake katika hali hiyo, kungeweza kutafsiriwa kuwa lipo kwa utashi wa Serikali iliyopo madarakani; hivyo, kutokidhi haja ya mfumo wa vyama vingi vya siasa nchini.

Mheshimiwa Spika, Mwenyekiti aliagiza Muundo wa Baraza utazamwe upya. Kufuatia maelekezo hayo, Serikali iliunda Kamati Maalum ya Kupendekeza Muundo Mpya wa Baraza la Usalama la Taifa. Kamati hii ilifanya kazi yake na kukabidhi taarifa Serikalini, juu ya mapendekezo ya muundo mpya wa Baraza la Usalama wa Taifa. Kutokana na mapendekezo hayo, mchakato wa kuanzishwa Baraza jipya kisheria ulianza.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Muswada ulioletwa Bungeni ukizingatia *schedule of amendments* ambayo imegawiwa leo, Wajumbe wa Baraza la Usalama la Taifa linalopendekezwa kuundwa ni kama ifuatavyo: Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Waziri Mkuu, Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Katibu Mkuu Kiongozi atakuwa Katibu wa Baraza la usalama la Taifa na Mwenyekiti wa Sekretarieti ya Baraza. Watu wengine kwa nyadhifa zao na uhitaji maalum wataitwa na Baraza kutoa ushauri wakati wowote kwa kadiri itakavyohitajika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unaunda Baraza lenye sura ya Jamhuri ya Muungano na pia unatambua uwepo wa Kamati ya Ulinzi na Usalama za Mikoa na Wilaya. Kamati hizi, hata hivyo, hazitakuwa sehemu ya Baraza lakini zitakuwa na uhusiano wa kikazi na Baraza.

Ninaomba nirudie hapo; hata hivyo, Kamati hizi hazitakuwa sehemu ya Baraza, lakini zitakuwa na uhusiano wa kikazi na Baraza. Jukumu kuu la Baraza la Usalama la Taifa ni kumshauri Rais kuhusu masuala ya Ulinzi na Usalama nchini. Inapendekezwa pia kuweka utaratibu wa utatibu wa taarifa za siri utakaowezesha watu binafsi, taasisi za umma na taasisi binafsi kushiriki kuchunguza mienendo ya wakazi wanaojihusisha na vitendo vya uhalifu na kuziwasilisha kwenye Mamlaka husika.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu tano. Sehemu ya kwanza inapendekeza masharti ya awali kama vile jina la sheria linavyopendekezwa, matumizi ya sheria na tafsiri ya maneno na misamiati itakayotumika. Sehemu ya pili inaanzisha Baraza la Usalama la Taifa na inapendekeza kazi na majukumu ya Baraza. Vile vile inapendekeza kuwepo kwa Sekretarieti ya Baraza na kuainisha kazi ya Sekretarieti. Sehemu ya tatu, inaanzisha Kamati za Usalama za Mikoa na Wilaya na inapendekeza Wajumbe wa Kamati hizo. Kazi za kila ngazi pia zimeainishwa katika sehemu hii.

Sehemu ya nne inaweka adhabu kwa Mjumbe atakayekiuka matumizi ya taarifa za kiusalama, ambazo atazijua kutokana na nafasi yake kama Mjumbe. Kadhalika, sehemu hii inaweka utaratibu wa vikao vya Kamati za Usalama, wajibu wa Kamati kutoa taarifa juu ya shughuli zake na masharti kuhusu gharama za kuendesha Baraza la Usalama la Taifa.

Aidha, Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Usalama wa Taifa, amepewa mamlaka ya kutengeneza Kanuni za Kiutendaji na mambo yatokanayo na masharti ya Sheria hii. Sehemu ya tano, inapendekeza kufanya marekebisho madogo katika sheria tofauti tano, kwa lengo la kuwianisha masharti ya sheria hizo na masharti ya Sheria ya Baraza la Taifa inavyopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, sheria hizo ni *The Tanzania Intelligence and Security Service Act, Cap 406; The National Defence Act, Cap 192; The National Service Act, Cap 193; The Tanzania Citizenship Act na The Disaster Relief Co-ordination Act, Cap 242.*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MHE. MUSSA A. ZUNGU - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA: Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kutoa maoni ya Kamati, kwanza, ninamshukuru mwenyezi Mungu, kwa kunipa pumzi ya kusimama hapa na kupata uhai wa kuweza kutoa maoni ya Kamati yetu. Pili, ninaungana na wenzangu wote, kuwapongeza Wabunge wawili wapya ambao wamechaguliwa na Mheshimiwa Rais jana kujiunga na Bunge hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Wananchi wangu wa Ilala kwa imani na ushirikiano mkubwa ambao wananipa katika Jimbo la Ilala. Bila wao siwezi kufanya kazi ya kuridhisha; wanaisaidia na wananipa ushirikiano mkubwa sana. Namshukuru Mbunge mwenzangu, jirani yangu, Mheshimiwa Iddi Azzan, kwa kushirikiana nami na kunipa miongozo ya kutetea maslahi ya wanyonge katika Majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kutoa maoni haya, nikuombe radhi wewe na baadhi ya Wabunge, kuna nukuu ya Katiba ambayo haikuwahi kuwekwa katika taarifa ambazo ninyi mmeagawiwa. Kwa ruhusa yako, ninaomba katika kuwasilisha niisome na kumbukumbu sahihi ziingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Spika, Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Muswada wa Sheria ya Baraza la Usalama la Taifa 2009 *(The National Security Council Bill, 2009)*.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutuwezesha kuwepo hapa tukiwa na afya njema ili kuweza kujadili mambo muhimu yanayogusa maslahi ya Umma wa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia kuchukua fursa hii, kukushukuru wewe binafsi, kwa busara zako na kuona umuhimu wa Kamati hii kujadili na hatimaye kuwasilisha Maoni yake Kuhusu Muswada wa Sheria ya Baraza la Usalama la Taifa wa Mwaka 2009. Hii inadhihirisha ufanisi wako katika kutekeleza dhana yako ya “*Kasi na Viwango*.”

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Muswada wa Sheria ya Baraza la Usalama la Taifa kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5). Kabla ya kutoa maoni ya Kamati,

ninaomba nichukue fursa hii kueleza hatua iliyotangulia kabla ya Kamati yangu kuushughulikia Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa, Muswada huu ulipelekwa kwa mara ya kwanza kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, ambayo iliwasilisha maoni yake katika Mkutano huu wa Kumi na Nane wa Bunge, kikao cha tarehe 30 Januari, 2010, ambapo Wabunge walipata fursa ya kuuchangia kwa kina na baadaye kuona umuhimu wa kurejesha Muswada huo kwenye Kamati na kupata fursa ya kujadiliana na Serikali kuhusu baadhi ya vifungu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uzito wa hoja hiyo na kwa busara zako, uliamua kupeleka Muswada huu kwenye Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na kuelekeza kuwa, Kamati ishirikiane na Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala katika kuupitia na kuuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, tarehe 4 Februari, 2010 Kamati yangu ilikutana kujadili jinsi itakavyoushughulikia Muswada huu.

SPIKA: Mheshimiwa Zungu, nikuombe kidogo utulie, kuna jambo la Kikanuni lazima tulifanye. Tafadhali.

Waheshimiwa Wabunge, zimesalia dakika dakika kumi tu kufika muda ambao kwa mujibu wa Kanuni ya 28(2), inatubidi tusimamishe shughuli hadi saa 11.00 jioni. Sasa kwa kuwa makubaliano yetu tusifanye hivyo ila tuumalize huu Muswada na pia tupate hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya kuliahirisha Bunge, ninamwomba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, asimame atoe hoja ya kutengua Kanuni hii ya 28(2) ili tuendeele na shughuli za Bunge hadi hapo tutakapomaliza shughuli zilizopangwa. Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 28(b), ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako liendeele kuketi hadi shughuli za Mkutano huu wa Kumi na Nane zitakapokamilika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Hoja ya Kutengua Kanuni za Bunge iliafikiwa na Bunge)

MHE. MUSSA A. ZUNGU - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA: Mheshimiwa Spika, tarehe 4 Februari, 2010, Kamati yangu ilikutana kujadili jinsi itakavyoushughulikia Muswada huu. Katika kuangalia maudhui ya Sheria inayopendekezwa, Kamati ilitumia uzoefu wake katika masuala ya Ulinzi na Usalama na kuona umuhimu wa kuvishirikisha Vyombo vya Ulinzi na Usalama kwa mujibu wa

Kanuni ya 84(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007. Mbali ya kwamba, Vyombo hivyo pia ni vya Serikali yenye mapendekezo ya Sheria hii, Kamati iliamini kuwa, maelezo yake yatakuwa na mchango mkubwa katika kuuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia asili na umuhimu wa Muswada huu, tarehe 10 Februari, 2010, Kamati ilikuwa na kikao cha pamoja na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala. Katika kikao hicho, Mawaziri walio katika sekta inayosimamiwa na Kamati, walihudhuria na kutoa maelezo ambayo yalisaidia kwa kiasi kikubwa. Mawaziri hao ni Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Lawrence K. Masha na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa Mheshimiwa Bernard K. Membe.

Mheshimiwa Spika, kama unavyofahamu, Baraza la Usalama la Taifa ni Chombo nyeti kinachogusa pia Utumishi wa Watumishi wa Umma kwa namna yake. Aidha, utekelezaji wa Sheria inayopendekezwa, unahitaji kuzingatia Sheria nyingine za nchi kama vile Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na Sheria zilizoanzisha Vyombo vya Ulinzi na Usalama. Kwa sababu hiyo, Kamati ilipokutana kuujadilili tena Muswada huu, Mheshimiwa Mathias M. Chikawe, Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Hawa Ghasia, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Mheshimiwa Jaji Fredrick M. Werema, Mwanasheria Mkuu wa Serikali walishiriki katika kikao cha Kamati na kutoa maelezo ambayo pia yalikuwa na mchango mkubwa.

Mheshimiwa Spika, ili kupata Taarifa muhimu kuhusu utaratibu mzuri, maadili muhimu na nguzo za ufanisi wa Baraza linalopendekezwa kuundwa, Kamati pia ilipata maelezo ya Vyombo vya Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utawala Bora), aliileza historia fupi ya uanzishwaji wa Baraza la Usalama wa Taifa, ambapo alifafanua hatua mbalimbali ambazo Baraza hilo lilipitia na lengo la uanzishwaji wake, ikiwa ni Chombo cha Serikali cha kumshauri Rais kuhusu masuala yote ya Usalama wa Taifa. Ili kubainisha baadhi ya masuala ya msingi katika uchambuzi wa Muswada, Mheshimiwa Waziri alifafanua kuhusu Muswada huu ulivyoanza na mapendekezo ya muundo mpya wa Baraza lenyewe.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo ya Waziri, Kamati ilipokea maoni ya Vyombo vya Ulinzi na Usalama. Ninapenda kuliarifu Bunge hili kuwa, vyombo hivi kwa ujumla viliafikiana na mapendekezo ya Serikali, pamoja na maoni ya Waheshimiwa Wabunge yaliyotolewa katika kikao cha tarehe 30 Januari, 2010. Wataalamu hao pamoja na maoni mengine, walishauri kuwa, Muundo wa Baraza uangaliwe kwa makini, jambo ambalo linapaswa kupewa uzito unaotakiwa. Aidha, walitoa maoni kuhusu Mamlaka ya Rais na Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Wilaya.

Mheshimiwa Spika, wakati wa majadiliano kuhusu Muswada huu, masuala ya mamlaka ya Baraza linaloundwa kuwa ya pekee (*Supremacy of the National Security Council*), dhana ya udhibiti baina ya Jumuiya ya Kiraia na Vyombo vya Dola na tatizo linalokusudiwa kutatuliwa na Sheria inayopendekezwa yalijitokeza. Katika ufafanuzi uliotolewa, Ibara za 33 na 44 za Katiba

ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 ni miongoni mwa rejea muhimu zilizotumika.

Mheshimiwa Spika, ninaomba pia kueleza hisia zilizojitokeza kwa baadhi ya watu kuhusu kazi na dhima ya Baraza la Usalama la Taifa. Wapo watu mbalimbali wanaodhani kuwa, kazi kubwa ya Baraza hili ni kuidhinisha nchi kuingia kwenye vita. Wengine wanahisia kuwa, Baraza hili litakiuka Katiba ya Nchi kwa kumshauri Rais kuamua nchi kuingia kwenye vita bila ya kujali masharti yaliyowekwa Ibara ya 44 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuwakumbusha watu hao masharti yaliyowekwa katika Ibara ya 44 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Katika Ibara hiyo, yameelezwa madaraka ya Rais kutangaza hali ya hatari kama inavyoanza Ibara hiyo katika Ibara ndogo ya (1) inayosomeka: “Bila ya kuathiri Katiba hii au Sheria yoyote iliyotungwa na Bunge kwa ajili hiyo, Rais aweza kutangaza kuwapo kwa hali ya vita kati ya Jamhuri ya Muungano na nchi yoyote.”

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo, jukumu la kutangaza hali ya hatari kama nilivyoeleza ni la Mheshimiwa Rais. Hata hivyo, nafasi ya Bunge kama Chombo cha Uwakilishi wa Wananchi katika hali hiyo imebainishwa katika Ibara hiyo, Ibara ndogo ya (2) kwa maneno yafuatayo: “Baada ya kutoa tangazo, Rais atapeleka nakala ya tangazo hilo kwa Spika wa Bunge, ambaye baada ya Kushauriana na Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, ndani ya siku kumi na nne kuanzia tarehe ya tangazo, ataitisha Mkutano wa Bunge ili kuitafakari hali ya mambo na kufikiria kupitisha au kutopitisha azimio la kuunga mkono tangazo la vita lililotolewa na Rais”.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza hayo, ninapenda kuliarifu Bunge hili kuwa, Kamati imeridhishwa na hatua ambazo Serikali ilichukua ili kurekebisha upungufu uliojitokeza katika Muswada huu. Hatua hizo zimezingatia ipasavyo hoja za Waheshimiwa Wabunge na maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuchambua Muswada, pamoja na hoja mbalimbali zilizotolewa na Wajumbe kujibiwa na Serikali, Kamati ilitoa maoni na ushauri kuuboresha Muswada huu. Naomba tena kuliarifu Bunge hili kuwa, Serikali iliafiki karibu maoni yote ya Kamati na kuahidi kuyafanyia kazi katika Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, katika Sehemu ya pili ya Muswada, Ibara ya 4, inazungumzia uanzishwaji na Muundo wa Baraza, yaani *Establishment and Structure of the Council*. Ibara ya 4(2) inaorodhesha Wajumbe wa Baraza la Usalama ambao kwa maoni ya Kamati, Wajumbe hao ni wengi sana. Kamati ilishauri kuwa, katika ibara ya (2), aya (f) mpaka aya (s) zifutwe ili kupunguza ukubwa wa Baraza. Hatua hii itasaidia kuimarisha suala la usiri na wepesi wa kutoa maamuzi na maelekezo. Serikali iliafiki ushauri huu na kuahidi kuuzingatia katika Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uamuzi wa Baraza kwa njia ya kura kama inavyoelezwa na Ibara ya 4(6), Kamati ilikuwa na maoni kuwa utaratibu huu unaingilia mamlaka ya Rais aliyonayo Kikatiba. Kamati ilipendekeza kufutwa kwa ibara hiyo, pendekezo ambalo Serikali iliahidi kulizingatia katika Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, ushauri mwingine uliotolewa na kuafikiwa na Serikali ulihusu Majukumu ya Baraza kama yalivyoainishwa katika Ibara ya 5. Kamati ilishauri kuwa ni vema majukumu yakajikita katika masuala ya utaratibu kama Ibara ya (5) fasili ya 2(a), (b), (c), (f) na (j). Kwa maoni hayo Serikali iliafiki kufuta aya (d), (e), (g), (h) na (i).

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya 6(1) inayotaja Sekretarieti ya Baraza la Usalama la Taifa, Magereza haikutajwa kuwemo katika Sekretarieti; hivyo, Kamati ilishauri kuwa upungufu huu urekebishwe na Serikali iliafiki kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu ya Muswada inazungumzia Kamati za Usalama za Mikoa na Wilaya. Kamati hizi zinaonekana kuwa ni sehemu ya Baraza la Usalama la Taifa, jambo ambalo si jema wala si desturi bora. Kamati inashauri kuwa, kifungu cha maneno “...of the Council” katika Ibara ya 8(1) kifutwe ili kuanzisha Kamati hizo bila ya kuzipa sura ya Baraza, ushauri ambao uliafikiwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 9 inazungumzia majukumu ya Kamati za Usalama za Mikoa. Katika Ibara ya 9(e), inayoipa Kamati ya Usalama ya Mkoa jukumu la kufikiria maombi ya ukazi wa kudumu na uraia na kumshauri Waziri. Kamati ina maoni kuwa, jukumu hilo linakinzana na utaratibu wa kutoruhusu ukazi wa kudumu kwa watu wasiokuwa raia wa nchi hii. Kamati ilishauri kuwa kifungu hicho kiondolewe, ushauri ambao ulipokelewa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya 10 inayohusu Wajumbe wa Kamati za Usalama za Wilaya, Kamati ilishauri kuwa Mshauri wa Mgambo wa Wilaya aongezwe katika orodha ya Wajumbe wanaotajwa na Ibara ya 10(1). Kwa kuwa kwa majukumu na utaalamu wake, ataisaidia sana Kamati hiyo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema tangu awali kuwa, Kamati ilitoa ushauri na maoni zaidi ya hayo niliyoyataja na Serikali iliafiki na kuahidi kuyafanyia kazi ipasavyo. Haya niliyoyataja ni baadhi tu ya maoni yaliyotolewa na Kamati. Yapo mengine kadhaa yaliyoafikiwa na Serikali na kufanyiwa kazi kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho. Aidha, niseme tu kuwa, sote tunafahamu kuwa kutungwa kwa Sheria ni jambo moja na utekelezaji mzuri wa Sheria iliyotungwa ni suala lingine. Kwa mantiki hiyo, Kamati inashauri kuwa utungaji wa sheria hii uende sambamba na utekelezaji bora wa sheria yenyewe na Kanuni zake ili kufikia madhumuni yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia maoni na ushauri kuhusu Muswada, Kamati inashauri kuhusu muundo wa jumla wa Sekretarieti ya Baraza la Usalama la Taifa. Kwa kuzingatia umuhimu wa kuwa na Mshauri wa Usalama wa Taifa (*National Security Advisor*), Kamati inashauri kuwa bila ya kuathiri utendaji na utaratibu uliopo wa Wakuu wa vyombo vingine vya ulinzi na usalama, Serikali ifikirie utaratibu wa kisheria utakaowezesha uteuzi wa mtu huyo na majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuhitimisha maoni ya Kamati kuhusu Muswada huu, naomba nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii. Aidha, namshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, Mheshimiwa Sofia M. Simba, kwa ufafanuzi mzuri aliutoa mara zote alipokutana na Kamati. Nawashukuru pia Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Hussein A. Mwinyi, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Lawrence K. Masha na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa Mheshimiwa Bernard K. Membe, kwa ushirikiano mkubwa na michango yao mizuri waliyoitoa mbele ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema tangu awali, Muswada huu ni nyeti na ulihitaji maoni na maelezo yenye wigo mpana zaidi. Nawashukuru sana Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mathias M. Chikawe, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Mheshimiwa Hawa Ghasia na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Jaji Fredrick M. Werema, walishiriki kwa maelezo yaliyoongeza ufafanuzi katika kuujadili Muswada huu. Michango ya Waheshimiwa Mawaziri wote hao na Wataalamu wa Serikali, ilitusaidia kwa kiasi kikubwa kukamilisha shughuli hii.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya uongozi wa Mheshimiwa George Malima Lubeleje, kwa ushirikiano waliotupatia wakati tukiujadili Muswada huu. Kipekee kabisa, nichukue fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii, kwa umakini mkubwa na ushirikiano waliutoa katika kufanikisha kazi hii. Kwa heshima na taadhima, naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Wilson M. Masilingi - Mwenyekiti, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Anna M. Abdallah, Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mheshimiwa Kanali Mstaafu Saleh A. Farrah, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa, Mheshimiwa Hassan C. Kigwalilo, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa William J. Kusila, Mheshimiwa Edward N. Lowassa, Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mheshimiwa Dkt. John S. Malecela, Mheshimiwa Janeth Maurice Massaburi, Mheshimiwa Kanali Mstaafu Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed, Mheshimiwa Dkt. Ibrahim S. Msabaha, Mheshimiwa Balozi Abdi H. Mshangama, Mheshimiwa Thomas A. Mwang'onda, Mheshimiwa Brig. Jenerali Mstaafu Hassan A. Ngwilizi, Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Muhammad I. Sanya, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo na Mheshimiwa Magalle John Shibuda. (*Makofi*)

Aidha, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge la Tanzania, Dkt. Thomas D. Kasililah na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake. Shukrani za pekee zinatolewa kwa Katibu wa Kamati hii, Ndg. Stella Mlambo, akisaidiana Ndg. Athuman Hussein na Ndg. Yona Kirumbi, kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuratibu shughuli zote za Kamati na kuandaa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mussa Zungu, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kwa kuwasilisha vizuri maoni ya Kamati. Sasa ni zamu ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu masuala haya ya ulinzi na usalama.

MHE. SHOKA KHAMIS JUMA - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA): Mheshimiwa Spika, maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Baraza la Usalama la Taifa wa Mwaka 2009 (*The National Security Council Act, 2009*).

Mheshimiwa Spika, kwa Mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 86(6), Toleo la Mwaka 2007, naomba kutoa maoni kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Baraza la Usalama la Taifa wa Mwaka 2009 (*The National Security Council Act, 2009*).

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba uniruhusu niwashukuru na kuwapongeza Watanzania wote na hasa wapiga kura wangu wa Jimbo la Micheweni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii, kuwapongeza Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu na Mheshimiwa Janeth Mbene, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, nitoe pole kwa Mheshimiwa Felister Bura, kwa kufiwa na mume wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kudumisha amani na utulivu katika nchi ili kutekeleza Ibara ya 146(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inayoeleza kuwa, bila kuathiri maelezo ya jumla yaliyomo katika Ibara ndogo (1) ya Ibara hii, kila chombo cha Serikali za Mitaa, kwa kuzingatia Masharti ya Sheria iliyoanzisha, kitahusika na shughuli zifuatazo: Kuhakikisha utekelezaji wa Sheria ya Ulinzi wa wananchi.

Kwa kuwa Sheria hii katika kifungu cha 10(1), Muundo wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya haimhusishi kiongozi yeyote wa Serikali za Mitaa katika Halmashauri ni kinyume cha dhana ya kupeleka madaraka kwa wananchi hususan katika ngazi ya Halmashauri, ambapo ndipo kwenye wananchi walio wengi. Kwa Muundo wa sasa, Kamati za Ulinzi na Usalama zipo chini ya mfumo wa Serikali Kuu na siyo Halmashauri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona ni vema Uongozi wa Halmashauri ukahusishwa ili kuendana na dhana ya (*D by D*) na mfumo mzima wa kupeleka madaraka kwa wananchi, ambapo Serikali Kuu inasisitiza dhamana ya kupeleka madaraka kwa wananchi, kwa kutofanya hivyo ni kukiuka Katiba ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali imefanya marekebisho kadhaa katika Muswada, tofauti na jinsi ulivyowasilishwa awali. Hata hivyo, inaelekea Serikali haijalewa kabisa hoja za Kambi ya Upinzani na hivyo haijazifanyia kazi ya kutosha. Ili tuweze kueleweka vizuri, tunafanya ufafanuzi wa kina hapa:-

(a) Kifungu cha 4(2) kimefanyiwa marekebisho kwa kufuta kifungu kidogo (f) hadi (s), yaani kwa kuwaondoa Mawaziri pamoja na Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama.

Rekebisho hili ni sahihi, kwa vile Wajumbe hao wasingeliweza kuongeza chochote katika Baraza hilo kwa kuwa ni wajibu wao wa kila siku kumshauri Mheshimiwa Rais katika masuala ya ulinzi na usalama. Kambi ya Upinzani inaunga mkono rekebisho hili. (*Makofi*)

(b) Wajumbe wa sasa wa Baraza hili ni Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mheshimiwa Rais ambaye ndiye Mwenyekiti. Kambi ya Upinzani bado inasisitiza kuwa, haioni umuhimu wa kuwatungia sheria viongozi hao wa juu, ambao kwa vyovyote vile ndio washauri wakuu wa Mheshimiwa Rais katika utendaji kazi wake wa kila siku, hasa katika masuala ya Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapenda kulikumbushia Bunge lako Tukufu, Ibara ya 34(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ninaomba kunukuu: “Mamlaka yote ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano juu ya mambo yote ya Muungano katika Jamhuri ya Muungano na pia juu ya mambo mengine yote yahasuyo Tanzania Bara, yatakuwa mikononi mwa Rais wa Jamhuri ya Muungano.”

Ibara hii ikisomwa pamoja na Ibara ya 148(1) na (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano inayosomeka: “ Bila ya kuathiri masharti yatakayowekwa na sheria yoyote iliyotungwa na Bunge, miongoni mwa madaraka ya Rais akiwa kama Amiri Jeshi Mkuu ni kuyaamuru majeshi ya nchi yatende mambo yanayohusika na vita vya ulinzi wa Jamhuri ya Muungano, mambo ya kuokoa maisha na mali ya watu katika hali ya hatari na mambo mengineyo ambayo Amiri Jeshi ataona yahitajika, na kwa ajili hiyo Amiri Jeshi aweza kuyaamuru hayo majeshi yatende mambo hayo ama ndani au nje ya Tanzania.”

Mheshimiwa Spika, hapa kuna mambo ya msingi ya kuzingatia:-

(a) Mambo yote yaliyotajwa hapa ni mambo ya dharura yasiyosubiri vikao, tena vya kisheria. Amiri Jeshi wakati wowote aweza kuamua hatua yoyote ichukuliwe kwa maslahi ya Tanzania. Ndiyo dhamana aliyopewa na Watanzania. Kambi ya Upinzani haioni kabisa umuhimu wa Amiri Jeshi Mkuu kutungiwa sheria katika utekelezaji wa majukumu yake hayo. Kwa vyovyote vile, Ibara ya 37(1) inatamka bayana kabisa kuwa: “...katika utendaji wa kazi na shughuli zake, Rais atakuwa huru na hatalazimika kufuata ushauri atakaopewa na mtu yeyote, isipokuwa pale tu anapotakiwa na katiba hii au na sheria nyingine yoyote, kufanya jambo lolote kulingana na ushauri anaopewa na mtu au mamlaka yoyote.”

Ni dhahiri Katiba wala Sheria hii, haiweki sharti la kumtaka Rais ambaye ni Amiri Jeshi Mkuu apate ushauri wa lazima katika masuala ya ulinzi na usalama. Hii inabaki kuwa jukumu la msingi la Rais (*prerogative*). Hii ni kwa sababu mamlaka ya Rais katika jambo la ulinzi na usalama ni *indivisible* na ana *absolute powers*. Rais ana mamlaka ya kutangaza vita kwa kuokoa Taifa hata bila ya kupata ushauri wa Makamu, Rais wa Zanzibar au Waziri Mkuu au Waziri Kiongozi katika jambo la kulinda *integrity* na *independence* ya Tanzania, yaani ardhi yote ya Tanzania na Uhuru wa Tanzania.

Ni kwa msingi huo, Ibara ya 148(2) (a) hadi (d) zinafafanua kwa kina madaraka ya Rais na inatamka wazi kuwa "... Mambo yafuatayo yatakuwa mikononi mwa Amiri Jeshi Mkuu." Kifungu hiki, hakimtaki Rais kupata ushauri, japo hakatazwi, kwa mtu au chombo chochote na ni dhahiri, kabla Rais kwa busara yake hajachukua hatua yoyote kubwa, atashauriana na Viongozi Wasaidizi wake Wakuu. (*Makofi*)

(b) Mheshimiwa Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano, haitoi ufafanuzi wowote kuhusu majukumu au wajibu wa Makamu wa Rais au Rais wa Zanzibar, isipokuwa majukumu yake kama Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; lakini vinginevyo, hata Rais wa Zanzibar pamoja na Makamu wa Rais, wanaingia katika Baraza la Mawaziri (Ibara ya 54(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania).

Ibara ya 54(1) ndiyo inayounda Kikatiba Baraza la Mawaziri na inasema wazi: "Kutakuwa na Baraza la Mawaziri ambalo Wajumbe wake watakuwa ni Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Rais wa Zanzibar na Mawaziri wote." Mtu pekee ambaye hayuko ni Waziri Kiongozi wa Zanzibar. Katiba ya Nchi inatamka wazi kabisa kuwa, "...Baraza la Mawaziri litakuwa ndicho chombo kikuu cha kumsahuri Rais juu ya mambo yote yanayohusika na utekelezaji wa madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii na litamsaidia na kumshauri Rais juu ya jambo lolote litakalowasilishwa kwenye Baraza hilo kwa mujibu wa maagizo maalum au maagizo ya jumla yatakayotolewa na Rais.

(c) Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais, Makamu wake, Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi wa Zanzibar ni watu ambao kimsingi, Kambi ya Upinzani inaamini wanawasiliana siyo tu kwa njia ya Mikutano, bali hata kwa simu, kutembeleana au kumtembelea Rais na kumpa ushauri wakati wote utakapokuwa unahitajika. Isitoshe, iwapo Mheshimiwa Rais, ataona kuna haja ya kuwa na mfumo wa kukutana kila wakati, Rais ana fursa na nafasi pana ya kutumia madaraka ya kuanzisha mfumo huo rasmi wa mawasiliano kati yake na Wasaidizi wake Wakuu kupitia *instruments. Decree* zinazohitaji tu kutangazwa katika Gazeti la Serikali kama Mawaziri wanavyofanya mara kwa mara kutengeneza Kanuni mbalimbali na Katiba, inampa mamlaka hayo kwa mujibu wa Ibara ya 37(8) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(a) Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani haioni kabisa mantiki ya Serikali kuleta tena Muswada huu, aidha, haukufanyiwa kazi ya kina au haujaiva vizuri ama Serikali haijatafakari kwa kina kazi za Baraza hili.

Yote yaliyotajwa katika majukumu ya Baraza hili ni majukumu ya kila siku ya Mawaziri wa Idara husika wa Ulinzi na Usalama wa Taifa, Wakuu wa Vyombo hivyo na hata chombo chochote ambacho Rais kwa mamlaka yake anaweza kukiunda kumsaidia kupata ushauri wa kina.

(b) Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaamini Rais hahitaji kutungiwa sheria ya kuwa na chombo cha kumshauri katika masuala mazito kama ya ulinzi na usalama, kwani ana uwezo wa kumwita mtu yeyote, kiongozi au hata asiye kiongozi, kama anaona ana taarifa muhimu kwa ulinzi wa nchi hii, ilimradi yeye ameridhika kuwa anahitaji ushauri au taarifa kwa

mtu huyo. Mamlaka hayo anayo pia kwa kumwita Makamu wake wa Rais, Waziri Mkuu, Rais wa Zanzibar wakati wowote bila kuwa na sheria mahususi iliyotungwa na Bunge. (*Makofi*)

(c) Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani imeona ni busara kuchambua kwa kina kipengele hiki kwani masuala ya Ulinzi na Usalama wa Taifa ni mazito, yanahitaji mashauriano mapana kwa mustakabali wa nchi yetu na utafakari na utafiti wa kina, wenzetu wanaendesha Mabaraza ya aina hiyo kama tutakavyoeleza hapo chini. Ingelikuwa Wajumbe wa Baraza wametoka nje, aidha, kutokana kwa vyombo au mhimili mwingine au hata *eminent persons* katika nchi hii, Kambi ya Upinzani isingelikuwa na tatizo kwani tunahitaji sana ushauri kutoka kwa watu walio nje ya Serikali. Kwa hali ilivyo ni kuwa Serikali inajishauri yenyewe, jambo ambalo kwa mujibu wa Ibara ya 54 haitaleti tija yoyote bali kuongeza gharama, kwani chombo hicho kimewekewa Sekretarieti ya peke yake. Tunahitaji kutumia fedha na rasilimali chache za nchi hii vizuri zaidi kwa kufanya maamuzi ya busara.

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi huo wa kina, kwa manufaa ya Bunge lako Tukufu, ninapenda kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kupitia mafungu mengineyo ili kujenga vizuri hoja yetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo yetu hapo juu, Kambi ya Upinzani imefanya uchunguzi katika nchi mbalimbali na tungependa kueleza ifuatavyo: Kifungu cha 4(2) cha Muswada kinachohusu Wajumbe wa Baraza la Usalama la Taifa. Baada ya kuliangalia na kufanya utafiti wa Muundo katika nchi nyingine wamefanyaje, kwa kuzingatia faida na madhara na kwa kuwa nia ya kulinda maslahi ya Taifa; Kambi ya Upinzani inapendekeza Muundo wa Baraza uwe kama wa nchi nyingine ambapo washauri hao wanatoka nje ya mfumo wa Serikali. Kambi inashauri Serikali ifanye utafiti wa kina ili kuleta sheria bora na imara kwa ulinzi na usalama wa nchi yetu, badala ya kuipitisha haraka haraka tu kama Serikali inavyofanya sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani imethibitisha kuwa, kama ilivyokuwa ikisema kila mara kuwa Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Wilaya zilikuwa zinafanya kazi zake bila kuwepo kisheria na wakati mwingine zilikuwa zinafanya kazi bila kufuata taratibu za jamii katika masuala mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 5(2)(a) yametumika maneno “*National Interests*” (Maslahi ya Taifa); Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe tafsiri ya maneno hayo kwani sasa matakwa ya wale walio madarakani ndiyo yanayotafsiriwa kama ni *National Interests* badala ya ustawi wa jamii katika tafsiri pana, kwani jamii imegawanyika katika makundi mbalimbali ambayo wananchi wanaona kuwa ni maslahi ya Taifa kwa mtazamo wao. Kuacha kuweka tafsiri ya neno hilo kwa chama kinachowala kwa wakati huo ni kuhatarisha usalama wenyewe wa Taifa, ambao ndio lengo kuu la sheria hii.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 6(1) kinachohusu Wajumbe wa *Secretariat* kимemtaja mtu kuwa Mratibu (*Coordinator*), lakini katika Muswada huu *Coordinator* na Wasaidizi wake hawakutolewa maelezo ni sifa gani wanatakiwa kuwa nazo. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuweka wazi sifa za *Coordinator* na Wasaidizi wake.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 15 cha Muswada huu, kuhusiana na gharama za Baraza; kwa Muundo wa Baraza ulivyo, gharama zote za Kamati zinatakiwa zilipwe kutoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali (*Consolidated Fund*); ni dhahiri kuwa hii itaongeza matumizi ya Serikali na kuzidisha mzigo kwa wananchi. Kambi ya Upinzani inataka kujua kwamba, fedha hizi zitatumika kwenye Baraza la Usalama la Taifa peke yake au hadi Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Wilaya? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Shoka, kwa kuwasilisha maelezo ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada. Waheshimiwa Wabunge, ninayo majina ya wachangiaji wawili; Mheshimiwa John Samweli Malecela, Mbunge wa Mtera na Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli.

MHE. JOHN S. MALECELA: Mheshimiwa Spika, kwanza, ningependa nichukue nafasi hii nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Ningependa nianze kwa kusema kwamba, Muswada kama ulivyoletwa sasa, ninaunga mkono mia kwa mia na ninawasihi Wabunge wenzangu tuunge mkono. (*Makofi*)

Kabla sijakwenda kwenye Muswada, ningependa na mimi niungane na wenzangu katika kutoa rambirambi zangu na za Wananchi wa Jimbo la Mtera, kwa Mheshimiwa Felister Bura kwa kufiwa na mpendwa mumewe. Tunampa pole, ingawa sisi wanadamu wenzake tunaweza kumfariji lakini Mwenyezi Mungu ambaye ndiye hutoa uhai na akauchukua tena, atamfariji zaidi kuliko sisi.

Nichukue pia nafasi kuwakaribisha na kuwapongeza wenzetu walioteuliwa kuwa Wabunge na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nao ni Mheshimiwa Ladhu na Mheshimiwa Mbene. Kwenu tunasema karibuni Bungeni na tuna hakika tutashirikiana katika ujenzi wa Taifa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa ningependa nije kwenye Muswada wenyewe; kwanza, ningependa nichukue nafasi hii kusema kwamba, kwa kweli Serikali imechukua hatua kubwa sana, imekuwa kama kuandika Muswada upya na kwa hali nzuri zaidi na inayoeleweka. (*Makofi*)

Jambo la kwanza ambalo lilikuwa tofauti katika Muswada kama ulivyokuja mara ya kwanza ilikuwa ni ukubwa wa Baraza, Baraza lilikuwa karibu na watu ishirini, lakini sasa mtaona kwamba katika Ibara ya 4 baada ya marekebisho ni watu watano tu, ambao ni Rais, Makamu wa Rais, Rais wa Zanzibar, Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi. Sasa mimi ninasema, kwanza, kwa hawa hata watu wanaposema suala la matumizi, hili Baraza litatumia fedha nyingi. Mimi ninadhani hili kwa kweli si sawa, kwanza, ukiwaona walivyo matumizi yake hayatakuwa makubwa. (*Makofi*)

Jambo lingine ambalo lilikuwepo na lilikuwa linaleta utata, ilikuwa ni Ibara ndogo ya 6 ya Ibara ya 4; vyombo vyote katika Jamhuri ningependa niseme katika ulimwengu huu,

mbinguni kuna Mungu na kwa sisi binadamu Mungu wa pili ni kama Rais, kwa sababu huyu ndiye ambaye Watanzania wote wamempa madaraka ya kuiangalia Tanzania, wamempa madaraka ya usalama wa Tanzania. Kwa hiyo, Ibara ya 6 ndogo ya Ibara ya 4 ilikuwa inakwenda kinyume na takwa hilo, kwa sababu ilikuwa inasema kwanza lile Baraza kubwa liwe na haki ya kupiga kura. Sasa kupiga kura maana yake ndiyo kusema kuwa, kuna mahali ambapo Rais angekuwa anataka hivi lakini Baraza linapiga kura vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, tukiendelea katika Muswada huu, kipengele kingine ambacho kilikuwa kinaleta matatizo kilikuwa ni *schedule* ambayo ipo ukurasa wa 16. Kwenye *schedule* hii kulikuwa na mambo mengi sana ambayo yalikuwa yanapingana na uendeshaji wa nchi. Ninashukuru sana kwamba, sasa *schedule* hii yote imefutwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ningependa nirudie tena kuishukuru Serikali kwa jinsi ilivyokubali kwamba, Muswada huu ubadilishwe kama ulivyobadilishwa na uwekwe katika hali ambayo itakuwa ni ya manufaa kwa nchi yetu. Ningependa kuisitiza usalama wa nchi ndio kitu muhimu sana, bila ya usalama wa nchi hakutakuwa na demokrasia, bila ya usalama wa nchi hakutakuwa na maendeleo, bila ya usalama wa nchi sidhani kama tungekuwa na Bunge lililojema, safi na watu wamekaa kwa usalama kama tulivyo kaa sasa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa John S. Malecela kwa tahadhari hizo. Msemaji wangu wa mwisho ni Mheshimiwa William H. Shellukindo.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niseme machache.

Kwanza kabisa, ninapenda kuipongeza Serikali kwa kuwa sikivu na imeonesha kwa vitendo kuwa sikivu. Ninasema hivi kwa sababu ushauri wote uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge waliozungumza wakati ule mimi nikiwa mmojawapo, wote umechukuliwa na umechukuliwa kwa sababu tulitoa kwa dhati na kwa uzalendo na wao wameangalia uzalendo ulivyo, tunashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Muswada huu haukuandikwa upya, niliuchangia wakati ule kwenye mambo ya kuimarisha tu. Ninaomba mwongozo wako kama niyaseme hapa ama ningojee kwenye kupitia vifungu ili tusipoteze muda zaidi.

SPIKA: Yaseme sasa ili Mheshimiwa Waziri aweze kujibu.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Sawa sawa. Katika ukurasa wa 5 ambao ni mwendelezo wa kifungu kikubwa cha 4(4), nimepitia yale marekebisho yote, ambacho kilikuwa cha 5 katika ukurasa wa 5, kuna sahihisho pale ili sentensi ikae sawasawa panaposema *The Council may invite any person*, nadhani badala ya *in its meeting* iwe *to its meetings* na nimemwomba *Attorney General* kwamba, ninadhani ile *its* ya pili katika mstari wa pili ninadhani haihitajiki. Hiyo ni moja kwa upande huu ukurasa wa tano.

Halafu ukurasa wa 6 kifungu 6 ambacho kina marekebisho, nimeangalia ile *subcaluse A* kwamba, *The Chief Secretary who shall be the head*, ile *head* isahihishwe iwe *capital and coordinator* ile *The Coordinator* iondoke pale, ninadhani ni *repetition*. Tunaweka tu hiyo ili mambo yakae vizuri, maana Sheria hii ya Rais ni lazima tuwe waangalifu sana, wenzake wanaweza wakaichukua wakasema hebu tuitazame halafu wakakuta vitu vidogovidogo hivyo; mtatuwia radhi kidogo.

Mwendelezo wa kifungu cha 7, ukurasa wa 7, *subclause 1(d)* inayosema; *keep and maintain records and control confidentiality of all documents relating to the Council activities*, pale kuna *Councils* hiyo “s” inakuwa *Council’s activities*.

Subclause ndogo ya pili katika *clause* hiyo hiyo ya 7, nilitaka tu tunyooshe ile ya pili inayosema *The Secretariat may co-opt any person during its meetings*; siyo mkutano mmoja ni *its meetings*.

Halafu tukienda kwenye ukurasa wa 8, *clause* ya 8(3) vilevile ninaomba ile sentensi inayoanzia na *the regional security committee may invite any person in*, badala ya “in” iwe “to” na ile *meeting* iwe *to its meetings*.

Ukurasa wa 11, *clause* ya 14(2), ule mstari wa tatu ile sentensi ya tatu inayosema *Committees considers* ile “s” ingeondoka kwa sababu kuna *plural* pale iwe *committees may consider* badala ya *considers*.

Ukurasa wa 12, *clause* ya 14(3) ule mstari wa pili unaoanzia na *regional security committees and the district security committee* pawe na “s” kwa maana zipo nyingi hizo.

Halafu *clause* ya 19, ukurasa wa 13, *subclause A*, roman (ii), ile sentensi inayoanzia na *inserting the words the council immediately after the words United Republic appearing in fourth* pale tuweke in the fourth line.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii kwa hayo machache ambayo nimeyatoa na ninashukuru. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Shellukindo, kwa kudhihirisha uzoefu wako katika kuchambua nyaraka hizi za Serikali na kwa kuwa nimeona Mwanasheria Mkuu wala hakushtuka na hayo, ninayachukulia kwamba ni masahihisho ya kawaida na yasituchukulie muda tena kwenye Kamati ya Bunge Zima.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, ninapenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi, kumpongeza Mheshimiwa Sophia Simba, Waziri wa Utawala Bora, kwa kuwasilisha Muswada mzuri, wenye nia thabiti ya kudumisha usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya Muswada huu kupitiwa upya ni ukweli usiojificha kuwa, Mheshimiwa Waziri pamoja na Watendaji wake kwa ushirikiano wa Kamati ya Utawala, Sheria

na Katiba na Tume ya Ulinzi na Usalama, wameufanyia marekebisho mazuri sana nimeridhika kabisa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya na Mikao ziwe na masanduku ya kupata taarifa na maoni mbalimbali kutoka kwa Wananchi, Watendaji na Viongozi mbalimbali, hii itasaidia vikao vyao kuwa na taarifa za hali ya usalama.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ninapenda kumalizia mchango wangu kwa kuunga mkono Muswada huu mia kwa mia na Mungu awatangulie wote watakaohusika kwenye Kamati Teule za Wilaya, Mikoa na Tume ya Ulinzi na Usalama, ikiongozwa na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wetu mpendwa.

SPIKA: Sasa nitamwita mtoa hoja, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utawala Bora), Mheshimiwa Sophia Simba.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA): Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru tena kwa kunipa nafasi hii ya kusimama hapa mbele ili niweze kuhitimisha yale ambayo tuliyaanza muda mfupi uliopita.

Nianze kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia Muswada huu kwa makini na kwa uwezo mkubwa, wakiwemo waliochangia kwa maandishi na kwa kusema hapa ndani ya Bunge lako Tukufu.

Kwa namna ya pekee, naomba kuzishukuru Kamati za Kudumu za Bunge za Nje, Ulinzi na Usalama na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa michango makini ambayo tumeizingatia na imeleta mabadiliko makubwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, ninapenda kuishukuru Kambi ya Upinzani kwa michango yake, bila kuwasahau Mawaziri mbalimbali ambao wamefanya kazi kubwa; walikuja na timu kubwa wakiongozana na Vyombo vya Ulinzi ambavyo viko chini yao, akiwemo Mheshimiwa Benard Membe, Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mheshimiwa Mwinyi, Mheshimiwa Lawrence Masha, Mheshimiwa Chikawe, pamoja na Uongozi wa Mheshimiwa *Attorney General*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa ridhaa yako, ninaomba sasa niwatambue Waheshimiwa Wabunge walichangia hoja hii. Waliochangia wa kusema ni Mheshimiwa Mussa A. Zungu - Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma - Msemaji wa Upinzani, Mheshimiwa John S. Malecela na Mheshimiwa William Shellukindo. (Makofi)

Waheshimiwa waliochangia kwa maandishi ni mmoja tu naye ni Mheshimiwa Diana M. Chilolo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ninaomba nijibu kwa kifupi baadhi ya hoja ambazo nyingine zimekuwa zikijirudiarudia.

Hoja ya ukubwa wa Baraza, ambalo limezungumzwa katika kifungu cha 4 nilishajibu kwamba, sasa tumebakiza watu watano ambao ni Rais, Makamu wa Rais, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, ninapenda nianze kwa hoja zilizotolewa na Kamati. Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama imetupongeza na imeunga mkono hoja, lakini imetoa hoja moja nayo ni kwamba, Serikali iangalie uwezekano wa kuwa na Mshauri wa Usalama wa Taifa (*The National Security Advisor*).

Mheshimiwa Spika, Serikali inapokea ushauri huu na itautafakari na kuona uwezekano wake, lakini si kuliweka katika Muswada huu kwa sasa kwa vile hili ni jambo jipya na linahitaji kupata taratibu zote za Serikali na kukubalika.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa nijibu yale ambayo yamezungumzwa na Kambi ya Upinzani. Kambi ya Upinzani inasema kwamba, si sahihi kumtungia Amiri Jeshi Mkuu Sheria katika masuala ambayo ana mamlaka nayo.

Kama nilivyosema wakati nikiwasilisha hoja hii, lengo la Muswada huu si kumtungia Amiri Jeshi Mkuu, Sheria hii itaweka chombo cha kumshauri Amiri Jeshi Mkuu na hivyo kurahisisha utekelezaji wa Mamlaka yake Kikatiba. Dhana ya kuwa na Baraza la Usalama la Taifa halimwondolei madaraka Rais hata kidogo, hili ni Baraza la Ushauri na nchi nyingi wamekuwa na Baraza la Ushauri kama hili ikiwemo Marekani, China, Pakistan, Ghana na nchi nyingine. Kwa hiyo, halitamwondolea madaraka yake kama inavyochukuliwa.

Suala lingine ambalo Kambi ya Upinzani imeuliza ni kwamba, Wajumbe wa Baraza la Usalama wa Taifa watoke nje ya mfumo wa Serikali. Dhana ya kuwa na Wajumbe kutoka Serikalini ni kwa ajili ya usiri na uwajibikaji. Aidha, si kweli kwamba, nchi nyingine zina Mabaraza ambayo yanaundwa na Wajumbe kutoka nje ya mfumo wa Serikali, kama yapo ni machache sana, lakini kwa nia ya kuwa na usiri na uwajibikaji ni vema kuwa na viongozi ambao wapo katika nafasi nyingine za Serikali, tafiti zinaonesha kwamba, nchi nyingi wanatumia utaratibu kama huo.

Kambi ya Upinzani pia imezungumzia Uongozi wa Halmashauri kutohusishwa ni kwenda kinyume na dhana ya *D by D*. Niseme tu kwamba, jukumu la kuweka utaratibu na miongozo kuhusu Ulinzi na Usalama ni la Serikali Kuu, Serikali za Mitaa ina jukumu la utekelezaji kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa kwa mujibu wa Ibara ya 34(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya ndizo zilizopewa jukumu na Serikali Kuu katika maeneo yao na Serikali za Mitaa zitatekeleza utaratibu uliowekwa na Kamati hizo; hivyo, siyo sahihi kuhusishwa katika Kamati hizo. Hata hivyo, kukiwa na haja ya kupata ushauri kutoka kwa Viongozi wa Serikali za Mitaa, wataitwa kwa mujibu wa kifungu kinachoruhusu mtu yeyote kutoa ushauri wa jambo lolote.

Mheshimiwa Spika, niendeleo kujibu yale ambayo pengine yalitolewa siku ile na hapa hayakurudiwa tena. Kutungwa kwa sheria hii kutaleta ongezeko la Sheria na hivyo kuwa na sheria nyingi zinazoshughulikia ulinzi na usalama; hili limejadiliwa sana.

Maoni ya Serikali ni kwamba, Sheria hii haiundi chombo kingine chenye sura ya vyombo vilivyoanzishwa na Sheria ambazo zimefafanuliwa hapa nchini.

Sheria nyingine ni kama *The National Security Act* inayoainisha mambo yanayohusu usalama wa taifa na inazuia vitendo hatarishi kwa usalama wa taifa.

Sheria nyingine ni *Tanzania Intelligence and Security Act* inayounda Idara ya Usalama wa Taifa na kuweka utaratibu wa kiutendaji. Aidha, *The National Defence Act* inaunda Jeshi la Ulinzi, Sheria ya *The Police Force and Auxiliary Forces Act* inayounda Jeshi la Polisi, Sheria ya *Prisons Act* inayonga Jeshi la Magereza na Sheria ya *The Immigration Act* inayounda Idara ya Uhamiaji. Kila chombo kilichoundwa na Sheria hizi, kinafanya kazi zake na kutoa ushauri kwa Rais bila kukihusisha chombo kingine.

Hivyo basi, ni vema kuwa na uratibu wa ushauri unaowasilishwa kwa Rais na vyombo hivyo. Baraza linalopendekezwa litakuwa ni Chombo Kikuu cha Kumshauri Rais juu ya masuala yote yanayohusu Ulinzi na Usalama wa Taifa kutokana na taarifa za kitaalamu zilizotoka katika vyombo vya Ulinzi na Usalama vilivyopo. Utaratibu huu utawezesha Rais kupata ushauri wa vyombo hivi.

Kwa nini itungwe sheria mpya wakati kuna sheria nyingine zinazoshughulikia masuala ya ulinzi na usalama?

Maoni ya Serikali ni kwamba, upo umuhimu wa kutunga Sheria hii ili kuweka utaratibu wa kuratibu masuala ya Ulinzi na Usalama kutoka kwenye vyombo mbalimbali vilivyoundwa Kisheria. Kwa kuwa vyombo vya Ulinzi na Usalama vimeundwa kisheria na masharti ya kazi zake yamewekwa kisheria, siyo vema kuendelea kuratibu ushauri kutoka kwa vyombo hivyo kwa utaratibu wa kiutawala tu.

Hoja kwamba, kuundwa kwa Baraza kutaongeza gharama; maoni ya Serikali ni kwamba, chombo hiki kitafanya shughuli za uratibu zaidi kuliko suala la kiutendaji. Kimsingi, sheria hii inalenga kurasimisha utaratibu ambao tayari upo kiutawala endapo mapendekezo ya kupunguza Wajumbe wa Baraza yatakubaliwa kama ilivyo sasa. Ni dhahiri kwamba, gharama za uendeshaji zitakuwa ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa nirudi kwa waliochangia kwa maandishi na nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa John Samuel Malecela, Mzee wetu, ambaye kwa kweli ametusaidia sana katika utungaji wa sheria hii hasa kwa michango yake na kwa jinsi alivyotupa moyo kwa kazi nzuri tuliyoifanya. Tunakushukuru sana, tukiamini unalielewa vizuri sana Baraza hili kwani ulikuwa mmojawapo katika kulihudumia Baraza hili wakati likiwa Tume na wakati mwingine. Kwa hiyo, tunakushukuru sana. (*Makofi*)

Tunashukuru sana Mheshimiwa William Shellukindo, kwa pongezi zako na pia tumezingatia mabadiliko yote uliyoyatoa ambayo yana msingi; tumeyachukua na tutaweka *amendments* hizo ndani ya Muswada wenyewe kama ulivyotoa.

Wa mwisho ambaye amechangia kwa maandishi alikuwa Mheshimiwa Diana Chilolo; yeye ametoa pongezi na amesema Kamati za Mikoa na Wilaya ziwe na sanduku la maoni.

Maoni yake ni sawa katika kusaidia upatikanaji wa maoni ya wananchi, lakini hilo litakuwa ndani ya utendaji wa kazi wa kamati hizo, hatutakuwa sahihi kuweka suala hilo katika sheria kwa sababu hata sasa bado upo utaratibu wa kutoa maoni hapa na pale; kwa hiyo, inawezekana kabisa itaendelea. Nakushukuru na ninaomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Utawala Bora. Waheshimiwa Wabunge, mtoa hoja ametoa hoja ya kuukubali Muswada huu wa Baraza la Usalama la Taifa na imeungwa mkono, lakini kwa mujibu wa Kanuni za 86, 87 hadi 88, inabidi tupitie utaratibu wa namna ya kuzishughulikia.

KAMATI YA BUNGE ZIMA

Muswada wa Sheria ya Baraza la Usalama la Taifa wa Mwaka 2009 (*The National Security Council Bill, 2009*)

Kifungu cha 1

Kifungu cha 2

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 3

Kifungu cha 4

Kifungu cha 5

Kifungu cha 6

Kifungu cha 7

Kifungu cha 8

Kifungu cha 9

Kifungu cha 10

Kifungu cha 11

Kifungu cha 12

Kifungu cha 13

Kifungu cha 14

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)

Kifungu cha 15

Kifungu cha 16

Kifungu cha 17

Kifungu cha 18

Kifungu cha 19

Kifungu cha 20

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 21

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

(Bunge lilirudia)

Muswada wa Sheria ya Baraza la Usalama la Taifa wa Mwaka 2009
(The Security Council Bill, 2009)

(Kusomwa Mara ya Tatu)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA): Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kuwa, Kamati ya Bunge Zima, imeupitia Muswada wa Sheria ya Baraza la Usalama la Taifa wa Mwaka 2009 kifungu kwa kifungu pamoja na marekebisho yake na kuukubali.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kuwa Muswada huo sasa upitishwe na Bunge la Tatu. Naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utawala Bora). Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyopo mbele yetu ni kwamba, tuukubali Muswada pamoja na marekebisho.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya
Tatu na Kupitishwa)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Muswada sasa umesomwa kwa mara ya tatu na kwa mujibu wa Kanuni ya 91, hiyo ni ishara kwamba, Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, limeupitisha Muswada huo na ni sheria ambayo itasubiri hatua ya mwisho ya Mheshimiwa Rais.

Namtakia mema Mheshimiwa Waziri katika hatua zinazofuata na ninampongeza kwa kuonesha jinsi Serikali ilivyo na usikivu, kwa sababu hii ni kazi ambayo imefanywa kwa pamoja

na hii ni dalili nzuri sana kwamba, Bunge na Serikali tufanye kazi kwa pamoja. Ahsante sana. (Makofi)

KUAHIRISHA BUNGE

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba nimwite Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili aweze kutoa hoja ya kuliahirisha Bunge. (Makofi)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, napenda kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwenye Rehema, kwa kutuwezesha kumaliza mwaka 2009 na kuanza mwaka 2010 salama. Nawatakia Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wote, Kheri ya Mwaka 2010. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kabla ya yote, napenda nitumie nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu na Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Wabunge katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hongereni Sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tarehe 31 Desemba, 2009, Nchi yetu ilipata msiba mkubwa wa kuondokewa na Mzee wetu, Mheshimiwa Rashidi Mfaume Kawawa, Waziri Mkuu Mstaafu na Makamu wa Pili wa Rais na wote tunakumbuka mchango wa Mheshimiwa Rashid Mfaume Kawawa kwa Taifa hili. Tunamwomba Mwenyezi Mungu, ailaze Roho ya Marehemu mahali Pema Peponi. Amina.

Nitumie nafasi hii kumpa pole Mheshimiwa Vita Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, pamoja na Familia ya Marehemu na Watanzania wote, kwa msiba huu wa Mzee wetu Rashid Mfaume Kawawa, ambao umewagusa Watanzania wote. Pia, nitumie nafasi hii kumpa pole kwa kufiwa na ndugu yake Mpendwa, Habiba Kawawa. Mfululizo wa matukio haya, kwa imani zetu tunasema yote haya ni Mapenzi ya Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, asubuhi ya leo tulipata Taarifa ya Msiba wa Mume wa Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Felister Aloyce Bura, Mbunge wa Viti Maalum, uliotokea jana Dar es Salaam. Sote tunampa pole sana. Nitumie fursa hii pia kutoa salamu za pole kwa Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote waliopoteza ndugu, jamaa, marafiki na mali kutokana na ajali, maradhi na sababu nyingine mbalimbali wakati wa kipindi hiki tangu Mkutano wa Kumi na Saba wa Bunge.

Ni hivi majuzi tu tarehe 2 Februari, 2010, ambapo Taifa limepoteza watu 25 kwa ajali iliyohusisha basi la abiria la kampuni ya Chatco, ambalo liligongana na basi dogo la Kampuni ya Mzuri Transport. Ajali hiyo ilitokea katika Kijiji cha Kitumbi, Kwamgolo Wilayani Handeni, Mkoani Tanga. Naungana na ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu wote, kumwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

Nitumie pia nafasi hii kutoa pole za pekee kwa Watanzania wote, walioguswa kwa namna moja au nyingine na majanga mbalimbali yakiwemo mafuriko yaliyotokea kutokana

na mvua katika kipindi hiki. Nimetembelea baadhi ya maeneo kama vile Wilayani Kilosa na Mpwapwa na nimejionea mwenyewe athari kubwa zilizotokana na mafuriko hayo. Baadhi ya maeneo athari ni kubwa sana na itachukua muda kurekebisha miundombinu ya Barabara na Reli iliyoharibika. Nawaomba waathirika na Wananchi wote kuwa na subira wakati Serikali inaendelea na juhudi za kukabiliana na maafa hayo.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu, Waheshimiwa Wabunge walipata fursa ya kuchagua Wajumbe watakaoliwakilisha Bunge letu kwenye Taasisi Tano muhimu za humu Nchini. Nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Profesa Feetham Filipino Banyikwa, Mbunge wa Ngara na Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini, kwa kuchaguliwa kuwa Wajumbe katika Bodi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Napenda pia kuwapongeza Mheshimiwa Daniel Nicodem Nsanzugwanko, Mbunge wa Kasulu Mashariki kuwa mwakilishi wa Bunge katika Bodi ya Chuo Kikuu cha Biashara na Stadi; Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge wa Kisesa kuwa mwakilishi wa Bunge hili katika Kamisheni ya Vyuo Vikuu Tanzania; Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mbunge wa Viti Maalum kuwa Mjumbe katika Bodi ya Taasisi ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere na Mheshimiwa Dkt. Binilith Satano Mahenge, Mbunge wa Makete kuwa Mjumbe katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya. Wote tunawatakia kheri katika kuliwakilisha Bunge hili katika Bodi za Taasisi hizo. Aidha, matumaini yetu ni kwamba, uwakilishi wao katika Taasisi hizi utatoa changamoto kwa Taasisi hizo katika kuongeza ufanisi zaidi na hivyo kutoa huduma bora zaidi kwa Wananchi.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kwa namna ya pekee, kumpongeza Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya, Mbunge wa Viti Maalum, kwa kuchaguliwa bila kupingwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya *Democracy Governance and Gender Equality* katika Bunge la SADC. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Willibrod Slaa, Mbunge wa Karatu, kwa kuchaguliwa tena kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya *Interparliamentary Capacity Building Committee*, moja ya Kamati Tano katika Bunge la SADC. Kuchaguliwa kwao ni ishara kwamba, wanatuwakilisha vizuri katika Bunge hilo ambalo Makamu Mwenyekiti wake ni Naibu Spika, Mheshimiwa Anne Makinda, Mbunge wa Njombe Kusini. Wote tunawapongeza kwa kutuwakilisha vema.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Timu ya Mpira ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa “kututoa Mchanga Machoni” kufuatia ushindi kwenye mashindano ya Ligi ya Mabunge ya Afrika Mashariki kuadhimisha Miaka Kumi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Timu hiyo ilishinda kwa Mabao 2 – 0 dhidi ya Timu ya Uganda. Tunajivunia Ushindi huu na Hongera Sana.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu wa Kumi na Nane wa Bunge, jumla ya Maswali 168 ya Msingi na 328 ya Nyongeza yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Wizara husika. Aidha, Utaratibu wa Maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kila Alhamisi (Chini ya Kanuni ya 38(1) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007), uliendelea kwa Waheshimiwa Wabunge kuuliza na kujibiwa. Jumla ya Maswali 22 ya Msingi na 14 ya Nyongeza yaliulizwa na kujibiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu, jumla ya Miswada minane imesomwa kwa mara ya kwanza na kupitia hatua zake zote. Miswada hiyo ni:-

(i) Muswada wa Sheria ya Uguzi na Ukunga ya Mwaka 2009 (*The Nursing and Midwifery Bill, 2009*);

(ii) Muswada wa Sheria ya Mawasiliano ya Elektroniki na Posta wa Mwaka 2009 (*The Electronic and Postal Communication Bill, 2009*);

(iii) Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2009 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.3) Bill, 2009*);

(iv) Muswada wa Sheria ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi wa Mwaka 2009 (*The Architects and Quantity Surveyors (Registration) Bill, 2009*);

(v) Muswada wa Sheria ya Gharama za Uchaguzi wa Mwaka 2009 (*The Election Expenses Bill, 2009*);

(vi) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi wa Mwaka 2009 (*The Electoral Laws (Miscellaneous Amendments) Bills, 2009*); na

(vii) Muswada wa Sheria ya Baraza la Usalama la Taifa wa Mwaka 2009 (*The National Security Council Bill, 2009*).

Hati ya Matumizi ya Nyongeza ya Mwaka 2010 (*Supplimentary Appropriation Bill, 2010*) iliwasilishwa, ikajadiliwa na kupitishwa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu lilijadili na kupitisha Maazimio sita. Maazimio hayo ni yafuatayo:-

(i) Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kahawa wa Mwaka 2007 (*The International Coffee Agreement - ICA, 2007*);

(ii) Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa kuhusu Kulinda Haki Miliki za Wagunduzi wa aina Mpya za Mimea (*The International Convention for the Protection of New Varieties of Plants*);

(iii) Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Jinsia na Maendeleo ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*) wa mwaka 2008 (*SADC Protocol on Gender and Development*);

(iv) Azimio la Bunge la Kuridhia Mapendekezo ya Mabadiliko katika baadhi ya vipengele vya Mkataba ulioanzisha Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF*);

(v) Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kuanzishwa kwa Kamisheni ya Maji ya Bonde la Mto Zambezi (*The Agreement on the Establishment of Zambezi Water Course Commission – ZAMCOM*); na

(vi) Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Ulinzi wa Pamoja wa Nchi za SADC (*The SADC Mutual Defence Pact*).

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu, pia Bunge lako Tukufu lilipokea Taarifa ya Utekelezaji wa baadhi ya Maazimio ya Bunge kutoka kwa Kamati mbalimbali za Kudumu za Bunge kama ifuatavyo:-

(i) Taarifa ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu athari za Mazingira katika Mgodi wa North Mara;

(ii) Taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini kuhusu Taarifa ya Serikali ya Utekelezaji wa Azimio la Bunge kuhusu mchakato wa Zabuni ya Kuzalisha Umeme ulioipa ushindi Kampuni ya *Richmond Development Company LLC*; na

(iii) Taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini juu ya Taarifa ya Serikali kuhusu Ubinafsishwaji wa Mgodi wa Kiwira.

Mwisho, Bunge lako Tukufu lilipokea Kauli ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji kuhusu Utekelezaji wa Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini; na Kauli ya Serikali ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko kuhusu Taulo za Kike Bandia aina ya *Always*.

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie fursa hii, kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kazi nzuri mliyoifanya katika kujadili na kupitisha Miswada, Maazimio na Taarifa za Kamati mbalimbali zilizowasilishwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 94 ya Kanuni za Bunge, Toleo la Mwaka 2007, katika Mkutano huu wa Kumi na Nane, Bunge lilikaa kama Kamati ya Mipango, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mwongozo wa Utayarishaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha 2010/2011 hadi 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati, Waheshimiwa Wabunge wote waliotoa michango yao mizuri na ushauri ambao Serikali itauzingatia wakati wa maandalizi ya Mpango wa Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2010/2011. Napenda kuwahakikishia kuwa, Serikali inathamini sana michango ya Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa ndiyo Wawakilishi wa Wananchi na sote tuna dhamana kubwa ya kuwahudumia Wananchi wetu na kukidhi matumaini yao.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha hivi karibuni tumeshuhudia Maafa mbalimbali yakitokea, lakini kubwa ikiwa ni Mafuriko yaliyotokana na Mvua kubwa zilizonyesha katika baadhi ya maeneo Nchini. Baada ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania kutoa tahadhari hiyo mapema mwaka jana, Serikali ilichukua hatua mbalimbali kwa lengo la kuzuia au

kupunguza athari za Maafa. Hatua hizo ni pamoja na kuitisha Mikutano ya Wadau wa Maafa, kuandaa mikakati ya kukabiliana na mvua hizo ili kupunguza Maafa Nchini. Mikutano hiyo ilishirikisha Waratibu wa Maafa wa Wizara, Mikoa, Mashirika na Taasisi za Serikali na Binafsi, Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa, pamoja na Vyombo vya Habari. Katika Mikutano hiyo, maelekezo ya kuandaa mikakati na tahadhari kwa lengo la kupunguza athari endapo Maafa yangetokea, yalitolewa. Aidha, Taarifa kwa Umma kupitia Vyombo vya Habari zilitolewa. Taarifa hizo ziliainisha hatua za kuchukuliwa na wanaohusika katika utekelezaji, sawa na Mwongozo wa Taifa wa Kudhibiti Maafa unavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, madhara makubwa ya Maafa yaliripotiwa kwa mara ya kwanza baada ya kunyesha mvua kubwa iliyosababisha Maporomoko ya Ardhi katika Wilaya ya Same mnamo mwezi Novemba 2009. Baada ya hapo, taarifa za Maafa ziliendelea kupokelewa kutoka katika Mikoani ya Kagera (Muleba); Morogoro (Kilosa na Morogoro Vijijini) na Dodoma (Kongwa, Mpwapwa, Chamwino) na Iringa (Idodi).

Mheshimiwa Spika, katika maeneo yote yaliyoathiriwa na Maafa kwa viwango mbalimbali, Kamati za Maafa za maeneo husika zimefanya kazi nzuri ya kukabili Maafa hayo. Aidha, Serikali ilihakikisha kwamba, misaada iliyotolewa na Wadau walioguswa na Maafa hayo, inasimamiwa na kuratibiwa vizuri. Kwa ujumla kwa mvua zilizokwishanyesha mwishoni mwa mwaka 2009 na mwanzoni mwa mwaka 2010, Wilaya ya Kilosa, Mkoani Morogoro, ndiyo ambayo imeathiriwa zaidi na mvua hizo, ikifuatiwa na Wilaya ya Mpwapwa, Mkoani Dodoma. Wananchi wengi wamekosa makazi na watu watatu walifariki. Aidha, Miundombinu ya Barabara na Reli ndiyo ambayo imeathirika zaidi na pia baadhi ya Shule zimebomoka. Ofisi ya Waziri Mkuu inaendelea kuratibu na kukabili Maafa hayo kwa kutoa misaada mbalimbali na kusimamia zoezi la kukabili Maafa hayo hadi hapo hali itakaporudi katika hali ya kawaida katika maeneo hayo.

Pamoja na vifaa mbalimbali, hadi sasa jumla ya Tani 237 za Mahindi toka Wakala wa Hifadhi ya Taifa zimetolewa na Serikali kusaidia katika Maafa hayo. Aidha, Shilingi Milioni 200 zimetolewa kwa ajili ya Operesheni ya Kutengeneza Nyumba za Waathirika na Shilingi Bilioni 3.2 zimetolewa kwa ajili ya kuanza kukarabati Reli na Barabara.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mvua kubwa ambazo zimesababisha madhara na Maafa makubwa yaliyotokea na ambayo yameleta hasara ya muda mrefu ujao, ni muhimu sana Mikoa na Wilaya zote Nchini kujiandaa, kuzuia na kukabiliana na Maafa wakati wowote yanapotokea. Mvua za Masika zinatarajiwa kunyesha katika muda mfupi unaokuja. Pamoja na mvua hizo, majanga mengine yoyote yanaweza kutokea sehemu yoyote katika Nchi yetu. Hivyo, ni wajibu wa kila Mkoa/Wilaya kuweka mipango madhubuti yenye lengo la kuzuia, kujiandaa kukabiliana na Maafa. Ofisi ya Waziri Mkuu itaendelea kutoa mafunzo kwa Kamati za Mikoa ambazo bado mafunzo hayo hayajatolewa. Vilevile, itaendelea kutoa tahadhari dhidi ya majanga yanayoweza kutokea. Hata hivyo, tumejifunza kuwa, Kitengo cha Maafa, Ofisi ya Waziri Mkuu, hakina uwezo wa kukabiliana na Maafa yanapokuwa ni makubwa na mengi. Kwa hiyo, Serikali itaangalia upya muundo na uwezeshaji wa Kitengo hiki kwa Wataalam, fedha na vifaa ili kiweze kukabiliana kwa ufanisi zaidi na matukio ya Maafa.

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii kupitia Bunge lako Tukufu, kutoa shukrani nyingi za dhati kwa wale wote waliotupatia misaada mbalimbali kutoka Ndani na Nje ya Nchi katika kipindi hiki cha Maafa. Kwanza, ninawashukuru sana Wananchi mmoja mmoja na kila mmoja kwa nafasi yake katika kusaidia kwenye Maafa haya. Aidha, nivishukuru Vikundi mbalimbali vya hapa Nchini, zikiwemo Taasisi mbalimbali, Makampuni kama VODACOM na CLOUDS FM, Madhehebu ya Dini, BAKWATA, CCT, Chama cha Msalaba Mwekundu Nchini na *Tanzania Insurers Association* kwa misaada yao.

Ninawashukuru kwa namna ya kipekee, Jeshi la Wananchi wa Tanzania, ambalo limefanya kazi nzuri na ambayo wanaendelea kuifanya hivi sasa katika Ujenzi wa Miundombinu iliyoharibiwa na mvua Mkoani Morogoro na Dodoma. Nawashukuru Viongozi mbalimbali, Waheshimiwa Wabunge, Madiwani na Wananchi wote walioathirika na Maafa haya, kwa uvumilivu wao na moyo wao wa kusaidiana na ninawasihi waendeleo kuvumilia na kuvuta subira katika kukabiliana na hali ngumu waliyonayo wakati Serikali ikiendelea na juhudi za kukabiliana nayo.

Vilevile, yapo Makampuni na Mashirika ya nje ya Nchi ambayo yametoa misaada yao kwa wakati kama vile UNICEF, WFP, USAID na DFID. Shukrani za pekee ziende kwa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa Libya, Serikali ya Marekani na Serikali ya Ufaransa, kwa misaada yao ya fedha na vifaa mbalimbali walivyotuletea kwa wakati muafaka ili Taifa letu liweze kukabili Maafa haya makubwa. Wote tunasema ahsanteni sana.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*Agricultural Sector Development Programme - ASDP*) inasimamiwa na Wizara za Sekta ya Kilimo, Chakula na Ushirika; Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; Viwanda, Biashara na Masoko; Maji na Umwagiliaji; na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI). Aidha, inashirikisha Sekta Binafsi, Wakulima, Wafugaji na Wafanyabiashara. Serikali za Mitaa zinatekeleza *ASDP* kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*District Agricultural Development Plans – DADPs*). Kutokana na utekelezaji wa *DADPs*, *ASDP* inatekeleza Sera ya kupeleka Madaraka kwa Wananchi (*D by D*), kwa kupeleka karibu asilimia 75 ya Bajeti ya *ASDP* Wilayani na Vijijini na kwa kuwashirikisha Wananchi katika kupanga na kutekeleza Miradi yenye kipaumbele kwao.

Mheshimiwa Spika, wajibu wa Serikali za Mitaa katika kutekeleza *ASDP* ni pamoja na kuandaa na kusimamia Mpango wa Utekelezaji wa *DADPs* kwenye Vijiji kwa Awamu (*Village Phase out Plan*).

Mpango huu unahimiza Halmashauri kuchagua Vijiji vichache vitakavyoanza kutekeleza *DADPs* katika Awamu ya Kwanza kwa kuibua na kupanga miradi michache ya kuongeza tija kwenye uzalishaji wa mazao na mifugo. Aidha, unahimiza miradi ya kuongeza kipato ikijumuisha usindikaji, maghala, masoko na barabara za vijijini ili kuwezesha walengwa kuwa na soko la uhakika pamoja na kuongeza kipato.

Wizara za Sekta ya Kilimo zimekwishatoa Mwongozo (*DADPs Planning and Implementation Guideline*), kwa Halmashauri zote za Wilaya Nchini ambao unaelekeza kwa kina:-

(i) Utaratibu wa kuchagua Vijiji vya kutekeleza *DADPs* kwa Awamu;

(ii) Jinsi ya kuwezesha Vijiji vilivyopo kwenye Mpango wa kutekeleza *DADPs* Awamu ya Kwanza kuandaa mipango ya maendeleo ya Kilimo ya Vijiji;

(iii) Kuzingatia vipaumbele vya Kilimo na Mifugo wakati wa kupitia mchakato wa fursa na vikwazo kwa maendeleo;

(iv) Stadi za kuandaa Andiko la Miradi ya Uwekezaji katika Kilimo ngazi ya Kijiji kwa kuzingatia manufaa ya Mradi, gharama ya Mradi, michango ya Walengwa, athari za mazingira na uendeleu wa Mradi;

(v) Utaratibu wa kuchagua Timu za Wawekezaji za Wilaya na Kata na kuzifanya kuwa za kudumu na kuongezwa Wataalamu wa ununuzi, mazingira na fedha;

(vi) Jinsi ya kuwashirikisha Walengwa katika kusimamia manunuzi, kutekeleza na kutathmini matokeo ya *DADPs*;

(vii) Kuzingatia matumizi sahihi ya ruzuku za maendeleo ya Kilimo wakati wa kuandaa mipango ya Bajeti na wakati wa utekelezaji, ikiwa ni pamoja na kuelekeza kiwango cha ruzuku kitakachotengwa kutekeleza miradi kwa kila Kijiji.

Mheshimiwa Spika, nimelazimika kuyaeleza haya kwa kina ili kuwawezesha Wananchi kujua kwamba, Mpango huu unawalenga wao wenyewe na kazi ya Halmashauri ni kuhakikisha elimu inawafikia ili waweze kuibua miradi ambayo itawanufaisha.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza *DADPs*, Serikali za Mitaa zinawajibika pia:-

(a) Kusimamia, kufuatilia na kuratibu utekelezaji wa Miradi ya *DADPs* kwa kuzingatia vigezo vya ubora, hususan miradi ya ujenzi na matumizi mazuri ya fedha (*Financial Management*);

(b) Kusimamia upatikanaji wa Zana za Kilimo kwa Vikundi vya Wakulima kwa vikundi hivyo kuchangia Asilimia 20 ya gharama;

(c) Kuongeza uwezo na kasi ya utekelezaji wa *DADPs* kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya fedha, kama vile mapato ya ndani (ushuru wa mazao), *TASAF* na Ruzuku ya Maendeleo ya Halmashauri, kwa lengo la kuongeza kasi ya maendeleo kwa Wananchi na pia kuongeza uwezo wa mapato ya ndani kwa kuwa sehemu kubwa ya mapato hayo yanatokana na shughuli za Kilimo na Mifugo; na

(d) Kutenga Maeneo Maalum ya Ardhi (*Land Bank*) kwa ajili ya uwekezaji, uzalishaji na biashara.

Mheshimiwa Spika, ili kuwa na usimamizi wa karibu wa uandaaji na utekelezaji wa Miradi ya DADPs, Waratibu wa ASDP katika ngazi ya Mkoa wameteuliwa na kuwezesha kifedha. Yafuatayo ni majukumu ya Sekretariati za Mikoa:-

(a) Kushiriki, kusimamia na kuhakikisha kuwa DADPs zinaandaliwa kutokana na Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Kijiji (*Village Agricultural Development Plans – VADPs*);

(b) Kuwezesha Vijiji vinavyotekeleza DADPs kuwa na Andiko la Mradi lililochambuliwa kwa vigezo vya faida kifedha, kiuchumi na kijamii, pamoja na matumizi sahihi ya Ruzuku za DADPs;

(c) Kuhakikisha wakati wa kuandaa mipango na Bajeti za Halmashauri ubora wa Miradi ya DADPs unazingatiwa na matumizi sahihi ya ruzuku za DADPs yamezingatiwa;

(d) Kusimamia matumizi ya fedha za DADPs kulingana na Mipango Kazi ya kila Halmashauri; na

(e) Kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa Miradi ya DADPs kwa kuzingatia vigezo vya ubora vilivyowekwa.

Napenda kutumia nafasi hii kuiagiza Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika; Mifugo na Uvuvi; Maji na Umwagiliaji; Viwanda, Biashara na Masoko; Maliasili na Utalii, kushirikiana vizuri na Serikali za Mitaa kutekeleza Mipango iliyopangwa katika ngazi zote kuanzia Vijijini, Wilayani na Sekretariati za Mikoa, kwa kuzingatia Mwongozo uliotolewa.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mifugo bado ina nafasi kubwa katika kujenga uchumi imara wa Taifa katika kuongeza kipato kwa Watanzania, hususan kuzalisha chakula, kutoa ajira na kuhifadhi Rasilimali za Taifa. Takwimu za Hali ya Uchumi mwaka 2008 zinaonesha Nchi yetu inayo idadi kubwa ya mifugo wakiwemo ng'ombe milioni 19.1, mbuzi milioni 13.6, kondoo milioni 3.6, nguruwe milioni 1.6 na kuku milioni 56. Aidha, kuna Rasilimali kubwa ya Ardhi ya Malisho ambayo inakadiriwa kuwa hekta milioni 60. Asilimia 40 ya eneo hili kwa ajili ya malisho, sawa na hekta milioni 24 lina tatizo la wingi wa ndorobo, hivyo kuacha asilimia 60, sawa na hekta milioni 36 ya eneo la ardhi hiyo kuwa ndiyo inayofaa kwa malisho.

Nchi yetu pia ina hali nzuri ya hewa inayofaa kwa ufugaji katika Kanda mbalimbali; Masoko ya uhakika ya ndani na nje ya Nchi; na Wataalamu wenye ujuzi na Elimu ya Asili kuhusu Mifugo; na kuna Sera nzuri za kiuchumi. Upatikanaji wa watu watakaoweza kufunzwa, pamoja na gharama nafuu za utendaji kazi.

Hivyo, zipo fursa za maeneo mengi ya kuwekeza katika Sekta ya Mifugo, ikiwa ni pamoja na kuwekeza katika kuanzisha mashamba makubwa ya mifugo (Ranchi); mashamba ya mbegu bora za malisho; viwanda vya kusindika mazao ya mifugo, viwanda vya kuzalisha vyakula vya mifugo, pembejeo za mifugo na kuanzisha machinjio ya kisasa.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mifugo ikiendelezwa inayo fursa ya kuongeza Mapato ya Serikali kwa kiwango kikubwa. Hivi sasa Mapato ya Serikali kutokana na Sekta ya Mifugo

yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka. Kwa mfano, katika kipindi cha miaka minne iliyopita, Mapato Serikalini yameongezeka kutoka shilingi milioni 740.2 mwaka 2005 hadi kufikia shilingi bilioni 1.1 mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio haya katika Sekta ya Mifugo, bado ziko Changamoto zinazoikabili Sekta hii. Changamoto hizo ni: Kasi ndogo ya utangaji wa maeneo ya ufugaji na kuijengea miundombinu; Uzalishaji duni na tija ndogo ya mifugo hasa ya asili; Ukosefu wa masoko ya uhakika; kuwepo kwa magonjwa mbalimbali ya mifugo; uhaba wa viwanda vya kusindika mazao ya mifugo; uwekezaji mdogo katika sekta ya mifugo; kutokuwepo kwa taasisi za mikopo zenye masharti nafuu; na upatikanaji na gharama kubwa za pembejeo za mifugo.

Jukumu kubwa la Serikali ni kuhakikisha kuna mikakati mahususi ya kukabiliana na changamoto hizi, hususan kuimarisha uzalishaji wa mifugo na mazao yake kwa kuhamasisha uwekezaji katika Sekta; na kuimarisha Vituo vya Ukaguzi wa Mifugo. Napenda kuiagiza Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kuhakikisha kwamba, haya yote yanatekelezwa kulingana na Mipango tuliyojiwekea sasa ili sekta hii nayo iweze kutoa mchango wake kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, tarehe 16 hadi 18 Desemba, 2009 tulikuwa na Mkutano wa Wadau wa Sekta ya Uvuvi uliofanyika Jijini Mwanza. Lengo la Mkutano huo lilikuwa kuhamasisha usimamizi na matumizi endelevu ya Rasilimali za Uvuvi Nchini chini ya Kaulimbiu ya “Kilimo Kwanza”.

Moja ya jambo muhimu lililojitokeza katika Mkutano huo ni kuwa Nchi yetu ina rasilimali kubwa ya mazao ya uvuvi, ambayo inahitaji kulindwa, kuhifadhiwa, kuimarisha usimamizi na kutumiwa kwa uendelevu kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vijavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Nchi yetu imejaliwa kuwa na Rasilimali kubwa ya Samaki na Viumbe wengine kwenye maji. Tanzania ni Nchi pekee ya Afrika inayozungukwa na maziwa yote makuu matatu, yaani Ziwa Victoria lenye kilometa za mraba 68,800, ambapo Tanzania inamiliki asilimia 51 (kilometa za mraba 35,088); Ziwa Tanganyika lenye Kilometa za Mraba 32,900 ,ambapo Tanzania inamiliki asilimia 41 (Kilometa za Mraba 13,489) na Ziwa Nyasa lenye Kilometa za Mraba 30,800 na Tanzania inamiliki asilimia 18.51 (kilometa za mraba 5,700).

Zaidi ya hayo, Nchi yetu ina eneo la Bahari limegawanyika katika Maji ya Kitaifa (*Territorial Sea*) yenye kilomita za mraba 64,000 na eneo la Bahari Kuu (*Deep Sea*) lenye Kilometa za Mraba zipatazo 223,000. Pia, yapo Maziwa ya kati na madogo 29, mabwawa mengi ya asili na ya kuchimba na maeneo ya ardhi oevu (*wetlands*).

Mheshimiwa Spika, katika Sekta hii ya Uvuvi, zipo pia fursa nyingine kama vile:-

(i) Kuwepo kwa rasilimali za uvuvi ambazo hazijavunwa vya kutosha kwenye maji ya kina kirefu na kwenye Ukanda wa Uchumi wa Baharini;

(ii) Fursa za kuanzisha Viwanda vya Uchakataji wa Samaki na mazao mengine ya uvuvi kwa lengo la kuongeza thamani kwa ajili ya Soko la Ndani na Nje;

(iii) Uwekezaji kwenye ukuzaji wa viumbe hai kwenye maji, uzalishaji wa mbegu za samaki na mimea inayokuzwa kwenye maji; na vyakula vya samaki na ufugaji samaki;

(iv) Uwekezaji katika Viwanda vya Kati vya kusindika mazao ya mwani;

(v) Uwekezaji katika Miundombinu ya kupokelea samaki;

(vi) Uwekezaji katika Viwanda vya kutengeneza zana na pembejeo za uvuvi na ukuzaji viumbe kwenye maji; na

(vii) Kuwepo kwa maeneo yanayofaa kwa utalii ikolojia na samaki wa mapambo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa ya Mwaka 2008, katika kipindi cha miaka minne iliyopita, 2005/2006 – 2008/2009, Sekta ya Uvuvi imechangia kwa kiwango kikubwa katika Pato la Taifa, ambapo imeweza kuingiza shilingi bilioni 1,041. Huu ni mchango mkubwa kwa maendeleo ya Nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyoonekana katika kipindi hiki, Sekta ya Uvuvi imekuwa na changamoto zifuatazo: kukomesha Biashara Haramu ya Uvuvi na mazao yake; kuongeza idadi ya Maafisa Uvuvi kwenye Halmashauri; kuongeza uwekezaji katika Sekta ya Uvuvi; kuwa na Bandari za Uvuvi zenye miundombinu kwa ajili ya kutega uchumi wa Bahari Kuu; kudhibiti uharibifu wa mazingira ya maeneo ya Uvuvi; na kuimarisha ulinzi wa rasilimali za uvuvi katika Bahari Kuu (EEZ) na mipakani na kwenye mialo kwa kutumia BMUs.

Mheshimiwa Spika, ipo orodha ndefu ya Mikakati ambayo imewekwa kukabiliana na changamoto hizi, ikiwemo Mkakati wa kudhibiti Uvuvi Haramu wa Mazao ya Uvuvi kwa kuimarisha doria na kuongeza vituo vya doria.

Aidha, Serikali imeweka Mkakati wa kuanzishwa kwa Benki ya Takwimu (*Database*) ya Maduhuli ya Nchi nzima yatokanayo na Rasilimali za Uvuvi. Ninapenda kuchukua nafasi hii, kuiagiza Wizara ya Mifugo na Uvuvi kusimamia kwa karibu maeneo ambayo tayari Serikali imeazimia na kuanza kuyatekeleza. Kwa mfano, Uvuvi Haramu ni kero kwa Wananchi na ni tatizo kubwa. Wito wangu kwa Wananchi wote na hasa Wavuvi ni kuwataka kuachana kabisa na Uvuvi Haramu, kwa sababu unasababisha uharibifu mkubwa wa Rasilimali za Majini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuhimiza ukuzaji wa viumbe hai kwenye maji kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa samaki na mazao mengine ya majini ili kuinua Pato la Taifa. Kwa sasa kuna mabwawa 14,746 ya samaki aina ya perege na mabwawa 63 ya samaki aina ya mwatiko na visima 9 vya samaki aina ya *trout*. Uzalishaji unakadiriwa kuwa ni wastani wa tani 2.7 za perege kwa hekta. Hata hivyo, kutokana na ukame, idadi ya mabwawa kwenye maji baridi imepungua kutoka mabwawa 14,746 na kufikia mabwawa 10,210. Jumla ya mabwawa 4,536 yamekufa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hali hii ya uzalishaji wa samaki, bado kuna changamoto kubwa zinazokabili ufugaji wa viumbe kwenye maji. Changamoto hizi ni pamoja na:-

(a) Upatikanaji wa Vifaranga vya Samaki na Vyakula vya Samaki na Viumbe wengine kwenye maji;

(b) Halmashauri kuajiri Wataalamu wa kutosha, upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya miundombinu ya uzalishaji, uchakataji, uhifadhi na usambazaji wa samaki na mazao ya uvuvi;

(c) Upatikanaji wa taarifa za masoko na elimu kwa Wananchi kuhusu manufaa ya ufugaji na ukuzaji wa viumbe kwenye maji; na

(d) Upatikanaji wa wagani wa aina hii ya ufugaji.

Serikali itahakikisha inaweka mikakati ya kukabiliana na changamoto hizi. Napenda kutumia nafasi hii, kuwahimiza Watanzania wote kuanza kutilia maanani ufugaji wa samaki na ukuzaji wa viumbe majini (*Aquaculture*). Nawaagiza Wakuu wa Mikoa na Wilaya zote kuwahimiza Wananchi kuchimba mabwawa ya kufuga samaki ili kujipatia kitoweo na hatimaye kupata lishe bora na kujiongezea kipato.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Nyuki nayo ina umuhimu mkubwa katika kuchangia ukuzaji wa Pato la Taifa, kuleta maendeleo na kuondoa umaskini katika jamii. Kuna jamii nyingi za Watanzania zinazotegemea Sekta hii kwa maisha yao ya kila siku. Ni kutokana na hali hiyo, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005, Kifungu cha 34(c) hadi (d) inasema kwamba, katika kipindi cha miaka mitano, Serikali itachukua hatua za kuongeza msukumo katika kuendeleza ufugaji nyuki kwa ajili ya kuzalisha asali na nta kibiashara na kuvutia Wawekezaji katika kuanzisha viwanda vya kuchakata asali na nta.

Vilevile, kuna Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki ambayo inajumuisha pamoja na mambo mengine, mabadiliko ya kijamii na kiuchumi yaliyofanywa na Serikali katika kuhimiza Sekta Binafsi kukuza uchumi. Lengo likiwa ni kuimarisha mchango wa Sekta ya Ufugaji Nyuki katika Maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, inakadiriwa kwamba, Tanzania ina rasilimali za ufugaji nyuki zenye uwezo wa kuzalisha mazao ya nyuki kufikia takriban tani 138,000 za asali zinazokadiriwa kuwa na thamani ya shilingi bilioni 184 na tani 9,200 za nta yenye thamani ya shilingi bilioni 24 kwa mwaka. Kwa sasa wastani wa uzalishaji ni tani 5,600 za asali, zenye thamani ya shilingi bilioni 14.5 na tani 379 za nta zenye thamani ya shilingi bilioni 1.04, ambazo huzalishwa nchini kwa mwaka.

Hata hivyo, takwimu zinaonesha kwamba, hii ni asilimia tano tu ya uwezo (*Potential*) wa uzalishaji. Hata hivyo, kati ya tani hizo 5,600 za asali inayozalishwa hapa Nchini ni tani 477 tu ndizo zinazosafirishwa kwenda nje ya Nchi, ambazo ni sawa na asilimia 11 ya asali inayozalishwa. Kiasi chote cha nta kinachozalishwa husafirishwa kwenda nje.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa hii ni dhahiri kwamba, kama Sekta hii ikipewa kipaumbele na Wadau wote, inayo nafasi ya kuchangia kwa kiasi kikubwa katika kukuza uchumi, kupunguza umaskini na kuongeza Pato la Taifa. Kinachojitokeza ni kwamba, soko la asali na nta lipo ndani na nje ya Nchi.

Napenda kutumia fursa hii kutoa wito kwa Wananchi kujitokeza kwa wingi kuanzisha mashamba ya ufugaji wa nyuki kwa ajili ya matumizi ya hapa Nchini na zaidi kusafirisha nje ya Nchi. Naitaka Wizara ya Maliasili na Utalii ijipange vizuri ili iweze kupeleka Wataalam maeneo ya ufugaji kuwasaidia Wananchi kutumia mbinu za kisasa katika ufugaji ili kuongeza tija na uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, kama zilivyo kwa Sekta nyingine, Sekta ya Nyuki inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(a) Ufugaji wa nyuki bado haufuati Kanuni na utaalamu wa kisasa. Wataalam wanasema kuwa zaidi ya asilimia 99 ya shughuli za ufugaji nyuki Tanzania, hufanywa na Wafugaji wa Jadi ambao idadi yao inakadiriwa kuwa milioni mbili;

(b) Matumizi ya zana duni katika ufugaji wa nyuki na urinaji wa asali yamechangia sana katika kupunguza kiwango cha asali na nta kinachozalishwa na pia kupunguza ubora wa asali;

(c) Kutokana na kutumia njia za jadi katika ufugaji wa nyuki, kuna uharibifu wa mazingira na hasa misitu ambayo inategemewa sana kwa ajili ya ufugaji. Vilevile, uchomaji ovyo wa mioto umechangia sana kupunguza ufugaji wa nyuki na hatimaye kupungua kwa uzalishaji wa asali na nta;

(d) Ubovu wa miundombinu kwenye maeneo ya uzalishaji na uchakataji, pamoja na upungufu wa Wataalam wa Ugani. Upo upungufu pia wa vitendea kazi na nyenzo za uzalishaji za mazao ya nyuki; na

(e) Sekta hii haijapewa kipaumbele stahiki aidha na Serikali au hata Sekta Binafsi. Ni imani yangu kwamba, Mheshimiwa Waziri Mama Mwangunga, atayachukulia yote haya kwa uzito unaostahili na kutoa kipaumbele kinachostahili ili tuweze kweli kuwasaidia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto hizo, ninafuraha kusema kuwa, bado Tanzania imeendelea kuzalisha Asali na Nta yenye ubora wa viwango vinavyokidhi mahitaji ya Soko la Nchi za Nje. Vilevile, pamoja na kuwepo kwa masharti magumu kuhusu kukidhi viwango vya ubora katika Soko la Kimataifa hasa katika Soko la Umoja wa Nchi za Ulaya, wafugaji nyuki wameweza kuzalisha mazao yenye ubora unaokubalika na kuuzwa katika masoko hayo.

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii kutoa wito kwa wenye hoteli na maduka makubwa (*Supermarkets*), wanunue asali inayozalishwa na Wananchi wetu kwa bei nzuri kama sehemu ya kutimiza wajibu wao kwa jamii (*Corporate Social Responsibility*). Vile vile, juhudi zinahitajika kwa Asasi zote zinazojikita katika ufugaji nyuki kuhamasisha vijana, wanawake na wananchi wengi zaidi ili waweze kushiriki kikamilifu katika shughuli za ufugaji nyuki. Lengo ni

kutumia fursa hii ya ufugaji nyuki na biashara ya mazao ya nyuki katika kuboresha maisha yetu na kuongeza Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Kilimo, inayojumuisha Mazao/Mifugo/Uvuvi/Nyuki katika Tanzania ina mchango mkubwa katika Uchumi wa Taifa. Sekta inaajiri asilimia 80 ya Watanzania wenye uwezo wa kufanya kazi na inachangia takriban asilimia 27 ya Pato la Taifa. Pamoja na umuhimu wa Sekta ya Kilimo Nchini, hali ya uwekezaji kwenye Sekta hii bado ipo chini ukilinganisha na Sekta nyingine kutokana na kutokuwepo kwa Vivutio vya Kutosha vya Uwekezaji. Kwa mfano, kati ya mwaka 1990 – 2008, uwekezaji katika Sekta ya Kilimo umekua kwa asilimia 6 tu, ukilinganisha na uwekezaji katika Sekta ya Mawasiliano asilimia 17, Ujenzi asilimia 17 na katika Sekta ya Madini ambao ulifikia asilimia 26.

Mheshimiwa Spika, takwimu hizo zinaonesha kuwa Sekta ya Kilimo, bado haijanufaika sana na uwekezaji wa moja kwa moja kutoka Nje ya Nchi (*Foreign Direct Investment - FDI*), pamoja na Wawekezaji wa Ndani ya Nchi. Kutokana na hali hiyo, Serikali hivi sasa inaendelea na mchakato wa kuangalia vivutio vingine zaidi ambavyo vitawavutia Wawekezaji ili kuongeza uwekezaji katika Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi na Nyuki kwa ajili ya mauzo ya ndani lakini vilevile na mauzo ya nje.

Kwa upande wa vivutio vinavyotokana na Sera za Kodi (*Tax Incentives*), pamoja na Sekta ya Kilimo kwa ujumla kusamehewa kodi mbalimbali, bado Sekta hii inatozwa Kodi na Ushuru kwenye ngazi ya uwekezaji na uzalishaji badala ya kutoza kodi kwenye faida. Maeneo yanayoangaliwa kwa upande wa Vivutio vya Sera za Kodi ni pamoja na Ushuru wa Mazao, Kodi ya Ardhi, Kodi ya Ongezeko la Thamani – VAT, Kodi ya Mapato na Ushuru wa Forodha katika maeneo yenye ushindani.

Aidha, kwa upande wa Vivutio visivyo vya Kodi (*Non Fiscal Incentives*), Serikali inaangalia uwezekano wa kuandaa Sera na Sheria zitakazojenga imani na kuwezesha Wawekezaji wengi kupenda kuwekeza kwenye Sekta ya Kilimo hasa katika kupata Mikopo, upatikanaji wa ardhi, upatikanaji wa pembejeo, kuboresha mifumo na miundombinu ya soko ili kukidhi mahitaji ya wazalishaji. Nimeiajiza Wizara ya Fedha na Uchumi kwa kushirikiana na Wizara za Kilimo, Chakula na Ushirika; Mifugo na Uvuvi; Maji na Umwagiliaji; Maliasili na Utalii; Viwanda, Biashara na Masoko; Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na Kituo cha Uwekezaji (TIC), kufanya kazi haraka kuangalia maeneo yote ambayo yanahitaji kuboreshwa ili ikiwezekana bajeti ijayo tuweze kupata baadhi ya manufaa yatakayotokana na kuwepo kwa vikwazo katika uwekezaji katika sekta hii.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa ambayo inarudisha nyuma maendeleo ya Sekta zote hizi za Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Nyuki ni ukosefu wa Miundombinu, ikiwa ni pamoja na Barabara, Bandari, Reli na Mashine za Barafu (*Storage Facilities*), lakini vile vile umeme. Ni dhahiri maendeleo ya Sekta hizi yanategemeana sana. Kwa maana hiyo, changamoto kubwa ni namna ya kuboresha Barabara zetu, huduma za Bandari na Reli kwa ajili ya usafirishaji wa mazao ya Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Nyuki.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa tumefanya vizuri katika Sekta ya Barabara. Kwa mfano, katika kipindi cha kuanzia Desemba, 2005 hadi Desemba, 2009, Serikali imefanikiwa kizifanyia

matengenezo jumla ya kilomita 19,549 katika kiwango cha lami na kilometa 19,858 kwa kiwango cha changarawe katika Barabara Kuu. Katika Barabara za Mikoa, jumla ya kilomita 1,979, zilifanyiwa matengenezo katika kiwango cha lami na kilometa 68,900 katika kiwango cha changarawe. Kuhusu ujenzi na ukarabati wa Barabara Kuu na Mikoa, jumla ya kilomita 359.18 za Barabara Kuu zilifanyiwa ukarabati katika kiwango cha lami na kilomita 1,106 zilijengwa katika kiwango cha lami.

Aidha, jumla ya kilomita 121 za Barabara za Mikoa zilijengwa kwa kiwango cha lami na kilomita 3,114 zilifanyiwa ukarabati kwa kiwango cha changarawe. Pia, jumla ya madaraja 50 katika Barabara za Mikoa yalijengwa.

Mheshimiwa Spika, nimetoa mfano wa ujenzi wa barabara, lakini Serikali inafanya juhudi za kuboresha huduma kwa upande wa Sekta ya Bandari, Reli na Viwanja vya Ndege, ambapo tutahakikisha tunaboresha huduma za Sekta hizo ili ziwe kichocheo cha uzalishaji katika Sekta za Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Nyuki.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kero wanazopata Wananchi, Wawekezaji na Wafanyabiashara, kutokana na mifumo ya huduma na taratibu katika maeneo ya kuanzisha biashara na miradi ya uwekezaji, matumizi ya rasilimali hususan nyumba na ardhi kama amana za kibiashara na urasimu katika mifumo ya usafirishaji. Serikali inatekeleza mchakato wa kuboresha mazingira wezeshaji ili kuendeleza Sekta Binafsi kwa kuzingatia mabadiliko yanayojitokeza Ulimwenguni, kuhamasisha urasimishaji wa Wawekezaji wa ndani na kuvutia Wawekezaji wa Kimataifa katika Dunia ya Utandawazi.

Mheshimiwa Spika, mbinu zinazotumika ni kurahisisha taratibu wanazopitia Wadau wa Sekta Binafsi kupata huduma zinazoweza kuendesha shughuli za kiuchumi kihalali na kwa ufanisi. Huduma husika ni pamoja na upatikanaji wa leseni na vibali mbalimbali vya kuendesha biashara na shughuli za kiuchumi; upatikanaji wa Hati Miliki za mali za kudumu; upatikanaji wa mikopo; kukomboa mizigo bandarini na usafirishaji barabarani. Maeneo mengine yanajumuisha matatizo ya miundombinu muhimu, usuluhishi wa migogoro ya kibiashara na mfumo wa Sheria na Soko la Ajira.

Mheshimiwa Spika, lengo kuu ni kuwezesha Wawekezaji kupata Leseni na huduma za kuanzisha na kufungua biashara kwa muda mfupi na gharama ndogo kabisa. Utekelezaji wa Mpango huu upo katika awamu mbili. Awamu ya kwanza inahusu maboresho yanayoweza kufanyika katika Muda Mfupi, yanayolenga kurekebisha Kanuni na Taratibu. Katika upeo wa Muda wa Kati, lengo ni kurekebisha Sheria husika na kujenga uwezo wa Asasi na Taasisi zinazosimamia utekelezaji ili kufanikisha malengo ya kuwepo kwa Sheria hizo bila kusababisha kero kwa Wananchi na kuathiri Wawekezaji. Vile vile, Serikali inaendelea na juhudi za uboreshaji wa miundombinu muhimu ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Barabara za Lami, upanuzi wa Viwanja vya Ndege, Uendeshaji wa Bandari na Reli.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza kutoa Hati Miliki za Kimila kwa Wananchi wanaomiliki Ardhi Vijijini chini ya Mradi wa Majaribio unaohusisha Wilaya 15 na utekelezaji umekwishaanza katika Wilaya za Babati, Bariadi, Namtumbo, Manyoni na nyinginezo. Katika Wilaya ya Babati mashamba 15,287, katika Vijiji 9, yametambuliwa na Hati 12,937

zimeandaliwa. Katika Wilaya ya Bariadi mashamba 18,141 yametambuliwa, Hati 15,205 zimeandaliwa na Hati 13,402 zimetolewa kwa wanaomiliki mashamba hayo. Mchakato wa kutambua mashamba katika Vijiji vingine 15 Wilayani Babati unaendelea na vipo Vijiji vingine 22 Wilayani Bariadi umeanza. Lengo ni kutambua mashamba yote na kutoa Hati Miliki za Kimila kwa Wanavijiji wote, Babati na Bariadi na katika Vijiji vinane katika Wilaya 13 zilizosalia kwa kuanzia, kama mbinu ya kujenga utaalamu na uzoefu wa kufikisha huduma hii kwa Watanzania wote katika muda muafaka.

Mheshimiwa Spika, zipo faida ambazo zimeanza kuonekana wazi kabisa katika upatikanaji wa Hati Miliki. Kwa mfano, Wakulima wa Mbozi wamefanikiwa kupata mkopo wa shilingi bilioni 10 kwa ajili ya kuendeleza mashamba yao. Aidha, upatikanaji wa Hati Miliki za Kimila unawasaidia Wakulima kuboresha maisha yao na maeneo mengine inapunguza ugomvi wa mara kwa mara wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, Urasimishaji wa Makazi yaliyojengwa kiholela katika Jiji la Dar es Salaam na la Mwanza unaendelea. Katika Jiji la Dar es Salaam, maombi ya Leseni za Makazi 91,169 yamepokelewa baada ya kukamilisha maandalizi husika na Leseni 90,000 zimetolewa. Mpaka sasa, Wadau 611 wametumia Hati zao kama Amana ya Mikopo ya Benki. Katika Mji wa Mwanza, jumla ya makazi yasiyo rasmi 17,061 yametambuliwa na Leseni za Makazi 280 zipo katika mchakato wa maandalizi na 180 zimekwishatolewa. Viwanja vilivyopimwa katika Jiji la Mwanza ni 3,395.

Mheshimiwa Spika, napenda kusesitiza kuwa, Wadau wakubwa katika jukumu la kuhamasisha na kuvutia Wawekezaji kwa kujenga mazingira wezesaji ni Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Mamlaka hizi zitafanikisha jukumu hili kwa kubadili fikra na mitazamo yao iliyoganda kuhusu Uwezesaji wa Sekta Binafsi na hivyo kuchukua hatua za kuangalia upya Kanuni na Taratibu za Kiutawala zinazohusu Sekta Binafsi na kubadili Sheria husika na hata kufuta au kuondoa Kanuni na Taratibu zinazokwamisha Wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, tunalo jukumu kubwa la kutunza mazingira yetu, kwani ni rasilimali pekee inayoweza kuamua mustakabali wa uhai wa Binadamu na maendeleo yake. Shughuli mbalimbali za kiuchumi zisizo endelevu ndani na nje ya Nchi yetu zimekuwa chanzo kikubwa cha majanga ya kimazingira kama athari za mabadiliko ya tabianchi na upotevu wa bioanuai. Hapa kwetu uharibifu mkubwa wa mazingira unatokana na ufyekaji misitu, uchomaji moto ovyo (mioto vichaa), uchimbaji madini usio endelevu, ufugaji na kilimo kisicho endelevu pamoja na utupaji ovyo wa taka kutoka viwandani na majumbani.

Mheshimiwa Spika, maisha ya kila siku ya Wananchi yanategemea sana ubora wa mazingira, hivyo juhudi za kuondokana na umaskini ni lazima zizingatie Hifadhi ya Mazingira ili ziweze kuzaa matunda yanayotarajiwa. Kwa ujumla uharibifu wa mazingira unadumaza juhudi za Serikali katika kuleta maendeleo endelevu. Hivyo ni lazima kila mmoja wetu kwa nafasi yake, ashiriki katika jitihada za kuzikabili changamoto za uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza Sheria na Mikakati mbalimbali ili kukabiliana na uharibifu wa mazingira Nchini. Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004, inaendelea kutekelezwa kwa kuhusisha Wadau wote katika ngazi mbalimbali. Kila Wizara

tayari imeteua Mratibu wa Mazingira ambaye husimamia shughuli za Hifadhi za Sekta. Aidha, kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), takriban asilimia 90 ya Halmashauri zimeteua Waratibu wa Mazingira kama Sheria inavyoelekeza na tayari wameanza kutekeleza majukumu yao kwa kushirikiana na Kamati za Mazingira za Wilaya. Kupitia Bunge lako Tukufu, nakiagiza kila Kijiji kiwe na Kamati ya Mazingira kama Sheria inavyoelekeza ili kuongeza ushirikishwaji wa jamii nzima katika shughuli za Hifadhi ya Mazingira kwa ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya tabianchi kwa sasa ni changamoto kubwa inayotukabili. Kwa siku za karibuni, tumeshuhudia ukame wa mara kwa mara na wenye athari kubwa katika maeneo mbalimbali ya Nchi yetu kama vile Wilaya za Ngorongoro na Longido. Aidha, mafuriko yameathiri Wilaya za Kilosa na Mpwapwa na tumeshuhudia maporomoko ya ardhi katika Wilaya ya Same na kuna ushahidi unaoonesha kina cha bahari kuongezeka. Haya ni baadhi tu ya madhara ambayo yameanza kujitokeza na kwa kadiri Joto la Dunia linavyozidi kuongezeka, madhara haya yatakuwa makubwa zaidi. Nimeagiza Ofisi ya Makamu wa Rais, Idara ya Mazingira, wahakikishe wanatoa Elimu ya kutosha kwa Wananchi ili wafahamu madhara haya na mikakati ya kukabiliana nayo. Vilevile, ni vizuri Wananchi wakafahamishwa fursa zilizopo katika utunzaji wa Mazingira hasa zitokanazo na utekelezaji wa Miradi ya kupunguza Gesi Joto.

Mheshimiwa Spika, katika utunzaji wa mazingira, ushirikishwaji wa Wananchi ni muhimu sana. Wananchi wanalo jukumu kubwa la kuhifadhi Mazingira ili kujihakikishia maendeleo endelevu. Kwa muktadha huu, Elimu ya Mazingira pamoja na uhamasishaji wa Wananchi katika kuhifadhi mazingira yao ni muhimu sana. Tuzo ya Rais ya Kuhifadhi Vyanzo vya Maji, Kupanda na Kutunza Miti Nchini inayoratibiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais itaanza kutolewa katika Kilele cha Siku ya Mazingira Duniani tarehe 5 Juni 2010. Tuzo hii inalenga kuwahamasisha Wananchi washiriki katika kutunza na kuhifadhi mazingira. Natoa wito kwa Wananchi wote kuongeza juhudi katika kuhifadhi na kutunza Mazingira kwa ajili yetu na vizazi vijavyo. Jambo la msingi ni kuhakikisha kwamba, elimu, uhamasishaji na matumizi ya Sheria vinakuwa na nafasi kubwa katika kuinua kiwango cha mafanikio ya shughuli za Hifadhi ya Mazingira. Ni muhimu haya yakasimamiwa na Viongozi katika ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, tathmini iliyofanywa mwaka 2009 na Shirika la Umoja wa Mataifa kuhusu Kupambana na Rushwa (*United Nations Convention Against Corruption 2003 – UNCAC*), kwa kushirikiana na Serikali za Uingereza na Uholanzi kuhusiana na Mapambano dhidi ya Rushwa Nchini, imeonesha kwamba, Tanzania ni Nchi inayopambana na Rushwa kwa dhati. Aidha, Tanzania ndiyo Nchi pekee Barani Afrika, ambayo imekamilisha mchakato wa tathmini hiyo ya Shirika la Umoja wa Mataifa kuhusu Kupambana na Rushwa. Rushwa katika Nchi yetu iko zaidi katika utoaji huduma kwa jamii na utoaji kandarasi. Aidha, Rushwa ipo katika Chaguzi hasa za Ndani ya Vyama vya Siasa, Taasisi na Asasi ambazo Uongozi unapatikana kwa njia za Uchaguzi hususan Uchaguzi Mkuu. Mara zote Rushwa inalenga zaidi katika mapato ya kifedha na rushwa ya zawadi.

Mheshimiwa Spika, katika mapambano dhidi ya Rushwa, Serikali imezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ambayo ni kuimarisha Utawala Bora na kujenga utamaduni wa uwajibikaji katika jamii ifikapo mwaka 2025. Kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Namba 11 ya Mwaka 2007, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ina

majukumu makuu yafuatayo: Kutoa Elimu kwa Umma kuhusu Rushwa; kuzuia Rushwa; na kupambana na Rushwa.

Mheshimiwa Spika, kama Tafiti mbalimbali zinavyoonesha, mafanikio katika kupambana na Rushwa yametokana na kuzingatia utekelezaji wa Lengo Namba 3 la Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Rushwa Awamu ya Pili (*NACSAP II*), unaosimamiwa na TAKUKURU. Mambo ambayo yametekelezwa ni pamoja na:-

(i) Kuanzisha Kamati za Uadilifu 260 katika Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Halmashauri za Wilaya, Miji na Majiji. Kamati hizo zimepata mafunzo juu ya majukumu yao na hivyo kuweza kusimamia kikamilifu suala la Rushwa na Maadili katika maeneo yao ya kazi;

(ii) Waheshimiwa Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Waheshimiwa Majaji wa Mahakama Kuu, Wahadhiri wa Vyuho Vikuu ambao kwa nyakati tofauti wamepatiwa mafunzo kwa ajili ya semina mbalimbali ya Miundombinu ya Maadili yanayohusiana na sehemu zao za kazi kwa lengo la kuchochea na kujenga uadilifu katika Vyombo hivi muhimu;

(iii) TAKUKURU imeendelea kutoa Elimu ya Rushwa kwa jamii kwa kutumia Vyombo vya Habari, machapisho na shughuli nyingine za kijamii katika ngazi ya Kitaifa, Mkoa na Wilaya. Katika kipindi hiki jumla ya semina 2,595, midahalo 155 na mikutano ya hadhara 2,211 ilifanyika;

(iv) Klabu za Wapambanaji wa Rushwa 2,030 zenye Wajumbe 178,142 zimefunguliwa katika Shule za Sekondari Nchini kote kwa kipindi cha Januari hadi Desemba, 2009 kwa lengo la kuanza kujenga fikra sahihi tangu wanapokuwa bado shuleni za kuchukua rushwa na kuzingatia maadili yao kwa Taifa letu.

(v) Hivi sasa TAKUKURU ina mtandao wake ikiwa ni njia mojawapo ya kusogeza fursa ya Wananchi kupata Taarifa mbalimbali kuhusiana na Rushwa;

(vi) Katika juhudi za Kupambana na Rushwa, hadi kufikia Januari 2010, Kesi 18 za Rushwa Kubwa (*Grand Corruption*) zilikuwa Mahakamani. Hivi sasa jumla ya kesi zote zilizoko Mahakamani Nchini kote ni 369; na

(vii) Kesi zilizofunguliwa Mahakamani kwa kipindi cha miaka minne iliyopita (2006 - 2009) ni 636, ambazo ni zaidi ya asilimia 49 ya kesi zilizofunguliwa Mahakamani kuanzia mwaka 1996 – 2005. Katika kipindi hiki fedha zilizookolewa ni shilingi bilioni 86.9.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo yanayotokana na utekelezaji wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, pia Serikali imeweza kuiimarisha TAKUKURU kwa kuiongezea watumishi na vitendea kazi ambapo katika kipindi cha mwaka 2006 – 2009, jumla ya watumishi 746 walijiriwa. Jengo la TAKUKURU Makao Makuu limekamiliwa na kuzinduliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Majengo ya Ofisi za Mkoa wa Temeke na Wilaya ya Maswa pia yamekamiliwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, majengo ya Ofisi za Mikoa ya Lindi, Manyara na Wilaya za Iramba na Mpanda yako katika hatua mbalimbali za ujenzi na yanatarajiwa kukamilika mwaka huu wa fedha 2009/2010.

Nitumie nafasi hii kuipongeza TAKUKURU kwa mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hiki cha utekelezaji wa majukumu yake. Wito wangu kwa Wananchi ni kuwaomba wote tutoe ushirikiano wa karibu kwa TAKUKURU ili iweze kutekeleza majukumu yake na hivyo kudumisha Utawala Bora Nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kulipongeza kwa dhati kabisa, Bunge lako kwa kuendelea kukemea vitendo vya rushwa na kuhimiza uadilifu katika utendaji kazi wa Watumishi wa Umma. Ninawashukuru pia kwa kuendelea kwa umakini mkubwa kutunga sheria zinazolenga kupambana na rushwa kama ilivyofanyika hivi punde katika Bunge hili ambalo tunamalizia, kwa kupitisha Muswada wa Sheria inayohusu gharama za uchaguzi ambayo kimsingi lengo lake kubwa ni kukabiliana na rushwa hasa katika ngazi za uchaguzi, wakati wa kura za maoni, kabla ya kura za maoni na wakati wa uchaguzi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, leo tunahitimisha Mkutano wa Kumi na Nane wa Bunge tukiwa tumebakiza Mikutano miwili tu kabla ya kuingia kwenye Uchaguzi Mkuu utakaofanyika mwezi Oktoba, 2010. Tunahitaji kujipanga vizuri na kuendelea kudumisha Amani, Utulivu na Mshikamano. Aidha, kwa kuzingatia changamoto mbalimbali ambazo zinatukabili katika kipindi hiki, mambo ya msingi ambayo ningependa kuyasisitiza ni haya yafuatayo:-

(i) Nchi yetu imekabiliwa na Maafa ya Mafuriko ambayo yameharibu Miundombinu ya Barabara na Reli kwa kiasi kikubwa pamoja na makazi ya watu. Naomba Wananchi wawe wavumilivu na wavute subira wakati Serikali inaendelea kukabiliana na changamoto hii;

(ii) Kaulimbiu ya Kilimo Kwanza ni kichocheo cha kuongeza kasi ya utekelezaji wa Mikakati ya Kitaifa ya kuendeleza Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Nyuki na kadhalika. Kila mmoja wetu tutumie Kaulimbiu hii kusukuma shughuli za kilimo. Tuwahimise Wananchi wajandae vizuri kwa kuandaa mashamba yao na kutumia vizuri mvua zilizopo;

(iii) Sekta ya Uvuvi ina fursa kubwa ya kuondoa umaskini kwa Wananchi wengi wa kipato cha chini. Viongozi wote katika ngazi za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa hawana budi kuchukua hatua za kuhimiza Wananchi kuibua miradi endelevu ya uvuvi, hasa ufugaji wa samaki. Vilevile, tupige vita uvuvi haramu katika maeneo yote yenye rasilimali za uvuvi.

(iv) Nchi yetu inayo nafasi kubwa ya uzalishaji wa asali na nta ambayo tukiitumia vizuri tunaweza kujenga uchumi imara na kuboresha maisha ya Wananchi wetu, hususan vijijini. Tutumie nafasi hii katika kukuza uchumi, kupunguza umaskini na kuongeza Pato la Taifa.

(v) Sekta ya Kilimo bado haijanufaika na uwekezaji wa moja kwa moja. Hata hivyo, zipo fursa za kutumia vivutio vilivyopo vinavyotokana na Sera za Kodi na zile zisizo za Kodi kwa lengo la kuongeza uwekezaji katika Sekta za Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Nyuki. Tuunge mkono juhudi za Serikali katika kuandaa mazingira mazuri yanayovutia Wawekezaji katika Sekta hizi.

(vi) Tunayo nafasi ya kutumia Hati Miliki za Kimila na Leseni za Makazi kwa ajili ya kupata mikopo ya biashara na kuendeleza mashamba ya Wakulima. Kila Halmashauri kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi iongeze kasi ya upatikanaji wa Hati Miliki na Leseni za Makazi ili kusaidia Wananchi wetu.

(vi) Uharibifu wa Mazingira unadumaza maendeleo. Ni vizuri Elimu ya Mazingira iendelee kutolewa kwa Wananchi ili kila Mwananchi ajue athari zinazotokana na uharibifu wa Mazingira. Kamati za Mazingira katika kila Kijiji zifanye kazi zake kama Sheria inavyoelekeza ili jamii ishiriki kikamilifu katika kulinda na kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuwashukuru tena wote waliotusaidia katika kufanikisha Mkutano huu. Shukrani za pekee ni kwako wewe Mheshimiwa Spika, kwa uongozi wako na umahiri mkubwa sana katika kuendesha shughuli za Bunge hili, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kukusaidia kuweza kuliongoza vizuri Bunge lako muda wote kama ambavyo mmekuwa mkifanya katika Mabunge mengine. *(Makofi)*

Ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yenu na hatimaye kukubali kupitisha Miswada mbalimbali na Maazimio yaliyowasilishwa katika Mkutano huu. Namshukuru sana Katibu wa Bunge na Wasaidizi wake, kwa huduma mbalimbali katika kufanikisha Mkutano huu. Wapo Wataalam wa Serikali, Madereva na Vyombo vya Habari ambao wote kwa pamoja ninasema ahsante sana kwa kutimiza wajibu wenu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, ninawatakia wote safari njema wakati mnaporejea katika Majimbo yenu, tuko katika hatua za lala salama na ninaomba kila mmoja wetu kila akipata nafsi asiache kukimbia kwenda Jimboni angalau kusema shikamoo kwa wagombea. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu liahirishwe hadi Siku ya Jumanne, tarehe 13 Aprili, 2010, saa tatu kamili asubuhi, litakapokutana hapa Mjini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa niaba yetu sisi Wabunge wote, kwa hotuba yako nzuri yenye maelekezo mazuri tu na mema ya kuiendesha nchi yetu. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na hasa wale mlioniandikia hapa, nimeigiza Idara ya *Hansard* ichapishe Hotuba hii ili muweze kugawiwa kila mmoja aweze kupata. Wale wanaoondoka leo pengine hatutawahi, lakini tunajua mahali pa kuwafikishia. Kwa hiyo, mtakuwa nayo kama Hotuba ya Rejea iliyo muhimu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, matangazo machache tu kuhusu ule msiba wetu; mwili wa marehemu mume wa Mheshimiwa Felister Bura, utawasili Dodoma leo jioni. Misa itafanyika kesho Jumamosi tarehe 13 Februari, 2009 saa 4.00 asubuhi katika Kanisa Katoliki la Parokia la Kiwanja cha Ndege.

Familia imekubali kutoa fursa wakati huo ya kuuaga mwili wa marehemu ili wale watakaokuwepo kesho waweze kufanya hivyo. Kwa sababu mazishi bado ni mbali kidogo, yatafanyika Jumatano tarehe 17 Februari, 2009 katika Kijiji Luanda Kiselu, Wilaya ya Rorya. Kwa hiyo, fursa ya kuagana na marehemu kwa kweli ni kesho na mwili utasafirishwa keshokutwa kwenda Musoma na baada ya hapo taratibu nyingine zitafuata kule Kijiji Luanda Kiselu, Wilaya ya Rorya.

Waheshimiwa, nakumbusha kwamba Wajumbe wa POAC na LAAC kesho saa 2.00 asubuhi kuna *forum* yenu ile ya siku mbili ya mashauriano. Kabla ya hapo, leo mara tukishaahirisha Shughuli za Bunge, naomba Wenyeviti wa Kamati hizo tukutane pale Ofisini kupokea vifaa kutoka kwa CAG wa Serikali. Kwa hiyo, tutoke hapa twende Ofisini kwangu tuweze kupokea vifaa. Hatuhitaji vigelegele kwa sababu tuna msiba.

Niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge Wanawake wote kwamba na wao mara tukitoka hapa, kuna Mkutano mfupi wa kuzingatia hali hii iliyomfika dada yetu Felister. Kwa hiyo, watakutana Ukumbi wa Pius Msekwa mara baada ya kutoka hapa. Kutokana na msiba huu, Mkutano wa Tume ya Utumishi ambao niliuitisha kesho saa 4.00 sasa umeahirishwa na mtaarifiwa baadae. Nadhani tutakifanyia Dar es Salaam kikao hiki chenye masuala muhimu yenye maslahi kwa Waheshimiwa Wabunge na Watumishi wa Bunge, naomba tukipata taarifa tuweze kuhudhuria ili tuyapitishe yaweze kuingia katika bajeti ya mwaka 2010/2011.

Baada ya matangazo hayo, kuna utaratibu katika Chama cha Mapinduzi unaitwa kutangaza nia, huwa unaudhi sana ikiwa wanaotangaza nia wanakusonga kwenye Jimbo. Sasa na mimi nimeona ni uungwana tu ili niweze kutangaza nia ya kugombea Uspika katika Bunge lijalo. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa dhati kabisa, mmekuwa walimu wangu kwa miaka mitano, mmenifundisha nimeizowea kazi hii. Nina hakika kabisa kwamba, mkinichagua kuwa Spika wa Bunge la Kumi, itakuwa bora zaidi kuliko ilivyokuwa. Hii ndiyo inaitwa kutangaza nia maana yake mtu usikae kimya kimya tu. Kwa hiyo, ninawashukuru sana kwa hilo, endeleeni kulikumbuka, nitawakumbusha tena baadae na wale wanaotaka kujaribu hii kazi ni ngumu kidogo, nimekaa kwenye Kiti hiki leo saa 3.00 asubuhi mpaka saa 9.00 mchana bila ya kuondoka; siyo jambo dogo hata kidogo. Ahsanteni sana. (*Makofi/Kicheko*)

Sasa nitakuombeni nyote tusimame kwa ajili ya Wimbo wa Taifa.

Samahani, nimeshabikia sana, Waheshimiwa Wabunge kaeni kwanza, nitawahoji mmesimama. (*Kicheko*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

WIMBO WA TAIFA

(Hapa Wabunge Waliimba Wimbo wa Taifa)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, pamoja na kuwatakia safari njema kwenda majumbani kwetu, natamka sasa kuliahirisha Bunge hadi Siku ya Jumanne, tarehe 13 Aprili, 2010, saa tatu asubuhi hapa Mjini Dodoma.

*(Saa 9.00 mchana Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne,
Tarehe 13 Aprili, 2010 Saa Tatu Asubuhi)*